# CONSITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LIKONI CONSTITUENCY, HELD AT LIKONI SECONDARY SCHOOL

**MONDAY, 2nd MAY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LIKONI CONSTITUENCY HELD AT LIKONI SECONDARY SCHOOL ON MONDAY 6th May 2002**

**Present**

Com. Zein Abubakar
Com. Prof. Wanjiku Kabira

**Secretariat In attendance**

Fatuma Jama - Program officer
Onesmus Kipchumba - Assistant program officer
Alice Thuo - Verbatim recorder
Nancy Odipo - Sign language interpreter

**The meeting was called to order at 10.15 a.m.**

**Com. Zein Abubakar:** Naomba amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe nanyi. Ningependa kutangaza kikao hiki kuwa ni kikao rasmi kwa minajili ya kukusanya maoni ya wakenya ili kurekebisha Katiba yetu. I would like to declare this officially as a sitting of the Constitution of Kenya Review Commission. It is a formal sitting for the purpose of collection of views of Kenyans with the purpose of reviewing our Constitution. Kwa ada za Tume ningeomba mshilikishi wa kazi ya Tume hapa Likoni atuanzie kwa dua halafu tutaendelea.

**Ahmed:** Kabla sijaongea juu ya jambo lolote na kama ada yetu, ningependa mwenyeji wetu Stan Seif atutilie dua kutufungulia mkutano wetu. Stan Seif.

**Stan Seif:** (Prayer in Islam).

**Ahmed:** Katika kikao chetu cha leo, ningependa kuwajulisha ma-commissioners ambao tuko nao. Kwa upande wangu wa mkono wa kulia ni Commissioner Abubakar Zein Abubakar. Na kwa upande mwingine ni Commissioner Prof. Wanjiku Kabira. Tunawakaribisha karibuni. Vile vile mimi ndiye msimamizi wa shughuli hizi za Tume (district coordinator) na niko na wasaidizi wangu, wanakamati tumegawanyika. Wengine wako hapa na wengine wanasimamia kituo cha Mtongwe. Hapa tuna Misi Juma. Tuna David Obelo pamoja na mimi sote watatu. Na waliobakia wako kituo cha Mtongwe. Kwa hivyo leo si siku yetu ya kusema. Leo ni siku yenu ya kuja kutoa maoni yenu. Na moja kwa moja nitawapeleka kwa Commissioners karibuni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Ahmed. Kwanza kabisa ningechukua fursa hii ya mbele kuwaomba radhi zenu utusame.

Kwa sababu tulikuwa tumewaita na kutaja kwamba tutafanya mkutano huu kwanzia saa mbili asubuhi. Sasa inaelekea saa nne na nusu na tunawaomba mtuwie radhi kwa sababu mbalimbali hatukuweza kuanza kwa muda tuliowaarifu kwamba tutaanza.

La pili ningependa kuwashukuru kwa kuonyesha uvumilifu mkubwa wa kusubiri mpaka sasa. Ningependa kumpa fursa kabla sijaendelea Professor Wanjiku Kabira awasalimie halafu nitaendelea kwa kuwatajia utaratibu tutakaotumia leo ili tuwe na nidhamu katika kutoa maoni. Halafu tutaenda moja kwa moja kuwaita watu waanze kutoa maoni yao. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Hamjamboni. Mimi pia ninauliza mtusamehe kwa sababu tumechelewa sana. Lakini tukianza tutafanya kazi kwa haraka na wale wanataka kuenda wataenda na wengine pengine watabaki na sisi. Lakini mtusamehe. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Professor Kabira. Utaratibu tukaoutumia ni utaratibu rahisi sana. Mlipokuwa mkiingia pale mlikutana na wale wasaidizi katika sehemu hii na walikuwa wakiandika majina ya watu. Majina haya ndio tutakayoyatumia kuwaita watu kutoa maoni yao. Kama ulijiandikisha kwamba wewe ni wa kwanza na wewe ndio utapewa fursa ya kwanza kuzungumza. Tutakaa kwanzia sasa mpaka saa kumi na mbili jioni. Ikifika saa kumi na mbili jioni, ikiwa bado kutakuwa kuna wakenya wanaotaka kutoa maoni yao, tutakaa mpaka tutakapomaliza. Au kukiingia kiza au giza tutashauriana tufanye nini.

Pili jambo la muhimu kujua ni kwamba ingawa nimesema tutatumia utaratibu huo, tutawaomba rukhusa zenu muafiki kwamba kukitokea sababu ya sisi kutengua kidogo utaratibu huu ili kutoa fursa kwa mtu anayestahiki kupewa fursa hiyo mtuwie radhi. Kwa mfano: Akaja bibi ambaye ni mja mzito, tutawaomba mtupe radhi tumpe fursa ya mbele afanye hivi. Sijui kama mnakubaliana na mimi? Akaja mtu mzee ambaye hawezi kuhimili kustahimili uchofu wa kukaa kwa muda mrefu, pia tutawaomba radhi tumpe fursa mzee kama huyo. Pia kukatokea mtu ambaye pengine ni mgonjwa ama ana dharura tuwaalifu kwamba dharura yenyewe ni hii na tuwaombe radhi tumpe mtu kama huyo fursa.

Jambo lingine la muhimu kufahamu ni kwamba kuna njia kadha za kutoa maoni. Unaweza kuwa wewe umekuja na ushaandika mambo yale unataka kutualifu sisi. Kwamba una mswada. You have a memorandum. If you have a memorandum, ikiwa una mswada utakuja hapa ufanye kati ya mambo mawili. La kwanza uwe unataka kutoa memorandum yako au mswada wako bila kuzungumza. Ukiwa wataka kufanya hivyo utakwenda kwa yule binti pale, utatoa memorandum yako uta-sign register kwamba umetoa memorandum.

La pili unataka pia kugusia na kuchambua kwa ufupi muhtasari wa mambo muhimu yaliyomo katika mswada wako. Hapo tutakupa dakika tano. Utumie ule mswada sio utusomee kila kitu. Lakini uchague yaliyo muhimu ndio wakenya wengine wafahamu mambo unayopendekeza wewe. Njia ingine ya kutoa maoni ni kwamba unakuja hapa na hujaandika lolote chini. Unataka kutoa oral submission au unataka kutoa maoni yako kwa kauli yako kwa mazungumzo peke yake. Ikiwa ni hivyo tutakupa dakika kumi utoe maoni yako. Ningependa kuwaomba wananchi watukufu kwamba itakuwa muhimu sisi ikiwa una

maoni yako wataka kuzungumzia shida tulizo nazo, ni sawa kuzungumzia shida. Lakini itakuwa bora zaidi ikiwa pia una mapendekezo shida hizo ama matatizo hayo yatatatuliwa vipi.

Mapendekezo: Kuna wakati mtanisikia mimi namuuliza mtu, je mapendekezo yako nini? Sio njia ya kumnyanyasa mtu au kumfanya afanye haraka lakini ni katika kutuongoza sisi katika kutoa mapendekezo. Jambo lingine la muhimu kufahamu ni kwamba unaweza kutumia Kiswahili katika kutoa maoni yako. Unaweza kutumia Kiingereza, na uweza kutumia lugha ingine yeyote ya Kenya. Lakini ikiwa unataka kutumia lugha ingine yeyote ya Kenya tafadhali mualifu mshilikishi wetu Bwana Ahmed. Kwamba mimi nataka kutumia lugha fulani. Hapo tutakuwa tumefanya mpango wa mtu kuja hapa na kutafsiri. Sijui kama tunafahamiana? Sawa?

Lingine la muhimu kufahamu ni nini? Sisi tumekuja hapa na wafanyikazi wengine wa Tume. Na ni muhimu kwenu kujua wafanyikazi hawa kazi yao ni nini. Sijui kama Bi. Fatuma kuna mobile microphone uanze kujitambulisha na kuwatambulisha wenzako. Lakini kiasi anatafuta microphone, ningependa tu kumtambua yule binti pale aliyevaa nguo ya pink. Njoo hapa mbele binti. Njooni hapa wote. Lakini ningetaka kutaja kazi ya huyu tu, hawa wengine watajitambulisha wenyewe. Huyu binti ni mtafsiri wa ishara (sign language interpreter). Ikiwa kuna ndugu zetu ambao ni walemavu hawasikii. Yeye kazi yake itakuwa kutafsiri mambo yanayoendelea hapa kwa ishara ili ndugu zetu hao wawe pamoja na sisi.

**Fatuma Jama:** Salam Alaikum. Kwa jina naitwa Fatuma Jama na mimi ni program officer.

**Alice Thuo:** Kwa majina naitwa Alice Thuo. Mimi ni verbatim recorder.

**Fatuma Jama:** Fatuma Jama, program officer.

**Nancy Odipo:** Naitwa Nancy Odipo. Sign language interpreter.

**Fridah Mwadime:** Hamjambo. Majina yangu ni Mrs. Fridah Mwadime. Mshilikishi wa mambo ya Tume wilaya ya Taita taveta.

**Com. Zein Abubakar:** Nadhani ndugu zetu kule nyuma wanaposema hawasikii hawasemi haya kwa uchokozi maanake ikiwa wanasema kwa uchokozi, itakapofika nafasi yako ya kuja kuzungumza na wewe utachokozwa hivyo hivyo. Sasa yule binti amesema yeye ni verbatim recorder. Pengine nifafanue kidogo kwamba kazi yake yeye ni ku-record kila neno litakalozungumzwa hapa kwa tape recorder. Atakuwa na tape recorder na zile cassettes mnazoziona atakuwa aki-record kila neno. Sisi tutakuwa tunachukua maandishi hapa. Saa ingine usione kwamba wazungumza na pengine siandiki wasema ‘ Commissioner vipi yule, mimi nasema maneno yeye hayaandiki.’ Kila neno litakuwa lina-recordiwa na ikisha-recordiwa haya tutayapeleka Nairobi yakaandikwe kama mswada neno kwa neno. Hatutaki hata neno moja lipotee.

Halafu Bi. Fridah pale atakuwa akiandika kwa mkono. Pia yeye atakuwa aki-record kwa mkono mambo haya. Halafu baadaye mtamwona kijana mwingine ambaye anaitwa Kipchumba atakuja pia naye aendeleee na kazi hiyo wapokezane kazi.

Jambo lingine la muhimu kufahamu katika kikao chetu na niko karibu kumaliza ndio kazi ianze. Kwamba mtu asiogope kwa jambo lolote kwamba utakalozungumza hapa hakuna hatua yeyote Mkenya anaweza kuchukuliwa kwa maneno ambayo atakayoyasema hapa. Watu hutuuliza 'je nikisema neno litamkasirisha mtu. Utakalo sema wewe ni lako wewe. Na ni muhimu sisi kufahamu katika kikao hiki kwamba mtu akija kutoa maoni yake hapa ni yake. Ikiwa hukubaliani na maoni yake subiri ifike fursa yako na wewe uje useme yako halafu useme sikubaliani na yule yule aliyesema hili na hili.

Lingine ni kwamba kuna watu watakuja kuzungumza maneno hapa halafu wewe uwe unakubaliana na maneno yale. Sisemi kwamba uache kuyasema maanake tumesema watu wengine wamesema yangu yashasemwa.Lakini hatujui yaliyosemwa ni yapi. Ikiwa unakubaliana na mambo hayo sema mimi nakubaliana na hili hili bila kulifafanua zaidi. Na ikiwa ufafanuzi uwe tofauti na ule mwingine. Sijui kama tunafahamiana.

La mwisho kabisa sisi watu wa pwani husema kwamba ni vizuri kuzungumza lugha ya murua. Nasema kweli useme lililo moyoni mwako lakini ni vizuri kutumia lugha ya murua. Na pia ni vizuri zaidi kwetu sisi mafunzo yetu yasema hata ukitaka kusema maneno magumu, utumie lugha laini. Au si sawa hivyo? Sasa la mwisho nilisema la mwisho kabisa nimekumbuka moja nilio sahau. Unaweza kuja hapa ukatoa maoni yako lakini sisi kama macommissioners twataka ufafanuzi. Sawa? Ikiwa twataka ufafanuzi mmoja wetu akiwa na swali utaambiwa subiri kidogo ujibu swali. Halafu utaulizwa swali halafu ujibu. Kuna mtu yeyote ana swali kabla hatujaanza. Ndio Mzee wangu.

**Speaker:** Niko na maswali mawili. La kwanza nauliza kama kutakuwa na kikao kingine kama hichi siku ingine. Swali la pili ni kwamba ikiwa leo mtu hakuweza kufika hapa na akatoa maoni, je anaweza kuasilisha mswada wake kivipi?

**Com. Zein Abubakar:** Swali lako la kwanza. Hakutakuwako na kikao kingine kama hiki siku ingine. Wakenya wanasema ' fanyeni kazi usiku na mchana mmalize kazi hii'. Kikao hichi ndio cha pekee. Lakini swali lako la pili lizuri linajalizia la kwanza kwa sababu bado……leo leo . Anauliza kama kuna siku ingine. Hakuna siku ingine lakini leo hapa hapa Likoni mahali kwingine kuna kikao kama hiki. Vinaendelea sambamba.

Swali lako la pili kwamba ikiwa leo haukutoa maoni au baadaye unataka kuongeza maoni yako, una ruhusa kufanya hivyo. Unaweza kututumia kwa sanduku letu la posta au pia unaweza kupeleka katika ofisi zetu za Mombasa ambazo ziko katika Kenya National Library hapa mjini Mombasa. Ukienda kumpa….kuna coordinators wawili huyu Bwana Ahmed au utupelekee pale ofisini tu uiwache pale.

Pia tuna address ya Mtandao ikiwa wataka kutumia au ukiwa uko Nairobi, tuko katika Kencom house second floor. Jumba la Kencom house ghorofa ya pili. Sasa ningependa kumuomba Sheikh Hassan apate fursa ya kwanza kutoa maoni yake. Sheikh Hassan tafadhali.

**Sheikh Hassan:** Salam Alaikum. (Islam). Kwanza napenda kutoa sikitiko yangu kwa kuwa ile Tume imechelewa sana kuanza kazi. Ijapokuwa tumeomba radhi lakini karatasi ni hii imesema saa mbili, saa mbili tumekuja leo ni siku ya kazi halafu saa nne na nusu inaanza baada ya masaa mawili na nusu. Ni sikitiko na hakika sisi wakenya tulikuwa na madhumaini makubwa kuwa Tume hii itarekebisha mambo lakini ikiwa mambo yao wenyewe hawakuweza kujirekebisha na wachelewa cha namna hii, hudhuufisha ile matumaini yetu. Kwa hivyo tunaomba mambo haya hakika si madogo yarekebishwe.

Jambo la pili, leo ni fursa kwangu mimi na kwa wakenya. Kwa kuwa tumepata nafasi ya kuulizwa Kenya mnayotaka iende namna gani? Baada ya Katiba iliyokuweko ambayo imetumika miaka arobaini, ambayo imetengeneza watu wachache, imepitisha watu wachache. Hii ni fursa kwetu sisi ikiwa tumeulizwa kusema ya kuwa ni Kenya gani tunayotaka na bila shaka ikiwa maoni yetu tunatoa kwa dhati na mambo tunayotaka tunaomba yazingatiwe. Tunataka yafuatiliwe ili tusipate taabu tena.

Nikianza kutoa maoni yangu, Katiba ya Kenya inasema Katiba ndiyo juu kuliko kila kitu. Mimi ningeomba Katiba kwa utangulizi iseme hivi: Katiba itakuwa chini za sheria za Mwenyezi Mungu kususha vitabu vilivyoteremsha Mwenyezi Mungu. Katiba ni kitu tumetengeneza sisi. Hata tukitengeneza kinamna gani haikosi kasoro ya hapa na pale. Lakini vitabu vitakatifu aliyeteremsha Mwenyezi Mungu (islam) mimi naamini ni kamili. Kama Koran karim au wenzetu wanaotumia Biblia. Kwa hivyo Katiba ya Kenya naomba kwa utangulizi ataje vipengele viwili hiyo ya kuwa ni Koran na Biblia haitapingana. Ihakikishwe kuwa sheria na Katiba itakayokuwako haitapingana na hizo vitabu viwili. Ikiwa Katiba itapingamana na vitu hivi viwili vifapilishwe.

Jambo lingine ambalo nataka kugusia ambayo inatuhusu zaidi sisi kama waislamu ni upande wa mahakama ya kadhi. Sisi tunapata taabu sana na tumepata taabu kwa mahakama ya kadhi. Sisi ni waislamu na lazima Katiba itutambue na Serikali pia kuwa sisi ni umma ambao wanasheria kamili ambayo haihitaji kuongezwa wala kupunguzwa. Kwa ajili hiyo kuwa tunaomba mahakama ya kadhi iwe na uwezo mkubwa ambayo inaweza kusikiza fadhia au kesi yeyote ambayo inahusu muislamu. Hiyo vile ilivyo hivyo sasa ya kuwa mambo ya talaka na ndoa na miradhi.

Tunataka mahakama ya kadhi iwe na uwezo zaidi, iweze kusikiza pavia ama malalamiko ama mashtaka yeyote ambayo inahusu sheria ya kiislamu kadhi aweze kusikiza. Kadhalika tunaomba ya kuwa mahakama ya kadhi ipanuke zaidi. Iwe kinyume ilivyo hivi sasa. Mahakama ya kadhi hivi sasa ni mahakama ndogo sana ambayo haina uwezo.

Kwa hivyo tunaomba mahakama ya kadhi igawanyike daraja tatu. Kuweko kadhi ndogo ambayo kesi ya mwanzo inaweza kusikiza ikiwa mtu hakuweza kuridhika ule uamuzi aliotelewa na kadhi waweza kwenda high court ambaye itakuwa vile vile katika mahakama ya kadhi ya chief kadhi. Ikiwa mtu hakuridhika kuweko court of appeal ambako kutakuwako wanachuoni

wa kiislamu wenye elimu na taaluma ambayo wanaweza kusikiza kesi kama hiyo. Tunaomba waislamu kesi ambayo inafika kwa mahakama ya kadhi katika daraja ya kwanza au ya pili au ya tatu, isiende tena katika mahakama nyingine yote kwa sababu ile ni madharau na ni kuvunja kwa sheria ya dini yetu.

Kwa hivyo tunataka mahakama ya kadhi iwe na nguvu ikianza kwa kadhi imalizike kwa kadhi. Ikiwa mtu hataki, yeye mwenyewe aende katika mahakama nyinginezo. Kadhalika sisi tunaomba kama waislamu na mimi nazungumza kama Imam, nazungumza kama mwanachama wa baraza la maimam. Sisi tunaomba uhuru ya dini kwa sababu mara nyingi tunaambiwa kuna uhuru ya kuabudu. Uhuru wa kuabudu ni mtu ikifika wakati wa sala akasali au ikifika wakati wa kanisa watu kuingia kanisa. Ikiwa pengine anaridhika hiyo sisi kidogo kwetu tuna uzito, kwa hivi leo tunataka uhuru ya dini.

Uhuru ya dini kwanza Serikali itambue waislamu na sheria yao. Mambo ambayo ni kinyume kabisa na sheria hii tukufu, Serikali isitulazimishe kwa njia yeyote iwe ni makosa kutulazimisha sisi mambo kama haya. Yeyote nasema ikiwa basi muislamu anaona ni makosa mali yake kuweka katika benki ama analipa riba awe ana uwezo wa kufungua benki za kiislamu ambayo haiendi na desturi kama hizo. Kwa hivyo tunaomba tueleweke kwamba sisi ni waislamu na mambo yetu ni kamili. Na mambo yetu yatambulike na tusilazimishwe mambo ambayo ni kinyume na dini yetu mambo ambayo hatukubali kwa imani yetu. Kadhalika tukisema uhuru ya dini, sisi waislamu mara nyingi tunaamini Serikali hii au Katiba iliyokuwako imetubagua ya kutosha ndio kwa ajili hii kila mahali leo tunajitokeza angalao Katiba itakayotengenezwa tupate nafuu.

Kwa hivyo ubaguzi ya kidini isiweko. Tukisema ubaguzi wa kidini ambao ni kinyume na uhuru ya dini. Kwa ikiwa muislamu atatengwa asipewe nafasi ya kusoma, asipewe nafasi ya kazi, asichaguliwe wadhifa kwa kuwa yeye ni muislamu hakika jambo kama lile linaweza kuleta hatari. Kwa hivyo sisi waislamu ni 30% katika idadi ya wakenya walioko. Kwa hivyo tunataka tupate haki zetu kulingamana na idadi yetu. Kila kitu tupate.

Ikiwa ni mawaziri tupate 30%, ikiwa ni Permanent Secretary tupate 30%. Ikiwa ni wakuenda nje kusomeshwa na Serikali tupate asilimia thelathini. Hatutakubali ile unyanyasaji na dhuluma ambayo hakika yatasababisha matatizo ya mara nyingi kutokeza na tunaona nchi zingine wenzetu za kiafrika ambayo mambo kama haya yatokea. Kadhalika kuna baadhi ya mambo ambayo ni kinyume na dini yetu na itikadi zetu ambayo tulikuwa tunataka iheshimiwe.

Mfano: Tunaona wakati watu wanaingia mahakama lazima watu wainame. Sasa kuinama huko sisi tunaamini ni kama purukuu. Ni kama yule anamwabudu. Unafanya kama kimungu anakaa. Kwa hivyo hatutaki mambo kama haya. Mimi sijui. Kama hiyo ni sheria iondolewe na ikiwa mambo kama hayo yataka kufanywa lazima waislamu waulizwe. Tume hii ikimaliza kazi yake mambo kama haya hatutafanya tena kwa sababu tusha eleza. Hatuwezi kufanya mambo kama haya au mengine judge anaiingia watu wote wanasimama. Kwa nini anasimama? Kwani yeye ni nani? Kwa hivyo mambo kama hayo tunapinga kwa sababu mtume wetu amekataa.

Hatutaki mambo kama haya katika mahakama ikiwa ni uadilifu, uadilifu ifanyike lakini yule judge asifanywe kama miungu. Na hakika ndiyo inafanyika. Ndio dhuluma mengi ambayo itakuweko. Jambo lingine ambao napenda kugusia ni tunasikia kwa hivi sasa kuna habufu* za watoto. Hakika ni nzuri na sisi kama waislamu tunaitambua haki ya mtoto. Toka azaliwe hata kabla hajazaliwa lazima umchague mama kisawasawa ambaye atakuzalia mtoto mzuri.

Lakini kuna mambo ambayo inaleta pingamizi. Hatukuwa tu waislamu tu, hata kwa wengine. Tunasikia kuna sheria inasema huna ruhusa ya kumuadhibu mtoto wako. Yaani huna ruhusa ya kumtia adabu mtoto wako ili kumuelekeza. Mambo kama haya italeta ufisadi na inaleta mashakeni. Nchi za wazunguni wamefanya na yako matatizo mengi. Mtoto amefura kichwa afanye analolitaka. Mtoto nimezaa namsomesha namlea Serikali kuniingilia mtoto usifanye hivi na hivi naona ni makosa.

Ikiwa kwenye kupiga ni kupitisha kiasi na kumdhulumu yule mtu haki yake mtoto haya ni mambo mengine. Lakini kumuadhibu kidogo hata kwa shule hata kwa skuli hata kwa madrasa sioni kama ni makosa. Narudia tena sisi mtume wetu (islam) asema ‘ waamrisheni watoto wenu Inshallah wakifika umri wa miaka kumi na saba’. ‘Na akifika miaka kumi, mtoto mpigeni. Fadhili huu huu mpigeni.

Sasa ni mtoto wangu mimi namwamrisha ajili ya sala. Ukinipeleka kortini eti nimepiga mtoto itakuwa namna gani. Kwa hivyo ni dhuluma na ni kuniingilia mimi uhuru yangu ndani ya nyumba yangu. Kwa hivyo tunataka mambo kama haya yasikuweko na tusiwe wakuiga wazungu wamefanya lazima tufanye. Hatuwezi. Sisi tuna desturi yetu, tuna mila yetu, tuna mienendo yetu mambo kama haya ni makosa yasizungumzwe wala yasijadiliwe wala yasiingiliwe.

Jambo lingine ambalo nataka kugusia kwa haraka haraka. (inaudible) ya zawadi hasa yale ya kuolewa ama kuoa. Sisi katika uislamu, msichana ikiwa amebarege nasema tena amebarege, amebarege miaka kumi na nne miaka kumi na tano, anataka kuolewa. Mimi nasema ni makosa mtu atoke aseme mtoto wangu hana ruhusa ya kuolewa ama kuoa. Hiyo ni uhuru yake yeye.

Sisi hakika tunauliza msichana mwenyewe kama anataka kuolewa na fulani, ikiwa amekubali makosa yako wapi na haya tunaona wazee wakipelekwa makortini, watu wakiteswa na hiyo naona ni makosa pia mambo kama haya. Na hatuyataki ile mambo kama haya. Kama Serikali kweli anataka kusaidia mtoto akiwa ameoa ama akiolewa aendelee na masomo.

Hapo itakuwa sawasawa maanake haimzuii ile jambo kama ile. Mtoto yuko Secondary kama mtoto hapa tumeona, ameolewa yuko form three aendelee, yuko form four aendelee. Ili kusiweko kizuizi au ameoa. Sasa ile imekuwa tayari wao wanazuia ile ambao hawatekelezi halafu wanaingilia mzazi, manyumba yake namna inavyokwenda ambayo haya ni makosa. Kwa hivyo kwa muhtasari hii ndiyo fikira yangu ambayo nilikuwa nataka kusema na nimekuja na wenzangu na tuna memorandum yetu ambao ndugu yetu Hassan atatoa. (kiislamu).

**Com. Zein Abubakar:** Shukrani Sheikh Hassan. Shukrani. Sheikh Hassan unahitajika kwenda pale kuandika jina kwamba

umetoa maoni yako kwenye register. Hiyo memorandum itatolewa na Sheikh Hassan. Sheikh Hassan tafadhali.

**Hassan Abdullah Hambigua:** Salaam Alaikum. Well I have the privilege to use the other national language English. So, I will highlight my proposals on behalf of (inaudible) Muslim Society.

**Com. Zein Abubakar:** Please give your name for the purpose of recording.

**Hassan Abdullah Hambigua:** Thank you. My full names are Hassan Abdullah Hambigua. Well these are the highlights of our proposals so they are not particularly from me but from my people. Proposal highlights. Kenya should adopt a regional or federal system of government rather than centralized which ensures marginalisation of smaller groups. A Kenyan citizen has the right to enjoy all that is provided for in the Constitution and has an obligation to ensure that the Constitution is enacted. We would propose that dual nationality be allowed.

Parliament should be given more power and involvement in defense and national security. In case Parliament fails three times to make a decision or significant issues for matters of national interest or public security. The Constitution should provide for an automatic referendum.

The Electoral Commission should be independent and seem to be independent. The Constitution should ensure that a ruling party cannot use state powers to destroy opposition. We should retain the Presidential system of Government but Presidential powers should be significantly be reduced. The post of regional leader should be introduced to lead each region as we are proposing a federal system of Government.

Every region should have its own regional Parliament and powers to manage and control its region. The Regional Parliament should have more powers than the leader alone. There should be a Regional and a National Parliament. Appointment of all high-ranking Government officers should be vetted and confirmed by Parliament not by the President. Anyone with questionable reputation or poor public record should not be accepted with the policy of 'one man one job'.

People should have the right to recall their MP incase of dissatisfaction of his performance. But only 75% of the votes that won him the seat should be able to disqualify. The concept of nominated MP's we propose should be retained but only vital professionals be appointed in such posts with representation from the youth, the women, and the disabled. Judiciary should be independent and every region participate in appointments which should only be confirmed by Parliament.

Kadhi's court should be more elaborate and powerful. The Mayor and council chairman be elected directly by the people and should have a five-year term. Constitution should protect security and provide healthcare, water, education, shelter, food, employment and basic rights for all Kenyans.

Education and health should be free and be seen to be free for all. Taxation should be relative. Lower for the poor and higher for the rich. Government should have powers to reclaim land acquired through improper methods and landowners should be clearly protected from land grabbers and (inaudible).

The pre-independence land treaties and agreement involving certain communities should be revisited and resolved according to the fair needs of such communities and the indigenous inhabitants. Kenyans ethnic and cultural diversity should be promoted but, and I insist but should not be allowed to threaten national unity. Therefore only national languages we propose should be used by officers in public offices both Government and private. The Controller and Auditor General should have adequate powers and access to Government offices.

All high-ranking officers should declare their wealth and assets. Constitution should ensure that industries are not established in residential areas and existing natural resources protected from grabbers. Constitution should protect ownership of natural resources discovered in personal owned property. Example is the 'Chairmen business or the Chairmen issue' and only purchased with mutual agreement with the owner.

The media and the press should be given freedom by the Constitution but misuse of such freedom should be punishable by law. There should be a special panel of professionals to advise the ministry of foreign affairs and all key foreign affairs policy be vetted by President. President should not have the final say. There should be no permanent commission. Only a small secretariat and appointment of such Commissioners should be appointed when a need arises. The Chief Justice should be incharge of Executive powers during Presidential election. He should be incharge of swearing in a new President.

The last issue I would like to talk about is the religious holidays. We currently believe as a minority people that the distribution of the religious holidays in this country are not equal or even proportional to the percentages given by statistics of people in this country and we would request that this matter be revisited by the Constitution. It should be openly addressed by the Constitution and we should not rely on Presidential directives. We have a more comprehensive memorandum which I will submit to the Commission. Thank you.

**Com. Zein Abubakar:** Thank you very much Hassan. The third speaker would be Athman Philip Ondasi. Uko? Karibu Mzee wangu.

**Athman Philip Ondasi:** Tume ya marekebisho ya Katiba. Katika maswali yenu mnauliza utangulizi. Sisi tunaona utangulizi kwanza Mungu atajwe, wananchi watajwe na mali asili yeyote mahali inapopatikana wananchi wafaidike nayo. Watu wote ndio wawe na uwezo wa mwisho. Juu ya kambi zote tekelezi; mahakama, bunge, wakenya wazingatie democracia juu ya uchumi, ardhi, makao, uhuru wa haki, usalama na mengineyo.

Mfumo wa Serikali: Tumeamua tunataka mfumo wa Serikali ama utawala wa majimbo. Tunataka majimbo ambayo Rais wa taifa atakuwa na sifa zifuatazo: Kwanza, Rais awe Mkenya mwananchi. Pili mwenye sifa na nidhamu za uongozi. Tatu, mwenye mali zinazofahamika alivyozipata. Nne, awe na umri wa kuanzia miaka arobaini na tano hadi sabini. Awe ameoa, awe na elimu isiopungua kidato cha nne au kuendelea.

Kuwe na Serikali. Kila jimbo liwe na Serikali yake ambaye Governor ndiye atakayekuwa kiongozi wa jimbo hilo.

Utawala: Serikali kuu igawanywe mamlaka na majimbo kuhusu yafuatayo. Kila jimbo litasimamia rasilimali zake zikiwa mali ya asili, kodi ama ushuru. Vitaendeshwa na kusimamiwa na majimbo yake yenyewe kibinafsi. Kama vile shule, uwajili, viwanda, ardhi, biashara, uridhi na mengineyo.

Bunge: Kila jimbo litakuwa na bunge lake na sheria zake za jimbo hilo bali na lile bunge kuu la taifa ambalo litawakilishwa na mabunge watakaokuwa kutoka kwa kila jimbo wasiopungua watano.

Bunge la taifa: Rais wa taifa awe mbunge. Mbunge awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea. Bunge liweze kupiga kura ya tulufu ya Rais. Bunge liwe na uwezo wa kudhibiti mali ya umma bila kupongwa. Bunge lifanye kazi kila siku. Bunge liwe na uwezo wa kuidhinisha ujira ya mkaguzi mkuu wa mali ya umma. Bunge liidhinishe vyovyote vile Rais atakavyochagua kama mabalozi wenye viti wakuu wa Serikali na kuwa na mashirika mengineyo na kadhalika.

Kuvunjwa kwa bunge: Uwezo wa kuahilisha na kuvunjwa bunge iwe ni wa Speaker wa bunge. Waziri Mkuu: Kuwe na Waziri Mkuu ambaye atagawana na Rais mamlaka. Jukumu lake litakuwa kuendesha shughuli zote za Serikali. Kuahilisha vikao vya bunge. Awe msemaji mkuu wa Serikali.

Rais na majukumu yake: Rais awe mkuu wa taifa. Rais atawakilisha taifa kimataifa. Rais atakuwa mfunguaji na mfungaji wa mikutano yote ya taifa.

Ukuu wa Katiba: Utaratibu wa bunge wa asilimia sitini na tano kuwa na uwezo wa kubadilisha Katiba uondolewe. Badala yake kwa vile Katiba imetungwa na wananchi, basi ni wao wao watakuwa kuwa na uwezo wa kubadilisha vifungo vyovyote pamoja na bunge. Kama bunge limeona ipo haja ya kifungo fulani ambacho kina dosari fulani ndio wananchi wahusike katika mikutano ya maoni kwa sababu ni wao ndio wahusika wakubwa. Ndio waliotunga na watakao fikia katika sehemu zote za Katiba. Mikutano hiyo ya maoni lazima iongozwe na Tume kuu ya marekebisho ya Katiba.

Uraia: Mkenya wa kuzaliwa mwananchi ndiyo mwenye haki ya uraia bila pingamizi. Utaratibu ulioko sasa wa kupeana uraia ubadilishwe. Lazima jamii ihusishwe katika kupitisha maombi hayo ili muombaji ajulikane mwelekeo wake au malengo yake

yafahamike. Ndio ule aliyezaliwa na mzazi mmoja mkenya na mgeni basi apewe uraia bila pingamizi.

Hakika majukumu ya uraia yatategemea vile uraia ulivyopatikana. Raia na haki zote za kimsingi na kidemocracia na kiuchumi na majukumu yake ni kudumisha amani nchini, kuheshimu mali, kulinda taifa, kustawisha uchumi. Katiba ikatae uraia wa nchi mbili.

Ulinzi na usalama wa taifa: Mamlaka ya kutangaza vita yawe ni jukumu la bunge. Katiba iruhusu Waziri Mkuu kuagiza mswada bungeni kuhusu janga la taifa kama vile vita, majanga, maasi na ukosefu kabisa wa usalama wa umma. Bunge lijadili liidhinishe majukumu hayo atakayo chukua Waziri Mkuu. Bunge ndio litakalo toa uamuzi na uwezo juu ya hali ya hatari.

Vyama vya kisiasa: Vyama vya kisiasa bali na kuhamanzisha umma visizughulishe na kuendeleza miradi ya kuyaletea maendeleo ya nchi kielimu, kiuchumi, kitaifa, kiafya na mengineyo. Katiba ielekeze uundaji, uongozi wa vyama vya kisiasa. Katiba itoe idadi maalum ya vyama vya kisiasa na vyama hivyo visizidi vitatu na visipungue viwili.

Shughuli za vyama vya kisiasa vighalamiwe na wanachama wake wala si pesa za umma kwa sababu zitaporwa. Kusiwe na haja ya kughalimia vyama vya kisiasa. Uhusiano kati ya dola na vyama vya kisiasa ni utekelezaji wa haki za binadamu na za kimsingi na maendeleo na kadhalika.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee Athmani dakika tano zimeisha ningeomba sasa uanze kufupisha. Unichagulie yale muhimu tu.

**Athman Philip Ondasi:** Kwa muhtasari? Hapa nimezungumzia muundo wa aina za Serikali. Tunataka muundo wa Serikali ya majimbo ambao mamlaka ya nchi inasimamiwa na bunge na mengineyo na kadhalika. Halafu bunge. Lazima bunge lihusishwe na vipengele vipige msasa na tarubini uteuzi wa viti vyote vya kikatiba.

Muundo wa utaratibu wa uchaguzi: Tufanye mfumo wa mseto katika uchaguzi. Tuendelee kuwa na mfumo ambao mwenye kura nyingi zaidi ndio mshindi.

Serikali ya mitaa: Wenyeviti wa mabaraza kama madiwani na ma-councillor wanafaa wachaguliwe na raia. Maana wao raia ndio wanaowaongoza si Serikali za wilaya.

Pili, Katiba iwapatie raia uwezo wa kurudisha Councillor au Mayor ikiwa atakosa nidhamu kwa kazi yake.

Mahakama: Muundo ulioko wa mahakama unatakikana marekebisho yafuatao: Majudge wa mahakama wasichaguliwe na Rais. Hata Judge mkuu wa Kenya asichaguliwe na Rais. Wote wachaguliwe kulingana na vile bunge litakavyopiga vipengele na elimu yao na ujuzi wa kazi wao walivyonavyo wawapigie kura wachaguliwe.

Haki za kimsingi: Masharti ya kimsingi ni kuhusu haki za kijamii. Katiba inapasa kutambua haki za watoto wanaokuwa na makundi walio wachache na walemavu.

Haki za ardhi na mali: Tunataka atakaye kuwa mmiliki wa mwisho wa ardhi awe ni jamii ya pale pale ambapo anaishi. Kwani yeye ndiye anajua mipaka na mahali alizaliwa na babu zake na babu yake. Serikali isiwe na uwezo wa kuchukua ardhi ya mtu binafsi kilazima kwa lengo lolote. Dola, Serikali kuu na Serikali ya mitaa.

Haki ya ardhi na mali: Vile vile tuna matatizo mengi ambayo yanatokana na ardhi. Mtu anaweza kusimama marekani, aka-apply ardhi hapa Kenya na akapewa ardhi hapa Mwambao raia ambao alikuwako mbeleni anafukuzwa kwa sababu mwenye kutoka Marekani amepewa title deed. Kwa hivyo mwenye cheti ndiye mmilikaji. Kifungo hivi tunaomba kibadilishwe.

Waheshimiwa ninashukuru sana kwa kutupa nafasi hii ya kuzungumzia mambo ya marekebisho ya Katiba. Wengi wao unaona tuko wanyonge hapa ni sababu ya Katiba tuliyo nayo. Kitu kama ardhi kuna wengine wamezeeka hajawahi kugusa title deed mkononi wala hawezi kwenda kuomba mkopo kwa benki akitumia title deed ya shamba lake. Hakuna. Haya yote yametuwezesha kuwa na unyonge mkubwa.

Kwa hivyo tunashukuru lakini hatujashukuru hatujaona kazi yenu. Siku tutakapoona kazi yenu ikitupa manufaa na kila mtu ataweza kumiliki mahali alipo, hatuna cha kuwapa isipokuwa tutatoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa Tume ya marekebisho ya Katiba. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Mzee Athmani. Bwana Mwinyi Ali. Tafadhali bwana.

**Mwinyi Ali:** Salam Alaikum wallah abdullahi wa barakadhi. Jina langu ni Mwinyi Ali na nimekuja kwa niaba yangu kwanza binafsi, pili kwa niaba ya miskiti ya Likoni na vile vile baraza la maimam katika Likoni division. Moja kwa moja naanza kutoa mapendekezo yangu. Mwanzo kulingana na utawala ama mfumo wa Serikali ambao tunaupenda ama twautaka sisi wakenya. Serikali tuliyo nao sasa mfumo wake ni ya umoja.

Yaani mambo yote yako hapo juu pamoja na kila kitu kitapitishwa hapo juu na yatakavyopitishwa hapo juu basi hakuna mwingine wa kuyatangua. Mfumo huo tumeona sisi umetuumiza kwa muda mrefu na sasa twasema twapendelea mfumo wa majimbo. Twapendelea mfumo wa Serikali *majimbo*. Kwa nini? Kwa sababu ndio tunaona tutaweza kupatikana uadilifu. Kila mtu ataweza kujua lile analolifanya na kile anachotaka ambacho anaweza kupata katika shughuli za Serikali yake anaweza akapata.

Jimbo litakuwa na bunge lake. Na liwe na sheria zake. Na liwe na askari wake. Liwe linaweza kusimamia mambo yake ya elimu. Liwe linaweza kusimamia mahospitali, mabarabara mambo mengi kama hayo katika kila jimbo. Na pia vile vile katika

Serikali za *majimbo* huwa kuna Serikali kuu. Kwa hivyo tunatarajia kuwa kutakuweko na Rais ambaye atakuwa amekaa juu ya Serikali ile kuu.

Lakini Rais huyu natoa mapendekezo ya kwamba atakapochaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano basi itakapomalizika kipindi chengine cha miaka mitano, Rais yule atoke jimbo jingine. Iwe hali ya mzunguko namna hii ili mradi katika kila jimbo katika Serikali ya Kenya liwe linaweza kupata utawala nao. Liweze kusimamia ule utawala wa Serikali ya jamhuri ya Kenya.

Bunge la taifa vile vile kama nilivyosema kutakuwa na Serikali kuu na vile vile kutakuwa na bunge la taifa ambalo litakuwa linawakilishwa na kila jimbo ama wilaya, wabunge watatoka katika hizo wilaya. Kwa hivyo wabunge wawe watachaguliwa na vizalia wa lile jimbo. Na atakaye simamia ubunge lazima awe ametoka katika……ni kizalia wa hilo jimbo hilo. Asiwe ni mtu kutoka pahali pengine halafu aje pale aweze kuchukua mamlaka hayo. Hataweza kujua matatizo ya wale watu. Kwa hivyo mbunge ni lazima awe ametoka, amezaliwa katika lile jimbo. Na watakao mchagua wawe basi pia ni vizalia wa hilo jimbo.

Na pia vile vile tunapendekeza kwamba mbunge ambaye atakwenda kinyume na mwongozo ama na matako ya watu wake basi Katiba iwaruhusu wale watu wake kumtoa kwa wakati huo atakapokosea.

Mahakama: Ikiwa kila jimbo litakuwa na mahakama tunapendekeza katika sehemu zetu hizi za Mkoa wa Pwani ambao majority ni waislamu, tunapendekeza mahakama ya kadhi. Mahakama ya kadhi iwe na mamlaka kamili. Kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu basi kuwe na ngazi kwanzia makazi wa chini mpaka wa juu wa high court. Na kusiwe tena zaidi ya high court kuwa kuna mwingine tena kwamba mtu kesi yake itakapo….pengine haikumridhisha, yeye aweza kukata appeal pahali pengine.

Mahakama ya kadhi iwe kamili. Kuanzia high court mpaka chini sub-ordinate court basi iwe ni kadhi moja kwa moja. Kwani kama kutatokea pahali pengine kwamba mtu hakuridhika na mahakama ya kadhi aende kukata appeal pahali pengine hiyo itakuwa ni kinyume na maongozi ya dini na itakuwa sheria za Mwenyezi Mungu zimedharauliwa. Na mwanadamu si kamili aliye kamili ni Mwenyezi Mungu kwa hivyo ni makosa kama tutakuwa tumedharau sheria za Mwenyezi Mungu.

Tulikuwa na uhuru wa kuabudu lakini tunasema sasa tunataka uhuru wa dini. Kwa nini? Dini kiislamu ni mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu. Kwa hivyo atakapopata uhuru wa dini mtu ataweza kukamilisha mambo yote ambayo yaliyomo ndani ya dini yake. Lakini kama kutapewa uhuru wa kuabudu peke yake basi atakuwa amefinywa na hajapata uhuru wa kisawasawa. Kwa hivyo tunayopendekeza tunasema tunataka uhuru wa dini ili mtu apate kukamilisha amri ama sheria za dini yake kikamilifu.

Kuna kumiliki ardhi: Leo kuna ardhi zile za watu binafsi na kuna ardhi zinazosemekana kwamba ni ardhi za Serikali. Lakini utashangaa, Serikali ikiwa ina miaka thelathini na nane ama arobaini. Kuna mtu anaishi katika ardhi ana miaka sitini ama sabini na yuko hapo kwa muda huo wote. Serikali na huyu mtu aliyetangulia ni nani? Itakuwaje leo huyu mtu aambiwe hiyo ardhi

anayoishi ni ya Serikali yeye ni squatter. Hapo lazima kuna uonefu hapo. Kwa hivyo twasema ardhi hizi ambazo zasemwa leo ni za Serikali na kuna watu wanaishi hapo kwa muda mrefu basi zipimiwe wale watu walioko waweze kuzimiliki ardhi hizo.

Vile vile kuna *u-squatter* wa watu binafsi. *U-squatter* wa watu binafsi ni yule mtu mwenye ardhi yake akawajengesha watu. Hawezi kuja akakupa ardhi tu hivi hivi jenga lazima utalipa. Halafu utaendelea kulipa pengine kila mwezi kila mwezi na umekaa hapo takriban miaka ishirini umejenga nyumba yako. Sasa ulilipa pesa kwanza ya kutosha pengine elfu arobaini, elfu hamsini kisha umeendelea kulipa pengine mia tano kila mwezi kwa muda wa miaka ishirini. Ni pesa ngapi? Kwa hivyo ni haki ya huyo mtu kupimiwa ardhi ile aweze kumiliki katika sehemu yake ile ya nyumba vile vile. Kama sehemu za mjini zilizofanyika.

Kuna mali asili: Kila pahali pana mali yake asili. Ardhi, kuna bahari, kuna sehemu nyingine zina madini, kuna sehemu nyingine zina misitu ambazo watu wanaweza kutoa mbao. Basi vitu kama hivyo vyote viwafae wale watajizalia wa pale mahali. Viwe vitaweza kuwafaa wao wenyewe. Leo watu wamekuwa maskini wa mwisho. Hatujijui, hatujitambui. Watoto wetu wamekuwa hawana elimu hatuwezi kumsongeza kijana yetu mbele kwa sababu ya umaskini. Hali tunazo rasilimali nyingi ambazo tunaweza kupata utajiri, tukawasomesha vijana wetu na kuendelea mpaka wakawa watu wa kisawasawa. Lakini tumekuwa watu wa hali ya chini.

Maskini tusiojiweza na hali uchumi tunao. Kwa hivyo zile mali asili ambazo tunazo ziweze kutufaa sisi vizalia wenyewe. Ikiwa ni bahari, ikiwa ni port, ikiwa ni misitu, ikiwa ni madini basi ziweze kutufaa sisi wenyewe. Kuna mambo kama ya mahoteli haya ya watalii hujengwa katika sehemu zetu lakini utakuta asilimia kubwa ya wale wanaofanya kazi katika mahoteli hayo si vizalia wa hapa. Kwa hivyo manufaa makubwa yanakwenda nje. Kwa hivyo twapendekeza yale mahoteli yanayojengwa hapa ya watalii na viwanda tunapendekeza kwamba percentage kubwa ya wale watakaoajiliwa wawe vizalia wa hapa.

Na pia vile vile hao wenye mahoteli na viwanda kuna faida wanapata kwa mwaka. Lazima kutoke asilimia fulani ibaki kwa wenyeji waweze kufanyia mambo yao ya kimji.

Elimu: Elimu kiislamu ni lazima. Mtume (islam) anasema (islam). Kuitafuta elimu ni lazima kwa muislamu mwanaume na muislamu mwanamke. Na pia vile vile ukiichunguza kimaisha, elimu ni chombo ambacho kinaweza kukuondolea umaskini. Ni chombo ambacho kinaweza kuondolea ujinga lakini leo Kenya elimu imekuwa ni chombo cha kuleta umaskini leo hii. Kwa sababu ukifika kiwango cha kumsomesha mtoto basi nyumba yako itaanguka itaporomoka. Hutatia makuti. Utavaa viraka. Kula kwako kutakuwa ni kwa udananda udananda. Kwa nini?Kwa sababu ya kumsomesha mtoto kwa vile elimu ilivyo ghali.

Kwa hivyo pendekezo yetu tunasema katika elimu, elimu iwe ya bure kuanzia Primary mpaka Secondary. Na si kwamba Serikali haiwezi. Tuna hakika inaweza. Kama kutakuweko na mipango mizuri ya mali zetu hizi resources zetu tulizo nazo elimu inaweza kuwa bure, watoto wakasoma mpaka kiwango cha juu. Nafikiri kwa hayo machache mimi nitakomea hapo na ninazo memorandum zangu, yangu binafsi na pia vile vile ya ma-imam. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Bwana Mwinyi, Alaikum Saalam. Bwana Mwinyi Commissioner ana swali ataka kukuuliza.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Mwinyi. Ningetaka kuuliza ulisema manufaa ya resources kama ile pesa inapatikana kwa hotels au the jobs that are offered, that a certain % should come to the local people. Si ndiyo? Nauliza kama waweza kutaja percentage kama ngapi?

**Mwinyi Ali:** Inaweza kutoka kama asilimia ishirini na tano halafu asilimia sabini na tano wabaki nao. Katika faida ile ambayo watapata. Lakini asilimia ya wale waajiriwa basi asilimia sabini na tano iwe ya wakazi wa hapa. Na asilimia ya faida ambayo itapatikana kubakia kwa wenyeji iwe asilimia ishirini na tano.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Bwana Mwinyi. Anayefuatia ni Bwana Mwinyi Ligoma.

**Mwinyi Ligoma:** Ma-commissioner na wananchi wenzangu salam alaikum. Kwa jina kamili kama mlivyosikia naitwa Mwinyi Ligoma na niko hapa kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya msikiti mkongwe zaidi Likoni ambao ni wa Baghalani. Ijapokuwa mwenyewe si mkongwe namna hiyo lakini nimechukua uzito wa maoni ya wenzangu na maoni yetu tumeyagawanya kwa vifungu fulani ambazo nitaanza kwa mukhtasari.

Kwanza ni utaratibu wa utawala kama walivyopendekeza wenzangu waliotangulia sisi pia vile vile tunapendekeza kwamba utawala wa nchi hii yote uwe wa *majimbo* kuwakilisha mikoa iliyoko kwa sasa. Vile vile tunapendekeza kuwa Katiba iwe wazi kuruhusu jimbo lolote kujitawala lenyewe itokeapo kuwa majimbo mengine hayakupendelea kujitawala *kimajimbo*.

Nina maana kuwa kama mikoa mingine haikutaka kujitawala kimajimbo lakini imetokea pengine jimbo moja ambayo limeona iko haja ya kujitegemea wenyewe, basi Katiba iwe huru kuruhusu jimbo hilo kujitawala. Vile vile Serikali hiyo ya jimbo itaongozwa na Governor ambaye atachaguliwa na wananchi.

Sehemu ya pili ni kuhusu Rais wa nchi. Kama ilivyo Rais wa nchi huwa ni ishara wa umoja wa kitaifa, tunapendekeza Rais wa nchi awepo lakini asiwe na nguvu nyingi mbali awe ni mkuu wa taifa pekee. Na Serikali kuu iwe mkuu wake ni Waziri Mkuu.

Rais huyo atakayechaguliwa na wananchi awe na sifa zifuatazo: Awe ni mwananchi mzalendo wa Kenya amri usiopungua miaka arobaini na tano na awe ameoa kisheria. Kama ilivyo kawaida ya mwafrika yule ambaye hajaoa kwa kweli huwa hajahitimu ama huwa hajakimu kimaisha kwa hivyo hatuwezi kumchukua mtu wa aina hii ambaye hawezi hata kumiliki nyumba yake ama bibi yake awe atamiliki watu milioni zaidi ya thelathini. Kwa hivyo tunapendekeza Rais awe ameoa kisheria na awe

amejiandikisha kupiga kura.

Elimu yake isiwe chini ya O'level na awe na akili timamu na asiwe na shutuma zozote zile. Raiwa awe atachukua hatamu isiyopungua miongo miwili ya miaka mitano mitano kila mmoja na baadaye Raisa atakayefuatia awe anatoka kutoka jimbo lingine. Hii itawezesha kugawanya utawala kwa kila jimbo. Vile vile Rais huyu atakuwa yeye anasimamia ulinzi wa nchi ndani na nje. Mashauri ya nchi za kigeni na hazina kuu ya taifa. Hizo ndizo zitakuwa ni kazi zake.

Ili hali sehemu ya tatu ambayo ni Waziri Mkuu, huyu ndiye atakayekuwa Mkuu wa Serikali ambaye atachaguliwa na wakilishi wa majimbo yote ya nchi ambapo yeye mwenyewe atakuwa ni mwakilishi wa jimbo moja. Yeye ndiye atakayeunda Serikali kuu kwa kuteuwa mawaziri wake na kupitishwa na bunge hilo. Bunge kuu hili tunaliita Senate. Bunge hili litaundwa na wakilishi wawili kutoka katika kila jimbo nchini. Mmoja wao wa wakilishi hawa atakuwa anatoka kutoka chama kinachotawala. Ili hali yule wa pili atatoka katika chama cha pili cha upinzani.

Waakilishi hawa ambao tutawaita Senators ndio watakaomchagua Waziri Mkuu miongoni mwao. Bunge hilo ndilo miongoni mwa kazi ingine litakaloidhinisha uteuzi wa wabunge wateule. Si Rais wala si Waziri Mkuu pekee atakayeteua bali ni wabunge ndio watakaoteua wabunge wateule na kila jimbo kuwe kutapatikana mbunge mmoja. Na Governor wa jimbo huyu ndiye atakaye kuwa Mkuu wa Serikali ya jimbo mwenye kuchaguliwa na wananchi kila baada ya miaka mitano. Yeye ndiye atakayeteua baraza la mawaziri wa Serikali hiyo kutoka wajumbe ambao watachaguliwa na wananchi kutoka maeneo yao ya wakilishi. Yeye atakuwa na sifa zifuatazo:

Awe ni mwananchi asili. Sio mzaliwa tu hata kama ametoka jimbo lingine lakini amezaliwa hapa basi ni awe ni asili ya jimbo lile. Na sote tunajijua yupi ni asili wa jimbo hili na ni yupi ni asili wa jimbo lingine. Kwa hivyo huyu atakuwa awe ni mwananchi asili wa jimbo hilo asiyepungua miaka thelathini na mitano. Na awe pia ameoa kisheria amejiandikisha kupiga kura na elimu yake isiwe chini ya O'level. Na kawaida ashinde kura nyingi na kupata asilimia ishirini na tano ya kura zote zilizopigwa katika wilaya zizizopungua tatu. Na yeye atachukua hatamu kwa muda usiozidi miongo miwili ya miaka mitano mitano kila mmoja.

Bunge la jimbo: Bunge hili linajumuisha wabunge wote wa *jimbo* wanaochaguliwa na wananchi kila baada ya miaka mitano. Bunge hilo ndilo litakalounda Serikali ya *jimbo* kuambatana na chama kilichoshinda uchaguzi. Na wabunge wa bunge hilo ndio watakaochagua wakilishi katika bunge kuu. Chama kile kinachotawala kitateua mwakilishi mmoja na kile cha pili cha upinzani kitateua mbunge mmoja. Na vile vile tunapendekeza Katiba hii wabunge wasihame vyama vyao mpaka baada ya miaka mitano ya uchaguzi.

Serikali za mitaa: Haya ni mabaraza ya wilaya ambayo yanawakilishwa na madiwani wanaochaguliwa na wananchi kila baada ya miaka mitano. Na wakuu wa mabaraza haya ambao ni Mayors na wenyeviti wachaguliwe na wananchi pia. Hawa pia wawe na sifa kama zile za mpiganiaji u-governor ama Rais.

Halafu board ya uajiri. Hapa twaweza sema hii ni sehemu nyeti sana ya uajiri na kila jimbo tunapendekeza liwe na boarad yake itakayoshughulikia uajili. Board hiyo ndio itakayohusika na kuwaajili wakuu wa wilaya ambao ni ma DC's na tarafa ambazo ni DO'S. Baada ya kuridhika na sifa na ujuzi wao. Kila anaye omba nyadhifa hizi awe anatoka katika sehemu anayotaka kuongoza. Naye pia awe ni mwananchi asili wa ile sehemu ambayo anataka kupigania ama kuchukua u-DO ama u-DC.

Vile vile tunapendekeza kuwa board hii ndiyo itakayohusika na kupendekeza kwa wananchi kumchagua chief wao na sub-chief wao na vile vile mkuu wa kijiji. Na pia tunapendekeza kikatiba awe mzee wa kijiji analipwa na Serikali. Sio awa atafanya kazi ya uongozi ikiwa yeye ndiye muhimu sana katika jamii maana yeye ndiye aliye karibu na raia lakini awe haambulii chochote.

Vile vile kuwe kikatiba iwe itakuwa lazima kwa muajiri* yeyote mahali popote anapofanya kazi zake ama shughuli zake basi wafanyikazi wake wote……mimi napendekeza wafanyikazi wake wote watoke eneo lile ambapo kazi yake ipo. Sio kuwa asilimia kadha asilimia kadha. Hapana. Wote watoke pale. Na ikiwa imetokea haja ya kuwa pengine mfanyikazi wa katika eneo lile hakuna mmoja ambaye pengine ama hakuna wale wanaostahili, hapo ndio atafute kutoka eneo lingine. Na liwe ni kati ya lile jimbo lile lile.

Kwa hivyo wote wafanyikazi watoke pale maana nina hakika hakuna kazi ambayo haiwezekani mahali fulani. Ama kama itatokea haiwezekani basi ni uhakika kuwa katika jimbo hilo lote hapatokosekana mtu ambaye hawezi. Hii ni ishara kubwa ambayo inatokea mahotelini hapa. Utapata wafanyikazi wanatoka sehemu ambazo sio zile ambazo zina kazi kama hiyo. Ambapo ukifika maeneo mengine utapata hata mfunguaji gate ni wa pale pale. Lakini huku utapata hata mfunguaji mlango gari ipite si wa hapo. Hiyo ni dharau kwa wale wenyeji wa pale maana imekuwa umelisusha akili zao za kuwa pia hawezi kufungua ule mlango ili gari ipite.

Halafu pia ofisi ya Chief Kadhi. Sehemu hii tunapendekeza kuwa Chief Kadhi wa taifa achaguliwe na Ma-imam wa misikiti yote ya nchi hii. Kila Imam wa msikiti awe ana haki sawa na Imam yeyote yule mwingine. Kwa hivyo Chief Kadhi awe amehitimu sheria ya kiislamu katika Chuo Kikuu kinachotambulika ulimwenguni. Vile vile kazi atasaidiwa na jopo la maulamaa wa kiislamu kama washauri wake. Vile vile Chief Kadhi awe na uwezo wa kuhukumu kesi zote zinazowahusu waislamu kuambatana na sheria za Quran na hadithi za mtume wetu Muhammed Swala Aleillah wa Salam.

Korti hii pia tunapendekeza iwe huru na uamuzi wake uwe ndio mwisho. Ma-Imam wote wa wilaya moja wamchague Kadhi wa wilaya yao. Ili hali ma-kadhi wote wa wilaya wamchague Kadhi mkuu wa jimbo lao. Na mwisho hatimaye ni mahakama: Kama ilivyo kawaida tunasema 'nguvu za maji ni mawe.' Hapa tunapendekeza kuwa nguvu za Katiba hii yetu itakuwa ni mahakama. Na mahakama itakuwa ina nguvu vizuri kuijenga Katiba yetu ikiwa mahakama hii itakuwa huru. Isiingiliwe na Serikali.

Kwa hivyo kuwe na mahakama kuu ya kitaifa na kila jimbo liwe na mahakama yake na mahakama hizi zote mbili ziwe huru na ziendeshe kazi zake bila kuingiliwa na Serikali. Hayo ndio maoni yetu na tuna memorandum ambayo tunaitayarisha ambayo baadaye tutaiwasilisha kwenu nyinyi. Kwa hayo machache, Maaslamu.

**Com. Zein Abubakar:** (islam) Lakini Mwinyi hiyo uliyo nayo hapo iwe chanzo uitoe hapo.

**Mwinyi Ligoma:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa bwana na uandike kwenye the register ya kwamba umetoa maoni. Asante. Anayefuatia ni Bwana Hamadi Bakari. Bwana Hamadi Bakari. Karibu bwana.

**Hamadi Bakari:** Salam Alaikum (islam). Kwa jina naitwa Hamadi Bakari Mguwa. Mapendekezo yangu kuambatana na Katiba kuhusu Serikali: Serikali ninayoitaka mimi nataka Serikali ya majimbo kwa sababu nitasema hivyo, hivi sasa Serikali iliyopo ambayo inasemekana ni Serikali ya mseto ina karibu miaka arobaini. Na mimi mwenyewe hapa ninayesimama hapa nina miaka zaidi ya arobaini. Hakuna siku hata moja ambayo katika Serikali hii ya mseto ambayo achaguliwa makamua wa Rais kutoka katika jimbo hili akaambiwa kwamba ‘wajisaji moja tu’. Akaambiwa huyu ni Makamu wa Rais. Kisha baada ya hapo akaondolewa. Hakuna hata kitu moja. Sasa mseto huu, mseto wa vipi?

**Com. Zein Abubakar:** Mzee wangu pale mchokozi anakwambia ‘songea kwenye microphone’.

**Hamadi Bakari:** Huu si mseto bali huu ni upande mmoja tu. Huu mpira huu unapigwa upande mmoja. Basi kwa hivyo sisi tunaonelea bwana Serikali ambayo itakayotufaa sisi ni Serikali ya majimbo. Na hili jimbo lazima liwe na sheria zake. Liwe na bunge lake. Watu wenyewe waweze kutoa sheria zao zile ambazo zitaweza kuwamiliki ama kuwahukumu kwa kila jimbo ama wale ambao twataka basi wabaki hivyo hivyo. Lakini wale wanaotaka jimbo basi wapate jimbo lao. Na ninasema hivyo kwa sababu nikirudi nyuma katika historia tunavyojua kwamba hasa katika huu Mkoa wa Pwani. Tunajua kwamba hiyo ugumbara kule ama ni huko Kenya ile ilikuwa ni British colony lakini hii haikuwa British colony. Sasa kwa sababu hiyo sisi tunataka mfumo wa majimbo. Ndio Serikali ambayo itaweza sisi tufanye mambo yetu vile tunavyotaka.

Jambo la pili ni kuhusu ardhi. Ardhi kwa hakika hivi sasa ukianzia hapo ferry hapo mpaka Lunga lunga hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweka kama elfu moja ama mia tano ambazo ni zake binafsi amepata tu hivi hivi. Hakuna hata mmoja. Lakini kuna watu ambao wametoka nje ya jimbo hili wana acre zaidi ya mia mbili wanatu (inaudible). Ambayo hii sasa ni maonevu katika nchi hii ambayo mambo haya yanaendelea. Sasa ardhi hii tunataka wale ambao wenyeji ama wenye nchi sio wananchi. Wenye nchi lazima wawe wako mustari wa mbele. Waganyiwe ardhi yao wenye nchi sio wananchi. Nikisema wananchi ni wale ambao wenye wa hapa hapa. Wananchi wale wanatoka sehemu zingine. Tunataka wenye nchi ndio wamiliki nchi yao sio wananchi.

Kitu kingine ni uchaguzi: Uchaguzi ambao tunautaka ikiwa mtu anaarifiwa kwamba yeye hatoki katika jimbo hilo basi asiweze kugombania kiti chochote ama wadhifa wa aina yeyote ile. Kwa watu wengine vile vile na ujinga wao ule ule watapelekana hivyo hivyo. Hivyo ndivyo tunavyotaka. Wale wajinga wapelekane na ujinga hivyo hivyo. Welevu nao wapelekane na werevu wao hivyo hivyo. Kila watu wawe kivile vile. Basi mpaka ulimwengu utakapokwisha……

**Laughter from the audience.**

Hivyo ndivyo tunavyotaka sisi. Uchaguzi tunataka uwe wa namna hiyo. Lakini sio kama vile ilivyo hivi sasa. Utakuta tuko kwamba tuko hapa tunasema kwamba sisi tumejitawala ama tu wananchi wa hapa lakini ukiangalia katika ofisi zote hizo huwezi ukakuta mtu wa hapo. Utakuta DC, amefa kuletwa hapa, DO ni wa kuletwa hapa. PC mwenyewe wa kuletwa. Sasa atakuwa na huruma na wewe kwa kitu gani? Na sisi tunasema kwamba 'zimwi la kwenu halikuli kwa kumaliza hata kama mla wa kwenu ni mbaya lakini hawezi kukufanya ubaya'. Sasa tunataka hivi bwana, ikiwa ni PC, ikiwa ni DC wote watoke mahali pale pale pale. Tena wawe ni wenye nchi sio wananchi. Kwa machache nayozungumza mimi nayopenda mimi ni hayo.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Bwana Bakari tumeyasikia. Sasa ningependa kutumia ile fursa mlionipa mimi kubadilisha utaratibu kidogo. Mliniwapa wenyewe sio? Sasa nitataka kumuita mwanafunzi mmoja halafu turudi kwenye orodha, mwanafunzi mwingine. Hapa shule leo imefungwa kwa sababu ya kazi hii. Lakini ilipofungwa, wakaambiwa wanafunzi pia wawe na haki ya kutoa maoni. Ndio wengine hawakuenda nyumbani wanasubiri kazi hiyo. Kuna mwanafunzi anayeitwa Stephen Kamaliki. Hayuko karibuni. Shaban Abdullah. Shaban uko karibu. Karibu Shaban.

**Shaban Abdullah:** Salam Alaikum wallahamdullahi wabara... Ama mimi maoni yangu ingawa bado naonekana mdogo lakini kuna ule uhuru wa kutoa maoni yangu. Ushaona? Sasa wazee haya maoni yangu bwana ni ya kutoka kwenye kifua changu ama akili yangu. Kwa hivyo kama yatawaudhi wengine sijui ni kivyao. Lakini mimi naona sawa. Ushaona? Sasa langu la kwanza ni huyu Kadhi. Yaani mambo yangu yatakuwa kwa religion sana kuliko kwa mambo ya kawaida.

Huyu Kadhi wa Kenya ama Kadhi yeyote wa Mombasa wa wapi? Alichaguliwa na nani? Kawaida mambo inavyotakikana yaani yule Kadhi achaguliwe na waislamu wenyewe. Wale waislamu wanaokaa pale ndio wamchague Kadhi wao. Lakini tukimwaangalia Kadhi wetu wa sasa huyu, Kadhi anachaguliwa na Serikali. Sasa wale ambao tuna watu wengi sana ambao waweza kuwa makadhi wazuri lakini sasa hawachaguliwi kwa sababu hawajulikani na Serikali. Inaweza kuwa mtu hakusoma hana lolote hana ule ujuzi wowote hana lakini sasa yeye anawekwa Kadhi kwa vile anajulikana na Serikali. Kwa hivyo hii mimi ningependa yaani Kadhi achaguliwe na waislamu walioko hapo.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa tumefahamu. Unapendekeza Kadhi achaguliwe na waislamu. Sawa.

**Shaban Abdullah:** Pili ni hizi ofisi za Kadhi yaani. Kwa vile hapa Coast ndio kwenye waislamu wengi yaani kwa nini sasa yule

Chief Kadhi atoke Nairobi ama yuko huko Nairobi na hajakuwapo hapa Coast na ndio kuna waislamu wengi. Kwa hivyo at least kila mkoa uwe na Kadhi wake. Kama Lamu kuwe na Kadhi wake. Hapa Mombasa kuwe na Kadhi wake na Kitale wapi yaani kila wilaya. Napendekeza hivo kuwe na Kadhi wake halafu Chief Kadhi atoke hapa Mombasa na ofisi yake iwe hapa hapa Mombasa. Ushaona? Hiyo ndiyo mapendekezo yangu kuhusu Kadhi. Naona nimeeleweka.

Halafu la tatu kama ingekuwa inawezekana hii sheria ya kiislamu iko na waislamu wako hapa Coast kwa nini wasihukumiwe na sheria ya kiislamu. Kwa nini? Na iliyoko sheria ya kiislamu iko clear na ina kila kitu chake. Sasa mambo ya ukimwi kama hapa Coast pia ni aibu. Kwa sababu ukimwi kiislamu, waislamu hawafai kuingiliana nje ya ndoa na wanaingiliana kwa sababu sheria hakuna. Sasa ikiwekwa ile sheria wale waislamu wakihukumiwa na ile sheria yao sioni kama hapa Coast patakuwa na ukimwi. Ushaona bwana? Kwa hivyo bwana hii sheria ya kiislamu, Coast itumike hata kama haijatumika kwa wale wenyewe waislamu pekee yake. Lakini itumike. Sasa sisi ni watu wa hapa na twataka tuhukumwe namna hii.

Halafu la mwisho ingawa tena kwa Serikali nataka hii vyeo vya Rais. Vyeo vya Rais vipunguzwe. Rais wetu sasa ana vyeo karibu ishirini. Sijui ni Commander in Chief, sijui nani? Kila cheo anacho yeye. Sasa mambo gani haya. Tumemweka yule Rais sasa tumemweka very powerful mpaka hatuwezi kum-control na vitu vyovyote.

Sasa Rais kwa mfano yaani tuchukulie Dick Waweru mambo yote ni ile examples tunaziita hivyo. Bwana Mwahima na Dick Waweru. Mwahima alikuwa Kanu, atoka Kanu anaingia wapi ameingia Ford People. Ametimuliwa. Dick Waweru alikuwa DP ameingia Kanu hakutimuliwa (inaudible) mambo gani haya? Sasa lazima tujue tumemweka yule nino pafu mpaka hawezi kufanya lolote. Analotaka yeye ndio analofanya. Analotaka yeye navyofanya. Hilo ndio maana naona hivi vyeo vya Rais vipunguzwe.

Kwa sababu sasa amekuwa powerful hatuwezi mwambia lolote hakuna aweza kwenda kumwambia lolote mpaka sasa. Kwani Mwahima amerudishwa? Yule hakusoma ndio hakusoma lakini si tumemchagua mwenyewe? Kesho basi uweko Rais msimpigie kura tutajua hamumtaki lakini sasa mumweka enyewe hapo…..jamani haya haya mimi naona kama democracy tushafahamu. Ni hayo tu wazee wangu.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Shabani. Sasa utahitajika uende pale kwenye register uandike register kwamba umetoa maoni. Asante Shabani. Baada ya kumpa mwanafunzi mmoja tunarudi kwenye orodha yetu halafu tutampa mwingine tena fursa. Godwin Ouma.

**Godwin Ouma:** Hamjambo wananchi. Kwa majina naitwa Godwin Ouma na niko na maoni Fulani ambayo ningependa kutoa hapa. Kwanza kabisa upande wa Rais, mimi vile mwenzangu ambaye ametoka kuzungumza saa hizi ameongea naonelea kwamba abakishwe na vyeo viwili. Kama mkuu wa nchi na mkuu wa majeshi pekee yake. Hii mambo ya kuwa Chancellor wa vyuo vikuu vitano, kwani hakuna wasomi ambao wanaweza kuwa Chancellors wa vyuo vikuu. Mara sijui nani mara nani.

Apunguzwe mpaka ibaki vyuo viwili peke yake.

Na ningependa pia Bunge lipewe mamlaka zaidi. Kwa sababu hivi sasa unapata Rais, kitambo tulikuwa tunaambiwa ako juu juu zaidi. Lakini saa hizi sijui kama bado iko hivyo. Chenye kinafanya niseme hivyo Rais unasikia hata kama amelala leo usiku pengine akiota kesho naenda kumtoa Permanent Secretary, ikifika saa tatu saa saba mtasikia ametimua Permanent Secretary fulani. Na hiyo haitakikani. Na upande wa kuchagua viongozi Rais akubaliwe kuteuwa viongozi wafuatao: Makamwa wa Rais, mawaziri wasaidizi, ma-permanent secretaries, Attorney General na mkuu wa utumishi wa Serikali peke yake.

Hao wa viti vingine pengine kama Chief of general staff, mkuu wa majeshi, Commissioner wa police, Chief Justice, DC, PC, hiyo yote ibakie bunge. Rais asikuwe na jambo lolote la kuchangia hapo. Na hao wachaguliwe kulingana na elimu yao. Kwa sababu watatuma maombi kupitia kwa idara zao. Wakituma elimu zao ….makaratasi ya kuonyesha wamefika kiwango fulani ndio sasa bunge litaamua. Hata kama ni kuachishwa kazi bunge hilo hilo ambao liwachagua tena lipitishe. Hapo tukihusisha Mkuu wa utumishi wa umma kwa sababu yeye ndiyo mwenyekiti wa tume ya kuajiri.

Kuna hii kasumba ambayo imeendelea hapa Kenya ambao upande wangu mimi sipendelei. Jana mtu amestaafu kama mfano mkurugenzi wa KPA, baada ya siku mbili ndio huyo anachukuliwa kuwa kusimamia sijui tume ya kufanya nini. Kwani hakuna watu wengi hapa wenye hawana kazi na wamesoma? Huyo peke yake alifikisha miaka ya kustaafu tena mbona arudishwe kwa kazi na kuna watu ambao hawana kazi. Kuna tume nyingi hapa zinatolewa. Tume sijui ya kuchunguza mioto, tume sijui ya kuchunguza nini hii ni pesa ya Serikali ambayo tungekuwa tunapewa raia kama kwa mwezi shilingi mia mbili kila mtu kutumia. Hizi tume zinatusaidia nini? Tume zinabuniwa hazileti matokeo. Zikileta matokeo yanafichwa na watu ambao wanajulikana. Sasa hiyo inatusaidia nini. Juzi mwaka uliyopita wametoa tume ya kuchunguza utaratibu wa elimu 8-4-4. Ilitoa mapendekezo yako wapi. Kwanza hata mimi najua nimekuwa msomi wa 8-4-4 lakini naona kama 8-4-4 haikunifaa. Hakuna kitu ilinisaidia.

Kama itabaki, masomo yapunguzwe kabisa. Kidato cha nne wafanye masomo tano. Sasa hii maneno ya tume eti nimeteuwa tume sijui ya kuchunguza nini. Hizi maneno za tume zifutiliwe mbali na kama ni lazima tume ikuwe, kama kwa mfano ya kurekebisha Katiba , tume ya vitu zingine. Bunge liamue na kwanza lichunguze hiyo tume itakuwa na umuhimu gani ndio hiyo tume itakubaliwa iendelee.

Tunataka uchaguzi wa Rais utengwe kando na uchaguzi wa wabunge na wa diwani. Uchaguzi wa Rais ukuje mapema kama mfano miezi mitatu kabla ya uchaguzi wa madiwani na ubunge. Mtu kama pengine ametaka kiti cha urais ameshindwa, anaweza kurudia kuchukua kiti ya ubunge ama udiwani. Tuna vyuo vya walimu. Walimu sana sana wa shule za msingi. Kwa vile vyuo wale sasa ndio wanafunzi. Hata wao wa Secondary afadhali. Kule mwanafunzi anafanya masomo kumi na nne. Sasa ya kazi gani? Mbona pia asipunguziwe afanye masomo mawili yaani tunaiita specialization. Akienda ajue mimi ni mwalimu wa hesabu, mwalimu wa Kiswahili, sio mwalimu wa Music, Home science, Art and craft, Business. Sasa hiyo yote inaenda kwa kichwa ya nani?

Kuna shida kubwa hapa mtu anaamua kesho Likoni iwe wilaya. Sasa wilaya hatukatai ndio umetuletea uongozi karibu. Sasa baada ya kuamua Likoni iwe wilaya, wanaenda kuweka makao makuu ya Likoni pale kwa ferry. Sasa unataka mtu wa Mtongwe huko uchini atakuwa anafika namna gani huku. Mbona hiyo makao makuu isiwekwe pale kati kati pa wilaya. Ama kama ni mkoa muweke makao makuu katikati. Ambapo kwanza wafanye uchunguzi katikati ni wapi. Hata kama hakujajengwa waweke hapo. Kila mtu iwe rahisi kwake kufika pale. Sio kuumiza watu wengine.

Kuna vijitabu huwa zinatolewa na Serikali zinaitwa Kenya Gazette. Hivi vitabu kama mimi upande wangu tangu nizaliwe nimewahi kusoma mara moja na ilikuwa tu ni siri ingine kali sana kupata hicho kitabu. Na kama kinatolewa kwa sababu ya wananchi mbona wananchi wasipewe hicho kitabu wakapitia. Sasa tunatoa maoni hapa, Bunge itaenda kupitisha sheria sisi tunatembea kama vipofu hatujui ni sheria gani ama nini kinaendelea. Vitabu zimefichwa sijui eti na nani na nani. Sasa hiyo kila mwananchi apewe kitabu mwenye anajua kusoma. Aelewe ni nini natakikana nifanye nini. Hatutakuwa na shida za watu sijui kufanya nini. Mtua anaelewa chenye anatakikana kufanya. Local authorities, Mayor na Chairman hawa wachaguliwe na watu moja kwa moja sio na madiwani. Sisi ndio tulichagua madiwani hao sasa tena tunataka kuchagua viongozi. Huyo Mayor sio eti anatumikia madiwani anatumikia kila mtu.

Hii maneno ya nominated MP’s ama Councillors. Saa hizi Bunge la Kenya kuna wabunge karibu mia mbili na ishirini na kitu. Kwani hao wabunge hawawezi kufanya kazi ndio waongeze tena wabunge wengine kumi na mbili wa kufanya nini? Hawezi kufanya kazi? Hawa watu wengine….hii ni kumaliza pesa za umma ambazo ningesema wangekuwa wanapea kila mwananchi hata shilingi mia mbili ama mia tatu kwa mwezi.

**Com. Zein Abubakar:** Hilo ushasema. Tushaliandika hilo.

**Godwin Ouma:** Kuna sana sana kama huu mwaka karibu tunafikia uchaguzi. Hii tarehe ya uchaguzi imewekwa ni kama ni siri ya mtu kwa nini. Hiyo tarehe isemwe mapema. Mtu akijua tarehe fulani nataka nichaguliwe ama nataka niongee na watu wanipe kura. Hiyo tarehe isiwe siri ya mtu. Si bibi yake mwenye inakuwa siri yake. Hii ni tarehe ya mwananchi yote. Halafu ukija upande wa mikutano pengine campaign.

Tuna watu ambao tunawatamani sana kusikia manifesto yao hata kama ni dakika mbili lakini hatuwapati. Kwa sababu Kenya ni kubwa. Mbona Kenya iko na kituo cha kutangaza T.V na redio mbona hao watu candidates, presidential candidates wasipewe kama dakika thelathini. Mtua aongee pale hata kama hautamwona life lakini umesikia chenye ameongea. Wewe mwenyewe umemwona. Utaamua umupee kura yako kuliko mtu sijui ndio yule anatakikana aende Kwale, kesho sijui aende Marsabit, kesho kutwa sijui aende Busia. Hiyo pia ni kurahisisha kazi.

**Com. Zein Abubakar:** Ouma dakika tano zishakwisha sasa ungekuwa unatakiwa kufupisha.

**Godwin Ouma:** Ilikuwa ni kumi?

**Com. Zein Abubakar:** Yako umeandika.

**Godwin Ouma:** Ni points tu.

**Com. Zein Abubakar:** Mbona wataka kutumia ujanja bwana?

**Godwin Ouma:** Hii si memorandum ni ile tu points.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa.

**Godwin Ouma:** Kitu kingine, Kenya ni multi-party na sasa tuna vile tunajua Rais anatakikana awe kwa vipindi viwili. Hizi pesa ambazo tunatumia hizi, tukisema kila Rais mwenye anakuja anatengeneza kuweka picha yake haitakuwa na maana. Pesa watengeneze zenye ziko na …..Kenya iko na picha zingine mzuri wanaweza kuweka kwa pesa. Pesa isikuwe na picha ya mtu.

**Clapping from the audience.**

Kwa sababu ni nchi nyingi ziko na pesa lakini hazina picha ya mtu. Mfano hata saa hizi naweza kuonyesha niko pesa za Uganda hakuna picha ya Museveni na ni Rais. Bunge lenyewe lione umuhimu wa wizara fulani ndio ….kama hiyo wizara ina maana kabisa ama ina manufaa kabisa ndio inaweza kuwa introduced. Sio mtu kutoka tu eti ametoa wizara sijui ya kufanya nini. Na hiyo wizara haitatusaidia chochote.

Halafu upande wa vyama vya upinzani ama political parties. Ningependelea kama zingepunguzwa zikuwa hata kama ni kumi. Kwa sababu kuna vyama…..watu wanatoka na vyama kuja kuharibia watu wengine. Afadhali tuwe na vyama vichache kama ni kumi ama ngapi lakini viwe vya maana. Mtu anapata wazee wawili, watatu ati anaenda ku-register chama. Cha kazi gani? Namalizia nikisema hivi, hata tukitaka Serikali ya aina gani, mseto sijui majimbo sijui nini bado tuendelee kuwa na uhuru wa kuongea, uhuru wa kuishi popote na uhuru wa kutembea. Ni hayo tu. Asante.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Asante sana Ouma. Mwanafunzi Caroline Omanyi.

**Caroline Omanyi:** Habari zenu, pointi yangu ya kwanza is about caning in schools. Mimi naona iregeshwe. Because the African child cannot work hard or do anything without implementing some force. If we decide vitu zetu zikuwe westernized, it

will spoil our young people. Hawatakuwa…..they won't grow up to be responsible. So hiyo ikuwe changed kidogo. It should be there but not too harsh. It should be moderate so as……ikuwe tu in a motive of change. Not hurting or something like that.

Then pointi ingine is about education system. At least we should look at the old one we had and we should give every student to get to the A' levels of form five and six in a very low cost. Because if for example I finish here in form four na nataka kwenda Oshwal academy form five and six, I will have to pay thousands of money. Kwa hivyo hiyo chance pia sitapata na campus pia inataka pesa nyingi kwa hivyo at least education inafaa pia ikuwe in a very low cost.

Another point is about the growing up of the young people. That is sex education. I think it should be brought in schools because our young people should know how to live and cope up with the changes they are having. So that we can we even stop the spread of diseases because if they know this in a very tender age, tutasaidiana both parents and the teachers. We should not leave the jobs for officials only but parents also should be responsible.

My last point is about political. Our leaders should have some degrees. Our MP's should be graduates from the University. You just don't need anybody picked up in a bush and is put in an office. MP of sijui…Public works. I mean you don't have a certificate from any place and then eti you are leaving people. Hata ukiletewa some Mayors from Italy you talk to them you tell them 'No I am busy' what is that and they are the people who are going to help you. So actually, you have the knowledge so as to lead other people.

Then they should stop using the political language. Ati free education. The President was talking about free education and yet the teachers are not paid. So what is he really telling us here? We cannot get free education really. We cannot get it because teachers are not paid and the facilities are not provided so where does that free education come from. They should say what they mean and mean what they say. Thank you.

**Com. Zein Abubakar:** Thank you Caroline. Thank you. Narudi kwenye orodha yetu. David Kileta. David Kileta.

**David Kileta:** Asalam alaikum. Mimi nawakilisha shirika la mazingira hapa linalojulikana kama KECO (Kaya Ecological and Cultural Organisation). Nitaanza na Bunge. Katiba mpya iweke masharti ya …….

**Com. Zein Abubakar:** Songea karibu na microphone.

**David Kileta:** Katiba mpya iweke masharti ya kimaadili ambayo kila mbunge lazima atimize kabla ya kuwasilisha application yake ya kuwa mbunge. Katiba mpya ipatie wananchi uwezo wa kuweza kumfuta mbunge ambaye hawajibiki kazi hata miaka mitano kabla haijasha. Nasema hivi kwa sababu saa hii campaign ziko karibu. Wabunge watakuja hapa na magari makubwa makubwa. Mtu hauzi sera anakuja na leso na masukari na nini. Wakiisha hongana wananchi wanaenda kukaa Nairobi wananchi

wanaanza kulia lia. Tunataka kukomesha huo mtindo wa kuja ku-take advantage ya umaskini wa watu.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa tumefahamu.

**David Kileta:** Point number three. Kazi ya mbunge iwe ya kila siku. Isiwe ya siku tatu kama sasa vile ilivyo. Wabunge wasiwe na ule uwezo wa kujiongezea mishahara kiholela holela kama vile wanavyofanya sasa. Majukumu ya Rais yaelezwe katika Katiba. Rais asiwe na uwezo wa kuvunja bunge katika hali yeyote.

Naingilia haki za kimsingi sasa: Haki za kimsingi Katiba iweke kuwa elimu, huduma za afya, maji hizi ziwe ni haki za kimsingi. Basic. Mtu ana pesa hana anatakiwa aishi. Awe na maji, awe na elimu na huduma za afya. Katiba ihakikishe wafanya kazi wote wa umma wanawakilishwa. Wanawakilishwa katika vyama vya wafanyakazi.

Mahakama: Katiba ihakikishe kwamba wananchi wote wasio na uwezo wa kulipia huduma za mawakili wanapata huduma hizo bila malipo. Wakuu wa Serikali yaani the Executive wasiwe na uwezo wa kuingilia mahakama. Mahakama iwe huru na uteuzi wote wa maafisa wa mahakama uidhinishwe na Bunge. Mahakama za kiafrika za kushughulikia maswala ya ardhi zilegeshwe katika Katiba (traditional tribunals).

Sasa tuje kwa uongozi na matumizi ya mali asili: Katiba iratibishe utaratibu wa mvumo wa majimbo kuhakikisha usawa katika ugawaji wa rasilimali. Mkaguzi mkuu wa fedha yaani Auditor General awe na uwezo wa ku-prosecute mtumishi yoyote wa Serikali directly to court akishafanya kazi yake bila kuingiliwa.

Na jamii wa mahali pale rasilimali zilipo ndio wawe na uwezo wa kumiliki rasilimali hizo. Nikimalizia, mamlaka ya nchi: Katiba itoe kibali ili Rais aweze kuondolewa mamlakani kwa kashfa yoyote ya ufisadi. Rais asiwe juu ya sheria.

Kwa upande wa ardhi nina vifungu vitatu vya muhimu ambavyo nataka kusema. Taratibu na desturi za kiafrika za ugawaji ardhi zibaki vile vile. Ziziingiliwe hatuwezi kubadilisha mila zetu kwa sababu ya hii mambo mnasikia affirmative action. Sheria za kiafrika zingine ni mzuri na zina maana. Sheria za Trustland Act, Crownland Act, Stateland Act, hizo sheria ziliwekwa na wazungu tangu ukoloni. Hazina maana haziambatani na maadili na matakwa yetu sasa tunataka zifutiliwe mbali. Na katika Trustland Act, Serikali za wilaya zisiwe wadhamini maana zinaitwa ni ardhi za mzama. Wasiwe trustees wa hizi ardhi peke yao.

Kuwe na kamati za watu wa sehemu hizo ambazo hizo kamati ziwe gazetted kuzuia ufisadi. Maanake wanakuwa ni trustees. Lakini trustees are very corrupt. Wanauza ardhi za wananchi. Hakuna Trustland yeyote ambayo hutolewa kwa manufaa ya wananchi. Kuwe na kipimo cha juu cha ardhi mtu anaweza kumiliki. Sio kama wakati huu mtu anamiliki ardhi dunia nzima. Nashukuru kwa haya machache.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Nadhani nina swali mimi. Unaposema kuwe na kiwango kinachotengwa cha kumiliki ardhi.

**David Kileta:** Sikusema kiwango kinachotengwa.

**Com. Zein Abubakar:** Mimi kama nilivyokuelewa kwamba kuwe kuna land ceiling kwamba kila mtu…ndio Kiswahili hicho pengine kwa Kiingereza utafahamu vizuri. When you are suggesting that there should be a land ceiling of ownership, unaweza kutoa pendekezo la kiwango. How much? What should be the limit?

**David Kileta:** A limit of a maximum of twenty acres for an individual.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa. Subiri kuna swali la Commissioner. Na vile…..

**David Kileta:** Concerning what?

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Traditional tribunals. Can you say something a little bit more about them?

**David Kileta:** Okey you know before colonial times we had our own traditional systems which were very relevant to our needs. Africans had the way how they used to distribute land and in case of disputes they had traditional courts. You see like land cases which are heard here in High court they are not fair because most of these rich people come with money and they pay themselves out. The poor man doesnot get the right now we want African tribunals to be gazetted. It should be set up. It was there during colonial times. Why not now? Am I clear?

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Bwana Kileta asante. Mwanafunzi Mwania Hamisi. Naam Mzee wangu. Naam. Sawa Mzee wangu. Wasema je mzee wangu?**……(interjection)**

**Speaker:** Nauliza hivi. Kwa nini yeye anatumia lugha ya Kiingereza. Watu wengi hapa hawaelewi Kiingereza. Kwa nini yeye anatumia lugha ya Kiingereza?

**Com. Zein Abubakar:** Sawa mzee wangu. Si pendekezo langu na unanijua kwamba sina pendekezo kama hilo la kukufanya wewe shahidi. Aah nisikize na mimi mzee wangu. Umesema yako na unisikize na mimi. Yaani tusikizane pande zote. Si unisikize basi Mzee wangu? Si usha sema yako na mimi niseme yangu. Mzee wangu kwa heshima zako, nilipoanza mapema, nilianza kwa kueleza mtu anaweza kutumia lugha gani hapa?

Na nilivyowaanzia hivyo lakini nilisema mtu anaweza kutumia Kiswahili, mtu anaweza kutumia Kiingereza na mtu anaweza kutumia lugha yoyote ingine ya Kenya. Kisa na sababu ya sisi hatuwezi kutafsiri kila neno litakalozungumzwa kwa Kiingereza hapa hatuna muda huo. Kisa na sababu lakini kama hivo fikiria ni watu wachache sana waliokuja kuzungumza hapa Kiingereza. Mmoja zaidi ya wawili.

Na kama wewe mzee wangu ulivyoona jambo nzuri na lenye maana lililotajwa hapo ukalifahamu, ukipata fursa njoo ulitongoe. Sijui kama twaelewana. Lakini kwa ufupi tu kumuridhisha mzee wangu ninaye muheshimu sana kwamba yule bwana aliyeondoka hapa kuna mambo mawili akayataja kwa Kiingereza pengine mnafaa kuyafahamu kwa Kiswahili. La kwanza alilozungumzia ni kuhusu mambo ya ardhi. Anasema wakati wa kabla ya uhuru kulikuwa kuna mamlaka ya wenyeji yanayosimamia mambo ya ardhi. Na yeye kapendekeza mamlaka hayo yarudishwe.

Na mamlaka hayo yatakuwa na shughuli ya kuangalia mambo ya umilikaji ardhi, mipaka inawekwa vipi, nani anapewa ardhi, nani ana haki gani ya utumizi wa ardhi, yasimamiwe na mamlaka hayo ya wenyeji. Hayo ndio aliyoyasema yeye. La pili, kasema kwamba kuwe kunawekwa kitengo maalum cha watu kumiliki ardhi. Najua hilo bwana akapenda Mzee wangu pia niseme. Sio sawa mzee wangu? Asema mtu asiruhusiwe kuwa na acres zaidi ya ishirini, ikifika ishirini basi. Haya. Waacha tumpe mwanafunzi fursa na yeye.

**Mwania Hamisi:** (islam). Kwa jina naitwa Mwania Hamisi, mimi pendekezo langu ni kwamba nataka Serikali ya *majimbo*. Serikali ninayoipendekeza mimi ni ya majimbo. Kila watu kwa mkoa wao wawe watamiliki mali zilizo kwao. Sio mali za hapa kuchukuliwa hapa kupelekwa mahali kwingine. Ama watu kutoka sehemu nyingine kuja kumiliki watu wa sehemu nyingine. Langu la pili ni kuhusu Rais yeyote atakayechaguliwa awe hatakuwa na ubaguzi. Awe atakuwa akiitwa mahali kwa mhadhara ama kwa mkutano awe ataweza kuhudhuria. Sio kuhudhuria sehemu za upande wa kabila yake peke yake na kuwaacha watu wa makabila nyingine kwa sababu huko si kwake. Ningependa Rais mahali popote kwa vile amechaguliwa na wananchi awe anasaidia wananchi wote sio kwa ubaguzi.

Jambo la pili ni kuhusu elimu. Nafikiri kabla ya mwaka haujaanza kulikuwa na …..kulisemekana kwamba elimu ni ya bure lakini kwa sasa watu walivyosikia watu walijua elimu ya bure. Lakini kwa kusema ukweli mpaka saa hii watu hawako hapa shuleni ni kwa sababu watu wamefukuzwa kuonyesha kwamba elimu sio ya bure. Watu wameregeshwa nyumbani kwa sababu ya karo. Kwa hivyo mtu akisema elimu ni bure, iwe kweli itakuwa bure. Akisema elimu ilipie afadhali watu wote wajue kwamba hakuna elimu ya bure. Kwa hayo machache. Salam Alaikum.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Asante sana Mwania. Andika jina kwenye register pale tafadhali. Tunarudi kwenye list yetu. Abdul Shabani. Bwana Abdul Shabani karibu bwana.

**Abdullu Shabani**: Commissioners na ndugu wa Likoni Salam alaikum. Kwanza kitu cha kwanza nitachokipendekeza ni sheria

yeyote itakayowekwa kwenye Katiba kama itahitalifiana na dini ya kiislamu, sisi hatutakuwa pamoja nayo. Na pili nilikuwa nataka Katiba ifuate kanuni za kidemocracia. Watu wawe juu ya sheria inayolinda haki za kimsingi kwa wananchi. Na ningependekeza pia mwananchi apewe uwezo wa kuasilisha maombi yake bunge ili kutekelezwa. Namaanisha a petition to the……

Halfu urekebishaji ujumuishe asilimia themanini ya wananchi. Napendekeza marekebisho yasifanywe na wabunge. Na raia mkenya apewe uwezo hiyo nafikiri nimeeleza. Uraia upewe yote atakayezaliwa na mkenya bali na kujali jinsia. Halafu ushahidi wa uraia wa Kenya uwe passporti badala ya hizi vitambulisho hizi.

Halafu upande wa majeshi: Uchaguaji wa majeshi ya silaha. Jeshi lichague hesabu sawa kila *jimbo* ili kushirikiana na ili kuondoa wanajeshi wengi kuwa *jimbo* moja ili kuleteana matatizo ya kiisalama. Na polisi wa utumishi, polisi wa magereza wawe wa kila *jimbo*. Halafu kazi ambao napendekeza zifanywe na *majimbo* nitazitaja kwa lugha ile nyingine. Major domestic concerns of government, education health, housing, agriculture, forestry, fisheries, planning, development, justice including police and prisons, local government, roads, tourism, the Acts, sports, Judicial matters communication and public works.

Halafu matters reserved to central Parliament, foreign policy, defence and micro-economic management and social security. We do not want unitary because it is a breeding crown for our tourism and deportism. It must be avoided in future for the sake of young children. Women be given chances of nominees. We want women to participate in decision making because it can enable them to debate a wide range of subjects including domestic violence, child abuse, handicap and the disabled which are the kind of issues that perhaps women are more sensitive to than men.

Na pia ningependekeza wananchi wawe na uwezo wa kuwafuta kazi wabunge waliochagua iwapo labda hawaasilishi miswada yao au iwapo wana upungufu labda wa akili. Na pia ningependekeza Serikali iwaweke wananchi wote sawa, wakiwemo watu wasiojiweza na wanawake.

Na pia ningependekeza nchi au Serikali kuelewa dini zilizoko ikiwa dini zilizo na wengi ni Islam na wakristu. Msimu huu akiwa Waziri mkuu kulingana na Serikali yangu ambayo ningependekeza ni ya *majimbo* na Head of State awe Waziri mkuu. Mwaka huu akiwa muislamu, mwaka mwingine awe mkristu. Au na msimu mimi naotaka. Msimamizi huyo akae miaka mitano tu badala ya vipindi viwili. Ili mwaka huu akiwa huyu muislamu mwingine awe mkristu. Na pia Waziri mkuu awe na imani ya dini. Waziri mkuu awe governor wa yale majimbo.

Halafu mahakama, kuwe na mahakama ya jimbo ambayo itasimamia kesi za majimbo na mahakama kuu ya majimbo. Halafu upande wa mahakama ya Kadhi, mwanzo tungependelea uteuzi wote wa mahakama hizi uhusishe waislamu. Na Kadhi apewe pia uwezo wa juu ambao utazuia kesi za kiislamu kupitishwa na mtu asiyekuwa muislamu. Na wadhifa wa waislamu usimamiwe na waislamu na wala usi-report kwenye Serikali ambao pengine yaweza kuwa na watu wasiokuwa waislamu.

Halafu upande wa haki za kimsingi: Ningependelea kuwe na elimu ya msingi ya bure na lazima. Na Katiba ilinde kila mkenya kupata haki ya kimsingi ambayo ni hiyo kula, kuvaa na kupata makao.

Haki ya kutuma maombi nafikiri zingine nimezieleza. Uongozi na matumizi ya mali asili. Rasilimali zote asili kama nilivyozitaja ziongozwe na Serikali ya jimbo. Bunge la majimbo lidhibiti mali zote za majimbo. Serikali iendelee kwa kuwa sawa kimajimbo kugawa rasilimali za taifa. Kuhusiana na maswali ya elimu, nafikiri ningependekeza kuwe na hii elimu ya bure na lazima na pesa za umma za Serikali zi-support school related facilities. Na pia students to specialize in Primary schools. Curriculum be reviewed to ensure new generation can sustain their lives. Wizara ya elimu kuinua talanta za vijana. Education be given to youths and others.

New Constitution to ensure regional barances in building education institutions e.g University, technical colleges, schools and whatever. Constitution to support in practical lessons to ensure sustainability in Kenya new generations. Halafu kuna lingine hapa, kila governor…..maanake natoa maoni haya kulingana na Katiba ilivyo. Waziri au Waziri mdogo au Rais mdogo hana ruhusa ya kutoka kuingia nchi nyingine bila ruhusa ya Rais. Mimi kwa maoni yangu nataka ma-governor wapewe ruhusa ya kutoka nje ya nchi kwenda tetea haki yao na kwenda tetea maendeleo ya jimbo lake.

Halafu ya mwisho ambayo ningetaka yadiliwe ningependa maoni haya yawe mijadala katika Bunge. Kufuatilia haki kutokana na mikataba iliyoko. Tungependa kila haki alokuwa nayo mkazi wa majimbo au jimbo apewe ridhaa kulingana na mikataba ya Lan caster. Mikataba iliyokuwako ambayo Serikali tuna imani ina historia zake. Na naweka moto hapa kuwa haki ya kweli ni haki ya lazima. Sisi wapwani tunapendekeza kutimiziwa kwa mikataba kutokana na kuungamana na Katiba la Kenya na kuungamana na Katiba ya mzururu wa Pwani.Tungependekeza ma-commissioners swala hili liwekwe katika mjadala na katika Katiba mpya ieleze kumejadiliwa nini au wamepitisha nini? Kw kufikia hapo asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Abdul. Tafadhali andika register pale jina lako. Kuna bwana mmoja ambaye amepatikana na dharura. Nilisema mtu akiwa na dharura tutaambiwa tupate kumpa fursa. John Kennedy. Na kwa vile John Kennedy umepewa fursa ya dharura, uyafanye mambo yawe haraka haraka.

**John Kennedy:** Bwana ma-commissioner, wananchi wenzangu hamjambo. Yangu mimi ni mawili ama matatu la kwanza likiwa ni kuhusu mambo ya elimu. Nafikiri katika Mkoa wetu wa Pwani ni muda mrefu sana tumepigania kwamba tuwe na chuo kikuu katika Mkoa wa Pwani na jambo hili kwa kweli halijashughulikiwa kikamilifu na mpaka leo tumeshindwa kupata chuo kikuu hapa Pwani.

Sababu hiyo imefanya kuwa sisi watu wa Pwani kwa namna moja au namna nyingine tumedharauliwa katika kupewa nyadhifa za kitaifa. Kwa hivyo ningependa Katiba hii ihakikishe kuwa mambo ya elimu kama vile vyuo vikuu kila Mkoa uweze kuwa

unapata wajibu sawa ama ugawaji sawa katika mambo ya elimu hasa hapa Pwani. Hilo ni la kwanza.

La pili, ni kuhusu uteuzi wa Rais. Rais kwa kusema ukweli kulingana na Katiba ilivyo hivi leo. Rais anatakikana kuwa awe ametimiza ama amepitishwa na kura asilimia ishirini na tano. Ikiwa je Rais amepitishwa na asilimia ishirini na tano na wale wengine pengine wapinzani wamepata asilimia sabini na tano, yupi aliyepata kura nyingi? Wa sabini na tano ama yule wa ishirini na tano? Kwa hivyo mimi nafikiria ikiwa itawezekana Katiba iweze kuturuhusu ama Katiba iweze kueleza waziwazi. Anayepata kura nyingi isiwe kuwa ni asilimia ishirini na tano ili aweze kwenda kuwa Rais. Tuangalie upande ule mwingine.

Wale wengine wamepata kura asilimia sabini na tano na Rais amepata kura asilimia elfu ishirini na tano. Mimi naona kwamba wale waliopata kura ishirini na tano wapewe nafasi ya kutafuta Rais miongoni mwao. Maanake wao ndio wenye kura nyingi. Kuonyesha kwamba wengi wa wale asilimia sabini na tano hawakumpendekeza, hawakumpenda yule aliyepata kura asilimia ishirini na tano. Kwa hivyo Rais kuchaguliwa na kura asilimia ishirini na tano, lao kama Katiba inaweza kubadilisha iwe asilimia hamsini ama hamsini na moja inaweza kuwa jambo la maana.

Mwisho, nikizungumzia mambo ya haki za kumiliki uraia: Hatujui kuna ndugu zetu wametoa mapendekezo hapa kuwa mtu anaweza kuwa ana mzazi mmoja anaweza kupewa uraia hapa Kenya. Lakini huyu mzazi hatujajua ni mzazi wa kike ama ni mzazi wa kiume.

Sisi Kenya leo hapa tuna watu wana uraia sehemu mbili na watu hawa wametuletea taabu maanake bahati mbaya ni watu wenye utajiri mkubwa, ni watu wenye mali nyingi ni watu wenye nguvu za kuweza kushawishi. Sisi maskini tukajikuta tuko katika hali ya taabu. Nitazungumzia mfano wa mambo yanaendelea hivi sasa. Poleni kama nitakuwa nimeudhi wengine. Lakini vita vilivyoko hivi sasa baina ya Mayor ama manicipaa ya Mombasa ni dhihirisho wazi kwa watu ambao pengine hawana macho ndio hawezi kuona.

Lakini jambo hili ni dhihirisho wazi kuwa kuna vita baina ya ubaguzi wa rangi. Ubaguzi huu wa rangi tumeuona umeleta madhara sehemu nyingi. Mimi nitoapo mfano wa taliban. Kenya tunajitaka, Mombasa twajitaka, tuje tuutafute umoja wa mataifa na Amerika kuja kutuondolea ubaguzi wa rangi Mombasa? Kwa hivyo ningependekeza ama ningependelea kuwa mtu anayechaguliwa kuwa kiongozi ama anayestahili kuchaguliwa kuwa kiongozi asiwe tu raia ambaye amepata umilikaji wa uraia ama u-citizen wa nchi mbali* awe ni raia ambaye babu zake na babu zake wanajulikana walizikwa wapi hapa Kenya. Na kama ni hapa Pwani, tuwe tunaweza kupata kumbukumbu ya familia yake, alizikwa wapi hapa Kenya.

Sio watu wa kufanya kuja hapa, leo kwa sababu wana mali wana pesa wamekuja kumiliki Mombasa, wamekuja kumiliki kiziwa. Kiziwani kusema ukweli ni wachache sana kati yetu sisi hapa tulioko hapa wanaomiliki ardhi pale kiziwani.

Wengi ni watu kufanya kuja na wameimiliki leo. Wameumiliki mpaka uongozi sisi ambao tunasema tu wenyeji wa hapa. Watu

wa digo, watu wa ndoromo, watu wa giriama, watu wa rabai, hatuna ardhi pale kiziwani. Hatuna mamlaka. Tunavuka kiziwani kama wafanyikazi. Tunakuja kulala mwituni. Jambo hili ningependa liangaliwe kimsingi nikijaribu kusisitiza kuwa anayechaguliwa kama kiongozi….

**Com. Zein Abubakar:** Kennedy wewe ulipewa kwa fursa ya kwamba unafupisha mambo kwa kuomba kuwaruka wenzako.

**John Kennedy:** Nayamaliza tafadhali Mheshimiwa.

**Com. Zein Abubakar:** Ukianza kutoa hotuba ndefu ndefu, nitakufupisha mara moja.

**John Kennedy:** Asante Mheshimiwa nayamaliza. Nasisitiza jambo hili nikisema kuwa anayechaguliwa hapa ni lazima awe ni mzaliwa wa hapa. Babu zake na babu zake wanajulikana walizikwa wapi? Nikimalizia. Kuhusu uteuzi ambao unafanyiwa viongozi wa wizara mbalimbali. Leo tunakuta kuwa hakuna usawa. Ukiangalia wizara nyingi zimechaguliwa ma-chairman, ma-director, ma PC, ma DO, ma DC kusema kweli kuna im-barance hapa.

Kuna kabila fulani lime-dominate sana katika vyeo vya ma PC na ma DC. Mtakubaliana nami wakenya kwamba ni kweli mambo haya. Jambo hili ningependa ……..pendekeza fulani lakini Bunge liwe lina uwezo wa kumpinga Rais yule kusema hapana sisi tunataka fulani pia apewe nafasi kwa sababu tunataka iwe baranced. Nina mengi lakini kwa hayo machache. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Kennedy. Narudi kwenye orodha ya watu. Francis Mugo.

**Francis Mugo:** Ma-commissioners na wananchi wenzangu salam alaikum. Mimi nikianza nitaanza kwa upande wa wafanyikazi. Mimi nikiangalia ya kwamba kila mwaka wanafunzi wetu watoto wetu wanahitimu katika vyuo vikuu na pia wale wengine wanahitimu katika ma-college yetu na wakitoka wachache tu ndio wanapata kazi. Kwa hivyo ningependekeza katika Kenya iwe mtu mmoja kazi moja. Shauri kuna wengine ambao wanapewa kazi ya u-director, anapewa kazi ya chairman hapa na pale kazi nyingi nyingi na kuna watu wengi ambao hawana kazi na wamehitimu.

**Com. Zein Abubakar:** Tumefahamu Mzee wangu.

**Francis Mugo:** Mtu aajiliwe kulingana na masomo yake na pia hata na ujuzi wake. Walemavu wakiwa wamehitimu pia wapewe kazi kama watu wale wengine na wasibaguliwe. Wapewe heshima kama watu wengine. Wafanyikazi ambao wamekuwa wagonjwa kazini wapewe heshima na ufariji. Na pia wapewe haki yao bila kucheleweshwa.

Wafanyikazi wapewe manyumba ya kuishi na makampuni hata na Serikali shauri wafanyikazi wana taabu hawana mahali ya

kukaa, hawana pesa za kulipia manyumba. Pesa ile wanapata wengine ni kidogo za kulipia manyumba wana shida. Pia wapewe usafiri. Wapewe transport ya kwenda kazini ili wawe na huduma ambayo inafaa.

Wafanyikazi wanaostaafu kazini wapewe haki yao bila kucheleweshwa kwa sababu wengine wanastaafu wanakwenda nyumbani kwenda Nairobi kutafuta haki yao mpaka wanakufa kabla hawajapata haki yao. Kwa hivyo wapewe haki yao mara moja ili waweze kujifaidisha.

Mishahara ya wafanyakazi ichunguzwe kote nchini ili wafanyikazi wapewe mishahara ambayo itawanufaisha. Shauri mishahara ambayo wanapewa sasa ni kidogo hata wengine hawapati lunch. Wanapata chakula ile wanakula ni chakula ambayo ni ya kushikilia roho tu. Ili tuzuie kunyanyaswa kwa wafanyikazi. Mfanyikazi anayefariki ni vizuri ashughulikiwe na pia marupu rupu yake yapewe familia bila kuchelewa. Saa ingine marupu rupu ambayo ingepewa familia inakatwa nusu wanapewa nusu ingine hata hawapati. Wengine hata hawajui njia gani watapata hiyo marupu rupu yao.

Kwa hivyo ni vizuri washughulikiwe ili familia yao waweze kufaidika na kazi ya mfanyikazi ambaye ni mume wao ama ni bibi yao. Rais wa jamhuri ya Kenya akichaguliwa yeye ajulishwe kazi yake ya kufanya ni gani. Shauri inaonekana Rais hajui kazi yake ni gani. Yeye unakuta hata anaenda kufungua kibanda. Yeye hajui kazi yake ni gani shauri hajaambiwa kazi yake gani. Kazi ambayo inafanywa na chifu inaenda kufanywa na Rais.

Kwa hivyo ni vizuri Rais akichaguliwa ajulishwe kazi yake ni A,B,C,D. Shauri hajui kazi yake ni gani. Rais akiwa atasafiri ng' ambo asafiri tu na viongozi ambao wanahusika katika wizara ambayo inahusika. Si kubeba tu watu ndege nzima wanaenda kutumia pesa ya Kenya na hakuna kazi wanaenda kufanya. Waende na wale watu wanahusika katika wizara hiyo ambayo wanaenda kufanya hiyo shughuli wanaenda.

Pia wakati kuna mikutano ambayo isiyokuwa ya kitaifa Rais aende na wale viongozi tu wanaohusika kwa ile wizara si wale ma ministers wote wanafunga kazi wanaenda kwa mkutano wa Rais. Kazi kule inalala. Ukienda kule haupati huduma shauri wameenda kwa mkutano wa Rais na hawahusiki. Kwa hivyo hiyo ichukuliwe maanani.

Holidays ukiangalia ni nyingi sana. Kuna zingine hata ukiulizwa maana yake hata hujui. Wewe unaambiwa kuna holiday na unasikia kuna holiday na unajua iko holiday. Lakini wewe ukiulizwa maana yake hujui. Hata mwenyewe mwenye kupewa hiyo holiday ukimuuliza maana yake anasema 'hata mimi niliona tu imewekwa'. Hajui. Kwa hivyo holidays zichunguzwe zile ambazo hazitahili ziondolewe.

Pesa za jamhuri ya Kenya mapendekezo yangu ni yarejeshwe katika sura ya mwanzilishi wa taifa ili apewe heshima yake na isibadirishwe. Kwa sababu kwa kubadilishwa badilishwa vile pesa zinabadilishwa yaani ni kuharibu uchumi wa Kenya. Ukiangalia pesa za Kenya vile zilivyo hata zina aibu. Kuna zingine kubwa. Pesa ni shilingi mia. Kuna zingine kubwa, kuna zingine

ndogo, kuna zingine zinabambuka bambuka sasa zina aibu pesa za Kenya.

Ukiangalia katika ile sarafu za Kenya, kuna tano kubwa, tano ndogo, mapeni ingine hata ikianguka mtoto hachukui. Haina kazi. Kwa hivyo pesa za Kenya ziregeshwe katika sura ya mwanzilishi wa taifa na zikae hivo hivo milele bila kubadilishwa. Hata Rais akija gani zikae hivo hivo. Masomo ya primary school yaghalamiwe na Serikali. Tena vitabu za textbooks na vile vingine vipatikane. Kwa sababu ukiangalia katika mashule wazazi wote wanapata shida sana kwa textbooks. Textbooks wana jamaa zao na idara ya elimu pengine sijui kwa sababu unaona kila mwaka kitabu cha textbook hakina kazi tena.

Ukienda kwa manyumba ya wazazi, vitabu vimejaa havina kazi. Na zamani kitabu kimoja kingetumiwa na watoto tano. Sasa vitabu tu zinarundika zinakuliwa na panya na ni mpya. Zichunguzwe vitabu, kwa ni ni zinabadilishwa kila mwaka. Kila mwaka vitabu zinabadilishwa. Kura zote za kisiasa ziwe zikihesabiwa katika kituo cha kupigia kura ili sote tujiepushe na wizi wa masanduku ya kura yakiwa yanasafirishwa.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee Mugo dakika tano zimeisha ungekuwa unaanza kufupisha.

**Francis Mugo:** Hospitali za Serikali zihudumiwe ipasavyo na wagonjwa wapewe madawa sawasawa bila kupewa makaratasi wa kanunue madawa nje. Ukiangalia watu wanakwenda hospitali, ukienda kule kwa laini unaenda tu unapewa kikaratasi kubwa, ukienda kwa dukani unaongezewa ugonjwa.

Kilimo cha kunyunyisia maji kianzishwe na Serikali kote nchini ili tumalize njaa. Ukiangalia kuna mito mingi katika nchi ya Kenya. Tuna mito ambayo iko na rotuba lakini Serikali haitilii maanani hii ukulima wa unyunyisaji wa maji. Maji inapotea bure. Kwa nini sisi tunapewa chakula na tuna ardhi nzuri. Kwa nini hatuletewi wataalamu watufundishe njia ya kunyunyisia mashamba maji ili tupate chakula hata tupate ya kuuza nje.

Kwa hivyo ningeuliza Serikali itilie mkazo tuwe na kilimo cha kunyunyisia maji. Shauri ya shida za vitambulisho, ningependekeza ya kwamba watoto wa kidato cha nne kabla hawajamaliza masomo yao wajaze forms za kitambulisho. Wakati wa kuchukua vyeti vyao wachukue pia na vitambulisho za Serikali na pia wachukue na pia wachukue na vitabu vya Katiba na Katiba isomeshwe shuleni. Ningependekeza hivi bungeni lazima nusu au zaidi ya wabunge wote mia mbili na ishirini na mbili wapige kura ili mswada wowote ufundishwe bungeni.

Ni aibu sana kuona wale wabunge wanapitisha mswada ni wadogo sana. Ni vizuri nusu yao wawe bungeni na wapitishe mswada ionekane kweli wabunge wamepitisha mswada na imekuwa mswada wa kweli.

Wabunge wanaohudhuria bunge kwa dharura wale wanakuja dakika tano na kurudi na wale wanakuja tu bungeni kulala wakomeshwe. Mashamba na plot za Serikali zilizonyakuliwa zichunguzwe ili zirudishiwe umma. Mashamba yamechakuliwa hata

choo zimejengwa manyumba hakuna choo town. Ukitaka kwenda choo urudi nyumbani ndio urudi kazini.

Watu ambao wana mashamba makubwa na hawayaitumii haya mashamba wachukuliwe na Serikali na yapewe maskini ambao hawana mashamba shauri mashamba haina kazi. Mayor na mji wawe wakichaguliwa na wananchi sababu hawa sasa wanatumikia ma-councillors hawatumikii wananchi. Ma-councillors wakishiba bas, wananchi wanakaa. Wakati tulipojinyakulia uhuru tuliambiwa ya kwamba tutashughulikia mambo matatu, moja magonjwa, ujinga, na umaskini.

Tuliona ya kwamba tulipewa wizara ya afya pia tukapewa wizara ya elimu lakini tangu tujinyakulie uhuru hakutupata wizara ya umaskini mpaka leo. Ningependekeza sasa tupate wizara ambayo ni ya umaskini ishughulikie umaskini tuweze kuondoa umaskini katika nchi hii yetu. Mtu akivunja mali ya umma achunguzwe akipatikana na hatia ahukumiwe kulingana na matando yake pia alazimishwe kurudisha alichochukua na kamwe asipewe uhamisho.

Kila mkenya ni heri awe na uhuru wa kusema, kutoa maoni na hata mapendekezo bila hofu yoyote. Hiyo pia itendeke kwa waandishi wa habari. Ni vizuri kila mfanyikazi kwanzia mawaziri kurudi chini wawe na uhuru wa kufanya kazi yao bila kuingiliwa kutoka juu. Unakuta mtu ni waziri lakini hawezi kutoa uamuzi wowote mpaka uulize juu atafanya nini. Kwa mambo yote inaenda ikichelewa shauri waziri hana uhuru wa kuamua. Shauri anaweza amua leo kesho atimuliwe. Kwa hivyo ni vizuri wapewe uhuru wa kufanya kazi bila hofu yeyote.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee wangu mambo mawili ya mwisho tutajisomea mswada wako. Umepitisha muda sana.

Bidhaa ambazo zauzwa hapa nchini ambazo zimeundwa hapa nchini, zina dhamana na ziko hali moja na zile za kutoka ng'ambo zisije zikaagizwa nje ili tuokoe viwanda vyetu. Shauri kuna bidhaa ambazo zinaundwa hapa nchini ambazo ukiangalia ziko sawa na zile za ng'ambo. Sasa unakuta hizo bidhaa zimejazwa hapa kutoka ng'ambo na tuna zetu. Viwanda vinazidi kufungwa.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee tumefahamu. Ukitupa point kwa point bila illustrations utamaliza haraka.

**Francis Mugo:** Viwanda vichunguzwe. Wanaunda vitu hapa halafu wanazituma ng'ambo hizo hizo vitu.Wanapiga mihuli na kureke...

**Interjection:** Kwa nini huyu amechukua muda mwingi sana. Na sisi tumekuja hapa asubuhi na mapema?

**Com. Zein Abubakar:** Tafadhali mzee wangu. Tafadhali Mzee wangu. Ngoja mzee mimi ndio nasimamia mkutano mzee wangu.

**Interjection:** Wataka niende zangu. Niende zangu?

**Com. Zein Abubakar:** Nakuheshimu sana. Usiende zako.

**Francis Mugo:** Nikimalizia, mikoa ambayo imesahauliwa na Serikali ni vizuri sasa zipewe nafasi ya kwanza katika kimaendeleo. Kwa hayo machache. Asanteni sana.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Mzee Mugo. Stan Seif fundi reje.

**Stan Seif fundi reje:** Salam Alaikum(islam). Ndugu zangu ma-commissioner na ndugu zangu mliohudhuria, nina shukrani kupata fursa hii ndogo ili kuweza kuzungumza machache kwa sababu ya kuweza kutanabaishana. Kutokamana na hali tuliyo nayo ilivyo katika kikatiba ni mara nyingine tena shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwamba tunapata fursa ya kuweza kuambiana ili tuangalie kwamba mzululu huu utakuwaje. Tunafahamu vizuri sisi kabla ya uhuru jinsi mambo yalivyotendwa tukapata Serikali hii tuliyo nayo. Serikali tuliyo nayo ikawa inatusukuma katika hali ya unyonge. Baada ya sisi kupata uhuru, kuna mipango iliyofanywa kugandimiza watu wa aina fulani mipango hii ilifanywa makusudi. Watu walijitengezea kwamba uhuru waja sisi tutanyakua Serikali na kweli waliweza kunyakua.

Tukawa tunaendelea lakini kwa sababu ya bahati mbaya ya watu wa pwani walibaki katika usingizi maana ilikuwa hawakujitayarisha. Halafu unyonge ulitupata wa kukosaelimu ikawa nyadhifa zote zimenyakuliwa. Sisi tukabaki katika usingizi moja kwa moja. Imetusukuma ikatusababishia sisi kwanza udhaifu uliotupata ni kukosa kazi. Kazi zikawa tumezikosa, tumepokonywa haki zetu mpaka ikwa inatakiwa kuandikwa kazi mtu mfagiaji Mombasa basi ataandikiwa Nairobi aletwe moja kwa moja mpaka Mombasa. Tumezikosa kazi.

Tunakuwa sisi ni wanyonge. Hatushughulikiwi. Haki zetu zimetupwa maana kule kupata kazi ni moja katika ya haki ya wazee ili wawalee watoto wao lakini sisi tunaanza kuuawa kutoka mashina, kwenye mashina.

Kwa hivyo Serikali hii tunaona kwamba mfumo huu hautufai. Tunataka katika Katiba hii iwe ni yenye kutambua na sisi katika nyanja za kikazi. Tukaja katika mfumo wa afya. Kama tulivyoambiwa vile vile tulivyoahidiwa. Lakini afya ilikuwa imekwenda mpaka sasa tunalipa pesa. Hali ya kwamba ugonjwa ukimuandama mtu hausubiri wala hauangalii kwamba mtu ana pesa au hana pesa. Kwa hivyo tunataka katika Katiba hii ikiwa Mungu atajalia iwe katika hali ya afya ni bure kila mmoja anatibiwa.

Vile vile tulipotoka katika hali ya afya tukaingia hali ya masomo. Masomo wakati tuliponyakua uhuru kama tunavyosema yalikuwa masomo ya ngazi za juu kama University yalikuwa ni bure. Yakaja vikwazo mpaka hivi sasa ikawa tunalipa kwanzia msitari wa chini mpaka juu hali imekuwa ni ngumu hivyo ni mikakati iliyowekwa makusudi ili waweze kusoma wale watoto ambao ni wa mishefa peke yao. Hao watoto ambao ni wa maskini wapate kufa watu wanauwana pole pole. Kwa hivyo vile vile ikiwa inawezekana tunaitaka Katiba tuizatiti iwe katika elimu ya University irudi vile vile kusaidiwa iwe ni ya bure katika maoni

yangu hayo.

Tulipomaliza tukaingilia katika kuishi katika ardhi. Tunaishi katika ardhi lakini mifumo tuliyo nayo ni ya kunyakua katika ardhi za wale wanyonge. Kwa nini isiwe hivyo? Ili hali ya kwamba wewe huwezi kujizatiti kutokamana na kielimu, kutokamana na uwezo. Hivyo basi wakati wa Serikali tuliyokuwa nayo, ilifanywa makusudi wakasema kwamba ‘sisi tunazitaka hizi ardhi tutazipata vipi? Wakaambiwa ngoja tutafanya mpango. Wakaletwa watu waje wapime hizi ardhi kila mmoja amiliki ardhi yake ili makusudi halafu ziweze hizo ardhi zije zinunuliwe. Wakati huo ulikuwa wa hayati Kenyatta. Na kweli ulifanywa hivyo zikawa kila mmoja kijipande chake anataka kuuza. Basi ardhi zimeuzwa rahisi rahisi hali ya kuwa ni rasilimali tulasi

ambazo ni zenye kudumu. Kwa hivyo tunataka vile vile wakati wa Katiba hii ziwe ardhi hizi ni zenye kushughulikiwa na ziachiwe mifumo ya wale watu wa zamani, wale wazee, makundi ya wazee waliokuwa wakizishughulikia wanajua mifumo yao. Mpaka huu ni wa nani, ardhi hii ni ya nani, na imemilikiwa ni nani.

Kwa sababu mambo haya huwa yanatoka kwa wakubwa, anasukumiwa mkubwa, inanunuliwa ardhi hali ya kuwa wewe umemiliki hapa, umekaa na minazi yako kumbe cheti kimeshauziwa mtu. Anacho cheti akija anakwambia ‘ondoka’. Kama ilivyotokea Ukunda watu wakauawa, watu wakafukuzwa na ardhi hizo zikamilikiwa. Vile vile Katiba ya Serikali tuliyo nayo ilikuwa ni mifumo ya kudhalilisha wananchi.

Wananchi wamezalilishwa muda mrefu, wananchi wamenyanyaswa muda mrefu sana kwa sababu ya kupotezewa haki zao. Haki mtu aliyo nayo imemfika kwamba hii ni haki yake lakini itapoteza makusudi na wala hana la kufanya. Nikitoa mfano mzuri, mfano uliotufika ukaacha kushughulikiwa kama vile watu wa Pwani au ferry ya Mtongwe ilipokuwa ilipozama watu wakafa na kukachangwa pesa zikaambiwa watu wao watasaidiwa na watu hao haki zao zimepotea.

Hakuna wa kumuuliza, huwezi kusema kwamba utakwenda kwa nani. Hizo haki zimepotezwa na haki hizi tunataka Katiba hii tuliyokuwa nayo iwe inachunga haki za wananchi kumpa mwenyewe, kumchukulia nyofu kumrejeshea kwenye mnyonge. Vile vile tunajua kwamba Katiba tuliyo nayo katika Serikali yetu inarudi katika kutunyanyasa. Mfano wanaweza kupanga mambo wakatuletea majanga makusudi ili majanga haya yaje yaweze kutuadhili sisi.

Mfano kama vita vya akina Bombo vilivyokuwa vilipangwa makusudi, tukaja tukapigwa wakauwawa, watu wengine wazee wakavuliwa nguo na wakachapwa na watoto wadogo. Hali hii ikawa kila mmoja anayejua imeanzia wapi matatizo yao yatarudia sisi wananchi tulioko hapa Pwani. Vile vile tunaomba Katiba hii tuliyo nayo iwe inastahi na kuheshimu ubinadamu. Hata hawa waliokuwa wanapigania haki za binadamu vile vile hakuna hata mmoja aliyeshughulika wala akaja akawa anazungumzia mazungumzo hayo bali imebaki ni kunyanyaswa. Tunataka vile vile Katiba ishughulikie huu uhuru wa mwanadamu na haki za kibanadamu ipiganiwe kwa kila mtu.

**Com. Zein Abubakar:** Stan Seif dakika kumi zimeisha ungekuwa wafupisha sasa.

**Stan Seif:** Na nafikiri na mimi nimefikia ukingoni. Asante sana. Vile vile jambo jingine ambalo linatushughulisha ambalo linatumaliza ambalo limeshatumaliza sisi sasa tumebaki kukata roho ni jambo la kuruhusu (inaudible) kuhusu ulevi. Ulevi umeenea katika sehemu ya Pwani. Watoto wameharibika. Mambo yamechafuka, kila pahali utakapoangalia unakuta kwamba hali ni mbaya. Na mambo haya yamefanywa makusudi na katika kutokamana na Katiba tuliyo nayo. Yamechaguliwa makusudi. Tunasukumiwa makusudi ili tupate kumalizika kabisa. Maana ukitaka kumaliza taifa wamalize vijana halafu itakuwa unaweza kwenda ukafanye mambo unayoyataka.

Hakuna mtu anayejijua, hakuna msomi, hakuna uzima, hakuna uhai. Watu wote hawajui wanaelekea wapi. Kwa hivyo tunataka Katiba hii inayokuja kitu cha kwanza tuangalie kuhusiana na habari ya (inaudible) kuhusu ulevi madawa ya kulevya. Na sisi tunajua kwamba kila pahali yako madawa ya kulevya lakini Serikali haijali chochote. Wanazidi sisi kutumaliza hili jambo hili tunataka Katiba tuliyo nayo Mwenyezi Mungu akitujalia mambo yakiwa mazuri basi vitu hivi viwe ni vyenye kusimamiwa na Katiba. Yawe ni mambo yenye kupangwa na sisi yaweze kutuokoa. Hapa natumai natia nanga. Nashukuru. (Islam).

**Com. Zein Abubakar:** Shukrani Stan Seif. Tafadhali andika register pale. Nimerudi kwenye list ya wanafunzi. Wamebakia wanafunzi watatu peke yake. Ramadhani Idd.

**Ramadhani Idd:** Salaam Alaikum(islam). Mimi nimekuja na maombi yangu au maneno yangu yafuatayo.

**Com. Zein Abubakar:** Ramadhani, taja jina lako ndio li-recordiwe.

**Ramadhani Idd:** Sawa. Jina langu naitwa Ramadhani Idd. Jambo la mwanzo ambao nataka kuzungumzia ni kuhusu ninio Agriculture au kilimo hapa nchini. Kwa upande huu nitachukulia mfano wa mambo ya kuhusu njaa. Nilikuwa napendekeza katika yaani hii nchi katika kila mkoa au kila wilaya kuwe kutakuwa na shamba au shamba fulani la acres kama tuseme kumi hivi ishirini nyingi yaani ambazo zitakuwa zimepandwa kitu kama mahindi hivi ambao yale mahindi yatakuwa yakitumikiwa kulisha wananchi wa Kenya.

Kwa mfano huu nitachukulia kama nchi ya India vile au China. Kule kuna watu wengi sana lakini kulingana na mimi sijasikia hata siku moja wamepelekewa msaada wa chakula. Kwa sababu ya mambo kama hayo. Kwa hivyo ningependekeza iwe hivyo kuwe na shamba katika kila wilaya ambao litapandwa chakula. Sio kupanda vitu kama kahawa, mtu anauza kwa faida yake mwenyewe. Kupandwe chakula ambacho kitatufaidisha sisi wenyewe.

Jambo lingine ni kuhusu qualifications yaani kikazi. Nilikuwa napendekeza kwa mfano mtu kama Rais au Mbunge. Yeye

kuchaguliwa kwake kama waziri kama wa kilimo, wa elimu awe ana ujuzi na ile kazi. Sio kuchaguliwe mtu ambaye hata mwenyewe kusoma hajui amewekwa Waziri wa elimu. Kwa hivyo ningependekeza iwe hivyo.

Jambo lingine ni kuhusu hii democracy. Democracy mimi kila siku naisikia lakini sioni kama yafuatwa. Na sio ukabila. Utaangalia kwa mfano mimi huku ni mndigo au mimi ni kabila yote, mjaluo nini, lakini nimefika mahali pana kampuni aliye mkubwa pale ni mjaluo au ni mkikuyu lakini mimi ni mndigo nimesema nataka kazi pale, kazi zitapata. Pakija mkikuyu atapewa kazi pale.

Jambo lingine ni kuhusu bado hapo hapo kwa democracy. Mimi nina shida nimetuma pengine kwa Rais kule. Nimesema nataka ombi fulani pengine ni mgonjwa lakini kulingana na wale watu ambao wako katika ile ofisi wataangalia huyu mtu yuko vipi ni maskini, ametoka wapi? Na kusema kweli barua haifikishwi. Na wewe uliyetuma malalamiko yako hayatafika kule. Kwa hivyo ningependa Rais awe ana haki ya kukutana na watu wake macho ana kwa ana na watu wawe wana haki ya kukutana na Rais kupeleka malalamiko yao. Hayo ndio maombi yangu. Asante sana.

**Com. Zein Abubakar:** Tunarudi katika orodha ile yetu ya wananchi. Mandingo Salim. Imeandikwa Mandingo. Asante bibi.

**Mandingo Salim:** Salam Alaikum.

**Com. Zein Abubakar:** Alaikum Salam.

**Mandingo Salim:** Mimi jina langu Mandingo.

**Com. Zein Abubakar:** Taja jina nzima ndio li-recordiwe.

**Mandingo Salim:** Jina langu naitwa Mandingo. Hilo ndio kiraufu kabisa.

**Com. Zein Abubakar:** La pili? Naitwa Alphis.

**Mandingo Salim:** Mimi sina mambo mengi lakini leo lazima mpasue. Ushasikia leo lazima mpasue! Kwa nini sisi tukienda bara hatuwezi kupatiwa mahali padogo kama hapa tukajenga kibanda. Sisi tukija hapa watu wa Coast tunapendekeza kuwakaribisha wenzetu lakini kwa nini sisi tukienda kule bara hatuwezi kupatiwa mahali padogo tukajenga kibanda. Kijulikane huyu ni mtu wa Coast anauliwa. Hiyo kitu kwa nini hamuangalii? Hiyo kitu kwa nini hamuangalii? Sisi tukienda kule tunapatiwa mahali kama hapa siku mbili tatu unaambiwa ni mtu wa Coast, unakatwa katwa mapanga tunaletwa kwetu maiti. Hiyo kitu namna gani sasa?

Halafu la pili ni juu ya kuwa msimamo wetu twataka majimbo. Huo ndio msimamo wetu wa pili. Mara ya kwanza hiyo.

Mshasikia? Huo ndio msimamo wa kwanza wa pili twataka majimbo. Kwa sababu gani kila siku sisi watu wa Coast wako waliosoma na kwa nini twaambiwa hatuwezi kupigania viti hapa kwetu tukapatiwa urais. Urais utasikia ni wa watu wa kutoka wapi? Watu wa kutoka juu. Mbona hapa kwetu kwa nini hatupiganii tukapata urais? Hiyo kitu kwa nini? Mbona hatuangalii sasa na kila siku tunaambiwa watu wa Coast watele waliosoma. Watu watele waliosoma waliofika University. Halafu twaambiwa watu wa Coast hatukusoma. Hatukusoma vipi? Hiyo kitu kwa nini hatukusoma, kila siku twaambiwa watu wa Coast hatuna maana.

Halafu jambo lingine ni juu ya kuwa twataka DC, PC, awe mtu wa Coast. Hiyo ndio tunataka. DO nani mkubwa yeyote anayesimamia (inaudible) kila siku utasikia sijui nani ni Mnandi ametoka juu amekuja tawala Mombasa. Kwa nini hapa kwetu hatuwezi kupata wakubwa hapa? Hapa kweli hatuwezi kupata wakubwa? Si hapa wakubwa watele waliosoma. Mbona kila siku tunaambiwa watu wa Coast hatuna maana. Kila siku tunaambiwa watu wa Coast hatuna maana mpaka saa ngapi. Nasi nasi kila siku twaambiwa watu wa Coast twangoja kupora maembe yaanguke ndio tuyaokote. Na watu wako tele waliosoma. Mbona kila siku twaonewa sana twaambiwa watu wa Coast hatuna maana. Watu walio na maana kwa nini sisi kila siku tunaambiwa hatuna maana. Nasi nasi safari hii twataka viti na si tuwe marais kama vile wenzetu. Sio kila siku twaambiwa watu wa Coast tuwe hatuna maana. Hilo neno la nne sasa.

La tano ni juu ya kuwa twataka University. Twataka chuo kikuu, ndio tunaotaka. Hiyo ndio kitu muhimu. La tano hivi. Halafu chuo kikuu tukimaliziwa twataka tujengewe Pwani kila pahali sehemu ziko tele za kujengewa nini? Za kujengewa vyuo vikuu. Halafu mimi nasema wazi leo hapa ni Pwani kuna Mkikuyu mmoja anaitwa Waitiki. Alikuja mwaka sitini na tatu wakati Kenya ilipopata uhuru. Yeye anasema ardhi ni yake na ekari mia ngapi? Ekari mia tisa na sabini na tano kule juu. Yeye anasema ardhi ni yake.

Mbona sisi tukienda kule kwao hatuwezi kumfanyia ardhi kubwa namna hiyo. Kila siku tunaambiwa Waitiki huyo alikuja na kusema ardhi ile ni yake. Miaka zipi alipatana nami? Twataka tujue yule mtu aliyemuuzia ile ardhi kule juu. Yeye anasema ardhi ni yake, alipewa na nani? Hiyo ni kitu muhimu ambayo twataka tujue sisi. Kila siku tunaambiwa mkikuyu uliyokuwa ukifika huko watu wanafukuzwa na mapanga vizuri sana watu wanapigwa vizuri sana kule juu. Ardhi hiyo kutoka tangu mwaka sitini na tatu mkikuyu huyo anasema ardhi ni yake.

Ardhi ni yake alipewa na nani huyo mkikuyu? Ndio twataka tumjue kuanzia sasa tujue yule mtu aliyemuuzia ile ardhi ambayo ina ekari mia tisa na sabini na tano. Sisi kila siku twateseka hatuna ardhi twaambiwa hii ardhi ni ya mkikuyu mbona sisi hatuendi kule kwao tukaenda vamia? Mbona sisi hatuendi kule kwao tukaenda vamia ndio tukajulikane kweli tuna mambo. Mbona sisi hatuendi kule? Basi sisi tutakazo ni ardhi zetu. Na kitu muhimu ndio hicho. Hiyo ndio kitu muhimu.

Halafu jambo lingine la sita ni juu ya pale Kilindini. 10% ya kila siku yaenda juu. Kwa nini sisi wenyewe hatuwezi kushikilia misimamo yetu. Kila siku twasikia pesa zimekwenda juu. Hiyo mipango twaionaje bwana, lazima tuangalie bwana. Maanake

kila siku twaambiwa sijui nani amekwenda wapi, sijui nani na watu wako tele waliosoma hapa. Hiyo kitu muhimu ndio mtuulilie bwana.

Na habari ya mambo ya nini…pia tulikuwa tunataka habari ya mambo ya …..watoto wetu pia tulikuwa tunataka wapate kazi. Maanake kampuni nyingi kule ukienda wasikia sijui nani mtu ametoka kwao. Watu wa Coast ni wa nne, watu wa kutoka juu ni karibu hamsini. Hiyo kitu bwana lazima tuililie bwana na watu wako tele waliosoma waliofika form four mpaka watu wako tele waliofika University. Kila siku twaambiwa watu wa Coast hatuna maana. Hatuna maana kivipi? Lazima nasi tuangalie bwana.

Halafu na mambo mengine ni juu ya nini? Ni juu ya kuwa sisi twataka tukimalizia tujengewe mahospitali kila mahali. Kwa sababu mahospitali hatuna hapa Likoni kwanza jambo la kwanza hatuna hospitali. Hiyo ndio kitu muhimu. Halafu kitu chengine ni juu ya kuwa twataka nini.. twataka kodi yenyewe tuichukue wenyewe. Twataka yule marikeni za tupatia ile Kilindini, wenyewe tuishikilie wenyewe. Hatutaki habari ya nani, sijui nani atoka huko kwao akuja ang’ang’ania na mambo ya hapa. Hiyo hatutaki.

Twataka mambo ya hapa wenyeji tushikilie wenyewe. Na mimi mwenyewe kutoka juzi natembelea nyumba baada ya nyumba. Nimeogelezwa nimepata nyumba karibu mia tatu. Na tulikuwa tunataka kusaidiwa na msaada kama milioni ngapi? Milioni tano. Twataka tuanzishe biashara za akina mama. Hakuna habari ya nini wala nini. Hiyo ndio kitu muhimu. Na tena akina mama ni watu wa hapa Coast. Sio kuwa ni mtu wa kutoka mbali aje hapa aje atutawale si wenyewe tulewe tu fuaa. Hiyo habari ya kulewa hatuitaki. Lazima sisi nasi tuamke.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Mandingo.

**Mandingo Salim:** Hiyo hatuitaki. Hiyo habari ya kulewa lazima tuamke.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Mandingo. Asante.

**Clapping from the audience.**

**Com. Zein Abubakar:** Haya tumshukuru Mandingo. Asante sana. Rama Muhammed.

**Ramadhani Mohammed:** Salam Alaikum(islam). Ma-commissioners wa Tume na wazazi ama wananchi ama wenye nchi mliohudhuria hapa mimi maoni yangu binafsi kwanza kama mlivyoelezwa na Commissioner kwamba mimi naitwa Ramadhani Muhammed na ni Imam wa msikiti wa Baghani kama alivyotangulia mzungumzaji wa kwanza ama wa kwanza kwanza. Ninazungumza maoni yangu binafsi kwa yale ambayo yalizungumzwa na mwenzangu alikuwa maoni ya maratibu wa msikiti wa Baghani kama msikiti mkongwe katika Likoni hii.

Jambo la kwanza ambalo nalizungumza kama maoni yangu ni kwamba Kenya tunadai…ama kunavyojua upande mwingine tunasema tuna uhuru. Lakini kwa hali ilivyo na ni kwa sababu ya kuwa Katiba tuliyo nayo si Katiba iliyoundwa na wenye nchi ni Katiba ambayo iliundwa na watu ambao sio wenyewe. Ndio sababu yakaja makosa kama haya.

Tukiangalia kidokezo cha kwanza ni kwamba mahakama tulizo nazo ingawaje imeondolewa kaa la moto kwenye upande mwingine kwamba hata mimi mmoja tunataka mahakama za Kadhi ama tunalilia mahakama za kiislamu. Ni kwa sababu mahakama tulizo nazo mtu akishikwa hapa anapelekwa kortini ama mahakamani. Hana kujitetea. Umeshikwa umeiba kitu fulani ama umezingiziwa kuwa una bangi mfukoni. Ni hivyo hivyo tayari mbio. Judge anakubaliana moja kwa moja ni kwamba ni kweli. Ukipinga rumadi miezi sita. Ukija kifungo kinaanza upya.

Kwa hivyo mapendekezo yangu katika Katiba ijayo ni kwamba lazima mshitakiwa na mshitaki watu wawe wazungumze ule ukweli hadharani pale kama ilivyo nchi zingine. Lakini sio kuwa Judge hakuwako. Aliyekuwako ni polisi aliyekushika sasa wewe watoka hii manifesta ama ni Sheikh yeye atoka msikitini pengine kusali pale. Washikwa mbona umeshikwa na bangi. Judge hakuweka uhukumiwe mwaka mzima ama miaka sita. Tayari ni kweli moja kwa moja kwamba askari akiandika malaika hiyo ishakubaliwa.

Kwa hiyo ni sababu ya kuwa Katiba tuliyo nayo si Katiba iliyoundwa na wenye nchi ni Katiba ambayo iliundwa na watu wa Lan Caster House huko, watu na mapendekezo yao. Kwa hivyo Katiba ninayo pendekeza mimi basi iwe inalinda ama inatoa nafasi ya mshitakiwa kujitetea. Sio wote katika sisi ambao tuna uwezo wa kuweka mawakili. Na kwa wale ambao watakuwa ni katika mimi ni kwamba mahakama za Kadhi ndio zitakuwa na uwezo zihukumu katika hali ya mazingira ya kiislamu.

Kidokezo kingine ni kwamba ingawaje kimegusiwa lakini upande mwingine hakikufafanuliwa ni kwamba Katiba tunayoitaka ama ninayoipendekeza mimi ni kwamba iwe itatoa uhuru wa dini. Yaani mtu aheshimiwe kulingana na mazingira yake ya kidini. Si vizuri iwe mimi ninajua wazi mambo ya mavazi ya muislamu ni mavazi kadha. Sasa kutokee kosa la mtu mwingine lizingiziwe kwamba ndio hawa.

Mtu anachukua kidevu kwa sababu ya kuwa kuna mtu fulani yaani kidevu alifanya hivi mtu anahukumiwa kwamba wewe ni katika ……..nafikiri tunajua nikisema hivyo ninasema nini. Watu wanashikwa kwa sababu ya Osama bin Laden. Vazi la kiislamu. Ni (inaudible) na katika uislamu kuweka kidevu. Sasa ukionekana na kidevu wewe basi ni katika wao. Unatiwa ndani. Yale ni mazingira ya kiislamu ama ya kidini lazima kuwe na uhuru katika mazingira ya mtu na dini yake. Kufafanua zaidi ni kwamba katika upande wa mahospitali yetu pia vile vile.

Napendekeza kwamba kuwe na uhuru wa kidini zaidi kwamba akina mama wazalishwe na akina mama. Sio kuwe eti mtu mume azalisha mke. Sasa haya mambo ya vipi tena? Ni dini ipi hiyo? Wako wanawake ambao wana elimu, wamehitimu wana

ujuzi wa kuwazalisha. Leo mume atatolewa sehemu ingine aje azalisha mtu.

Halafu mke huyo atakuwa ana fakhali tele mbele ya yule bwana. Hakuna cha ufakhali. Kwa hiyo kwa kuheshimu mazingira ya kidini na basi na haki katika upande wa mahospitali, madaktari wawe wenye kugawanya huyu atashughulikia upande huu na we washughulikia upande huu.

Kidokezi kingine ambacho ni kuhusu upande wa kutaka…..mapendekezo yangu ni kwamba kwa sababu tunataka Kenya iwe moja kati ya super powers, basi lazima iwe katika mfumo wa majimbo ili kurahisisha usambazaji wa huduma kwa watu. Watu wanakufa mahospitali kwa sababu mpaka madawa ya-signiwe na waziri huko. Inachukua karibu wiki mbili, huku hospitali hazina madawa. Watu wanataka huduma za elimu. Leo watu wanashughulikia miaka thelathini, arobaini, Mkoa wa Pwani hauna chuo. Yaani sote sisi hatuna elimu za kusoma? Hatuna akili za kuwa twaweza kusoma? Lakini ni kwa sababu jambo mpaka lipitishwe wapi? Ili watu wazungumza halafu likakaliwe tena.

Kwa hiyo pia nafikiri katika hali ya mikao, mabwana Commissioner nafikiri nalizungumza hadharani na wengine. Tulikuwa tukisumbuliwa pia ijapo kweli kwamba watueleze kwamba kuna mwaliko hivi mambo yatazungumzwa huko mbele. Kwa hiyo ningechukua nafasi hii pia kuomba isisitizwe kwamba maoni ya wananchi isiwe yanatumiwa tu halafu baadhi ya watu wakakae wayapitishe kizingini. Yawe yatatiliwa maanani. Na ikiwa basi hiyo kunakuwa na ungumu yule aliyekuwa akishikilia upande wake, asimamie upande wake aishe.

Kitu ingine ni kwamba ni jambo ambalo ni muhimu nasi jingine ni ardhi. Kuna baadhi ya watu kama tulivyosikia na watu wanajulikana na sio wa hapa mpaka sehemu zingine. Mtu anakuwa na ardhi ekari elfu moja na zaidi. Hapa kuna wakenya ama wenye nchi elfu mbili wanaitwa ma-squatter hawana ardhi. Sasa hili Katiba hapa sijui….lakini ni kwa sababu haikutungwa na wenye nchi. Imetungwa na watu ambao sio wakenya.

Kwa hivyo mapendekezo yangu ni kwamba Katiba itakayokuja basi itilie maanani ugawaji wa ardhi. Kwanza aangaliwe mwenye nchi sio mwananchi ama mpita njia. Na wale ambao wamechukua mashamba ya watu ama mtu alikwenda kuvamia, kuwe na uwezo ama Katiba iruhusu kuchukua ardhi zile na wagawie watu ambao hawana mashamba wa sehemu ile wa eneo lili. Hayo ni mapendekezo yangu.

La mwisho ni kwamba…ama ni mtu alikuja kunivamia. Kuwe na uwezo ama Katiba iruhusu kuchukua ardhi zile na wagawie watu ambao hawana mashamba wa sehemu ile wa eneo lile. Hayo ni mapendekezo yangu. La pili ama la mwisho ni kwamba kitu kingine kinakuwa ni tatizo sana, mtu katika Katiba ama sijui ni maoni ya mtu, wewe umeajiriwa leo waambiwa wewe uzungumze na mwajili wako. Fisi azungumze na mbuzi waelewane itakuwa vipi. Fisi ataka kula mbuzi, leo mbuzi ambao mwaelewana nyinyi. Tajiri anataka kumtumia mfanyikazi kivyovyote anufaike yeye. Waambiwe wewe zungumza na mwaajili wako muelewane. Kwa hiyo Katiba hapa lazima ikubaliwe ama isimamie mishahara ya wafanyi kazi.

La mwisho kabisa ili kusimamia rasilimali za eneo ama za nchi lazima rasilimali hizi ama wasimamizi wawe wanatoka jimbo lile lile. Wanatoka sehemu ile ile. Na hayo yote hayaji ila mpaka kuwe na mfumo wa majimbo. Kila itakavyokuwa kwa sababu ikiwa kuna mkubwa na watu wamepinga kitu kama hiki basi tutakuwa tuko pale pale hatutaendelea. Lakini kukija mfumo wa majimbo si rahisi mimi nina shamba langu la kahawa nilitie moto niende kwingine. Haiwezekani. Kwa hiyo lazima nitakuwa naliangalia vyema kwa sababu natoka jimbo hili na ninalijua kwamba ni moja kati ya rasilimali zetu. Kwa hivyo rasilimali lazima zisimamiwe na wenyeji wa jimbo lile ili tuwe ni wenye kunufaika zaidi.

Kwa hayo natoa shukrani kwa ma-commissioner wa Tume na wenye nchi kunisikiliza na ninasisitiza ama nakokoteza bwana Commissioner, haya yote yanayozungumzwa katika vikao vyenu yawe kweli yatapewa nafasi zaidi. Kusiinuke mwingine ama baadhi ya watu wakaja wao wako juu kuliko hayo yaliyozungumzwa. Wakati mwingine isije ikaambiwa kuna mashtaka ina maoni tena. Nafikiri kikao hiki pia wewe utaweza kustaajabu kutakuja wana watu kama ishirini kusudi mwajua ni yale (islam).

**Com. Zein Abubakar:** Shukrani Mustadhi Ramadhani. Tafadhali andika jina lako kwenye register pale. Ningependa tu kukuhakikishia kwamba nilikuwa hapa katika elimu ya uraia nikawaambia mambo haya mnayotueleza, Mustadhi wanisikiza?

**Mustadhi Ramadhani:** Twasikizana.

**Com. Zein Abubakar:** Yatarudi hapa hapa tukisha andika ripoti yetu. Myaangalie yamo au hayamo. Sawa. Wamebakia wanafunzi wawili. Nampa nafasi hii Geoffrey Waweru. Mwanafunzi Geoffrey Waweru. Geoffrey yuko. Haraka haraka basi njoo.

**Geoffrey Waweru:** Habari zenu. Kwa majina najulikana Geoffrey maina Waweru. Kwanza kabisa ningependa kuzungumzia kuhusu Kadhi. Sisi wanafunzi twasoma kutoka Standard one mpka eight, mpaka form four, mpaka University twaambiwa hakuna kazi. Na ili hali mtu mmoja ashikilia kazi tano. Kwa nini?

Langu la pili, tukilinganisha kazi ya ualimu na kazi ya mbung, je ni kazi gani muhimu? Na kwa nini walimu wanalipwa mishahara kidogo na wabunge wanalipwa pesa nyingi na ili hali walimu ndio wa muhimu. Kwa nini? Wabunge mimi sioni kazi yao muhimu na ingawa si mwalimu hangekuwa mbunge. Mwalimu amefundisha kutoka Standard one mpaka eight, mpaka form four. Halafu mwalimu huyo huyo ndiye alipwa mshahara kidogo. Na ili hali mbunge yu alipwa maelfu ya pesa. Okey.

Pointi yangu ya tatu. Hawa wabunge ambao mwawasikia wanalipwa pesa nyingi lakini kwa unyakuzi wa ardhi wako, kwa unyakuzi wa vyeo vya …. wako, ma plot wako sasa tueleweje lakini. Tueleweje? Ya tatu ni corruption. Kenya yetu ino twasema economy, economy iko chini na ili hali vitu hivi vyote vya Kenya tunaovikuza hapa, maili tuviuze hapa wakuta kuna vingine vyatolewa ng'ambo. Tu-choose kwa mfano sukari. Sukari hutoka ng'ambo ikaletwa hapa na ili hali hapa Mombasa

kwenyewe kuna kiwanda kilifungwa kikiuza sukari. Kwa nini? Kwa nini na hatufaidiki? Hatufaidiki na kile ambao tunakipanda hapa. Tunaletewa vitu kutoka ng'ambo. Kwani hao ma-ministers wana-appointiwa wanafanya kazi gani?

Langu la nne ni kuhusu freedom fighters. Kenya twajua ilikombolewa na watu fulani na twawamanya basi ni watu gani na gani na gani? Lakini watu hawa hatuwatilii maanani. Bunge hawaangaliliwi tukichukua mfano Paul Ngei nilisikia sijui ni mwaka gani alikuwa akifukuzwa ati hajalipa rent. Nikichukulia mfano mwingine Munyao. Aliyepandisha bendera ya Kenya huko juu sijui Mt. Kenya wala mountain nini? Juzi juzi pia ati yeye amekosa pesa za matibabu ya hospitali. Je huu ni ungwana jamani. Watu hawa yafaa tuwaangalie na yafaa pia wawe na sikukuu yao maalum twasherekea. Kwani si tutasikia tu sikukuu za watu Moi day, Biwott day, nani day, kwa nini? Kwa nini hatuna freedom fighting day kila siku tuwe tukasherekea pia sisi. Asanteni

**Clapping from the audience.**

**Com. Zein Abubakar:** Asante Geoffrey. Tunarudi kwenye orodha yetu, bwana Naftal Swale. Nasoro Swale.

**Nasoro Swale:** (Islam). Wazee wangu pamoja na macommissioner hamjambo. Asanteni sana. Ningependekeza Serikali pamoja na Katiba ilinde maoni yetu na iyatilie maanani. Jina langu naitwa Nasoro Swale. Kama tunavyojua kuwa ardhi ni msingi wa maendeleo. Tungependelea kwamba Katiba itilie maanani jambo la mashamba hasa kama vile utoaji wa hati za kumiliki mashamba tena hasa kwa wenyeji wa Pwani. Na endapo kutatokea na uuzaji wa ardhi za sehemu fulani hasa vihusishwe wenyeji wa sehemu hiyo ama wazee wa mitaa.

Lazima Serikali iwe na uwezo wa kuchukua ardhi ya mtu binafsi akiwa haitumii kwa manufaa yeyote ili wapatiwe wasiokuwa na mashamba. Serikali za mitaa ziwe na uwezo wa kudhibiti ardhi zile zinazotumiwa. Kwa mfano kama Vipingo ni shamba kubwa sana lakini naona halitumiwi kwa chochote bali kwengine kwa upande wa makonge na haifaidishi mwananchi yeyote wa Pwani. Ama kwa mfano kama vile Ramisi saa hii ni msitu.

Ikiwa mwenyeji wa hapa pia hana hata acre moja. Serikali za mitaa, wazee wa mitaa na mahakama ya Kadhi lazima lishughulikie ubadilishaji na uridhishaji wa ardhi kwa watu wanaohusika kama vile wafiliwa. Kwa mtu binafsi tungependa awe na kiwango cha acre ishirini peke yake ili hali wengine wapate. Samahani. Sababu kuna wengine humiliki ardhi kubwa kuliko wenyeji wa kijizingizia hizo ardhi waliuziwa. Kwa mtu ambaye si mkaaji wa mkoa ule, lazima kuwe na vikwazo vya kumiliki shamba hilo analolikalia.

Mfano kama si mtu wa eneo hilo la Pwani. Hasa kuhusu watu kama wale ambao si watu wa Pwani na wanakalia ardhi wakizingizia kuwa walilinunua shamba hilo lazima liwe na vikwazo. Kwa sababu ni makosa ikiwa kama mimi sina hata nusu acre lakini nasikia kuna mtu ana acre mia tisa.

Jambo jingine kwa sababu sitaki kusema mambo mengi sana. Mimi ni raia wa Kenya, mzaliwa wa Kenya, ma-commissioner hii ni birth certificate. Ningewaomba niwapatie hii kwa sababu ni- na zingine mkazifananishe na zile birth certificates zenu ama za watu wengine. Kwa sababu kosa la hii birth certificate ndio ni ya mtoto wangu, mimi ni babake. Asanteni.

**(Women session hearing with Com. Prof. Wanjiku Kabira).**

**Mwanamwinyi Hussein:** Jina langu ni Mwanamwinyi Hussein. Sasa ninavyotaka mimi Serikali yetu nataka iwe ya majimbo. Tumechoka sasa kunyanyaswa nyanyaswa twataka hii ya majimbo na watoto wetu wa kwanzia hapa Mombasa wote watoto wawe na kazi. Na tukieleza twaambiwa hatusomi na tuna watoto ambao wamesoma. Wasichana, wavulana hilo ni jambo langu la pili.

Jambo langu la tatu nataka tupatiwe ardhi yetu kama inavyowezekana na Serikali. Jambo langu la nne ni kuwa sisi tukifiliwa na mabwana zetu huwa ile haki yetu hatupatiwi. Hatupatiwi kabisa. Twaambia 'wewe haya bwanako ashakufa nenda zako, nenda zako'. Sasa hilo pia Serikali waliangalie. Jambo letu la nne ni elimu. Twataka irudi vile vile itusaidie. Kama nilivyokwambia elimu ilikuwa ya bure. Ilikuwa ya bure mbele sasa hivi sasa hata ukipeleka mtoto class ya kwanza mpaka uwe na pesa chungu nzima. Wengine wana uwezo na wengine hawana uwezo. Kwa hivyo mimi mambo yangu ni hayo na Serikali wayaangalie.

Na upande wetu wa dini. Kama kutawezekana Chief Kadhi wetu sisi wenyewe tunaweza kumchagua. Anayetuwakilisha sisi. Kama kutakuwa na upande pia kuwe na mwanamke ambao tuna matatizo yetu tunaweza kumueleza. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Kuwe na wanawake wengine …….

**Mwanamwinyi Hussein:** Waeko. Maanake sasa hatupati ni yeye tu peke yake. Hata ukiwa na maneno yako pengine ya siri nini huwezi taja.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Huwezi kumuambia.

**Mwanamwinyi Hussein:** Sasa kuwe na mwanamke pengine anayeweza kwenda naye chini yake tukawa tutaongea naye.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Na mambo ya akina mama?

**Mwanamwinyi Hussein:** Mambo ya akina mama ya vikundi?

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Yes.

**Mwanamwinyi Hussein:** Pia zaendeleze mambo yetu ya vikundi ya akina mama. Sasa tukiwa tutaendeleza na kikundi chetu kitakuwa ni raha.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Na mambo ya akina mama katika uongozi?

**Mwanamwinyi Hussein:** Uongozi pia. Pia twataka uongozi wa akina mama. Maanake sasa akina mama si wanawekwa nyuma sana. Akina mama wamewekwa nyuma na akina mama ndio wanaozaa akina baba lazima wapewe cheo yao nayo kidogo. Kwa hivyo mimi maoni yangu ni hayo.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Asante sana. Sijui kama mama utakuja hapa karibu na mimi kwa sababu ya hii recorder. Na utaje jina.

**Sophia:** Naitwa Sophia

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sophia? Na hiyo ingine.

**Sophia:** Jina?

**Interjection:** Asema jina lake yu aitwa Sophia.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sophia?

**Audience:** Naam.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sophia, lakini una jina moja tu?

**Sophia:** Jina moja.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Ni sawa.

**Sophia:** Nasema hivi kuhusu habari ya ardhi. Umepata ardhi, umeipata umeijenga na ungali msichana mpaka umezaa, mpaka umejukuu bado unalipa kiwanja. Sasa yule mwenye kiwanja anasema ikiwa unataka kiwanja utoke shilingi elfu arobaini na tano nikuuzie kiwanja. Na miaka yote hiyo niliyokaa nina haki sasa atupatie kiwanja. Sasa bado sisi tuwe tukilipa mimi nife mama na mjukuu wangu naye akae, azae bado aendelea kulipa kiwanja mpaka miaka mingapi sisi tunakuwa tunalipa? Si ni miaka mingi unalipa tu kiwanja. Sasa tunahitaji sasa yule mwenye kiwanja ameshatajirika kitambo sana kutoka enzi za marehemu Kenyatta

huku alipa kodi ya kiwanja mpaka dakika hii. Sasa atupatie nafasi sisi atupatie viwanja bila kulipa.

Na kitu chengine ni kuhusu mahabusu ambao wamefungwa. Wanavyoteswa si halali na chakula wanachopawa si kizuri. Lazima waangaliwe kwa mambo ya kigonjwa na kuangaliwa vile maisha mazuri anavyoishi, pahali pa kulala mahabusu. Tunalilia mahabusu waangaliwe vizuri. Yangu ni hayo.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Asante sana.

**Sophia:** Hii ni yangu.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Hii ni yako. Okey asante.

**Sophia Abdul:** Mimi naitwa Sophia Abdul Amani

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Abdul?

**Sophia Abdul:** Amani.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey.

**Sophia Abdul:** Mimi ningependelea Serikali ya majimbo kwa sababu Serikali ya majimbo ndiyo itatuletea maendeleo. Kila mmoja akasaidie mkoa wake ili watu wote wawe na manufaa. Manufaa ya kiugonjwa ni hospitali, manufaa kwa misaada ya wote itakuwa ikiwa ikitokana na Serikali. Kwa sababu sehemu za bara kuna shule watu wanataka misaada ya pesa kule sides za juu lakini kama hapa Pwani watu hawapati msaada wa aina yeyote. Watoto wanasoma wanakaa tu.

Na pia ningependa tujengewe shule kuu University. Tuwe nazo za kutosha. Mbili ama tatu maanake hapa mtu akipita mpaka aende bara. Halafu kitu kingine ningetaka ni hospitali. Kuwe na vifaa na mabara. Hapa hospitali ni za bure lakini ni bure je na ukienda mpaka utoe pesa ndio upate matibabu. Halafu kama wagonjwa wa ukimwi. Wagonjwa wa ukimwi pia wangefaa wapate misaada kutokana na Serikali. Kama ni ya vyakula na madawa mpaka mtu afe.

Mambo ya kusimamishwa kazi mtu akitokea na ugonjwa kama wa ukimwi hivi ni vibaya. Mtu akafanye kazi mpaka dakika ya mwisho ambayo itakuwa hajiwezi halafu ndio akae.

Halafu upande wa ardhi: Upande wa ardhi watu wenye ardhi kubwa zaidi wangefaa wachunguzwe. Kuwe kuna kiwango fulani cha umilikaji wa ardhi. Kuwe na …..tuseme kama acre kumi na zaidi kuendelea maanake utakuta nikwaambie pengine si

mwenyeji wa pale, amekuja na ameshika ardhi zaidi kama ya acre kumi, ishirini, na ana title deed. Na wenyeji wa pale ambao wana acre mbili, kamoja hawana title deed achunguzwe. Kuwe kuna kiwango ambacho mtu asiwe na zaidi ya acres kadha za ardhi maanake wengi wao huwa ndio wanyang'anyi.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Na upande wa akina mama?

**Sophia Abdul:** Na upande wa makazi pia watu watasaidika kwa sababu kama ni hapa Coast kama tuseme pale Coast mkubwa anawekwa ni wa Pwani anahakikisha kutakuwa na kiwango fulani kama 75% itakuwa ni ya wapwani, asilimia ishirini na tano itakuwa ni ya wabara. Lakini kwa hapo utakuta wapwani kama sehemu ingine ni kidogo wabara ndio wengi sana.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Na upande wa akina mama.

**Sophia Abdul:** Kwa upande wa akina mama pia kwa maendeleo kama sehemu za bara utakuta watu wakipata misaada, wanapata misaada sawa sawa ambayo wanajiendeleza lakini kama sisi hapa wapwani, kukija misaada msaada kidogo ambao hata haiwezi kukunufaisha na chochote.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Una ingine. Ongeza tu ukiwa una ingine.

**Interjection:** Kama una nyingine ongeza hata kama ushazungumza.

**Sophia Abdul:** Naeleza pia kwa upande mwingine kama wa misaada kama ya wakulima sisi watu wa Pwani twaambiwa tuko nyuma sana eti ni wavivu lakini ni vifaa tu na kama wenzetu wa bara hupewa misaada ya mbolea, vifaa kama tractors za kwenda kulimia. Lakini kama sisi hapa hatupati misaada yeyote. Endapo sisi tungepata misaada kama hiyo pia na sisi tungeweza kupata mazao mazuri.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana akina mama. Okey.

**Asha Juma:** Nataka  kwamba Serikali iwe Serikali ya *majimbo*.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Taja jina lako?

**Asha Juma:** Jina. Bi. Asha Juma.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Umesema jina la pili ni gani?

**Asha Juma:** Juma. Niendelee.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sawa.

**Asha Juma:** Serikali ya majimbo, kila jimbo iwe ikijitawala yenyewe. Tuseme kama mambo ya kazi, majority ambayo wataandikwa kazi wawe wa sehemu ile yaani wawe wa lile jimbo.

**Frida Mwadime:** Endelea tu.

**Asha Juma:** Pili ningesema kuhusu mambo ya elimu. Hasa tuseme kama hivi skuli, form four hivi, watu wakifanya mtihani wakimaliza, kuna wale ambao huwa wana-pass na wale huwa wana-fail. Kwa hivyo katika hii sehemu yetu tuseme mambo ya kuandikwa kazi ama college unaambiwa kuwa college mtu lazima awe na C+ ndio apate college. Na kuna lazima wengine ambao wame-fail sasa katika hiyo Serikali itakayokuja hawa failures pia waangaliwe watafanyiwa mpango gani. Kwa sababu kila college inaanzisha kwa C+ na lazima kuna ambao wata-fail watapata D- ama D+ kwa kusema hao wamepangiwa mpango gani. Wangepangiwa wafanye kazi kama zile za polisi, kama hao wakisema za polisi, za seremala zinaweza kuwa zikiwafaa watu kama hawa.

Halafu jambo lingine ni la kuhusu Chief Kadhi. Sisi waislamu tunataka Chief Kadhi tumchague sisi wenyewe. Na katika ofisi ya Chief Kadhi pia kuwe na wanawake ambao wanafanya kazi pale kwa sababu kuna mambo mengine ya kike wataka umuelezee mwanamke. Katika hiyo ofisi ya Chief Kadhi tuwe pia na wanawake ambao wameandikwa kazi hapo.

Jambo lingine ni kuhusu sisi wanawake. Twataka pia tuchaguliwe kama wabunge ama tupewe vyeo fulani katika Serikali. Halafu kuhusu health. Tunataka tujengewe hospitali. Hospitali ambazo ziko na vifaa na za bei nafuu.

Mambo ya kazi pia kusiwe na ubinafsi. Ubinafsi yaani nikisema kuwa wewe umeandikwa kazi u mjaluo uandike watu wajaluo wenzako aah. Tuondoe ubinafsi kuwa twachanganyika. Tukiandikwa kazi twachanganyika kwenye kazi.

**Frida Mwadime:** Tosha.

**Asha Juma:** Tosha.

**Frida Mwadime:** Commissioner do you have any question?

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Kuna mambo mengine ambayo ungetaka kuzungumza juu ya wanawake?

**Asha Juma:** Juu ya wanawake?

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Kwa sababu tuko hapa leo.

**Asha Juma:** Juu ya wanawake kuna lile ningesema juu ya wanawake. Kuna haya mambo tuseme umeolewa na bwana. Umekaa naye, umezaa watoto halafu yule bwana anakufukuza. Juu ya kukufukuza kabisa ashaleta bibi mwingine. Sasa wakuta wewe ulikaa naye, mkajenga mkanunua vitu sasa zile vitu hazikufai. Anakufukuza na haupati kitu chochote pale. Sasa Serikali pia iangalie mambo kama hayo. Sio bwana akufukuze uende kabisa ukapate shida yeye alete bibi mwingine akae. Mambo kama hayo pia yafaa yaangaliwe.

Halafu mambo ya rape. Mtu aki-rape iwekwe miaka fulani ambayo ataadhiibiwa. Aadhibiwe kabisa mtu aki-rape. Na haya ya kupigwa na mabwana. Bwana amekuja amelewa, anakupiga, hayo pia twataka yaangaliwe.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira :** Ni sawa. Utaandika jina?

**Asha Juma:** Kule nishaandika tayari.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira :** Umeandika?

**Asha Juma:** Naam.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira :** Okey.

**Asha Juma:** Na sisi wanawake wa huku Coast pia twataka tupewe at least tuongoze kidogo. Huku Coast wanawake wajua pia wame……

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Viongozi kama Councillors au…

**Asha Juma:** Kama Councillors kama wabunge, nominated tuseme.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** So you are saying wanawake wawe nominated?

**Asha Juma:** Wakuwe nominated. Councillors na kwa bunge pia.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Wote.

**Asha Juma:** Naam.Wanawake tupewe haki zetu.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Asante sana. You know my feet are swollen and I can't lift my leg.

**Frida Mwadime:** I think it is because of the heat and also travelling. You know you have to stretch them somehow.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** You know I can't stretch them until**…(interjection)**

**Frida Mwadime:** Then tomorrow you are also travelling.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** No, tomorrow we have a meeting.

**Frida Mwadime:** The meeting at Nyali beach?

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Yes.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Unajua tukiandika na tuki-record itakuwa rahisi kwenda kuandika mambo vile inatakikana.

**Sauda Ali:** Ni sawa.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Unaitwa?

**Sauda Ali:** Sauda.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sauda?

**Sauda Ali:** Sauda Ali. Mimi maoni yangu ilikuwa ni kwa upande wa wafanyikazi. Kwa upande wa wafanyikazi. Kwa upande wa wafanyikazi kuna wengine tumeamua dini ya kiislamu bora ufanye kazi. Kwa yule aliyeandikwa zamani mfano kama mtu aliyeandikwa mwaka wa sitini na saba, ameitumikia hiyo baraza kwa muda huo wowote.

Pamekuja mtu ambaye ameandikwa mwaka wa tisaini na saba hilo tuseme saba. Na pia ukiangalia ile darasa alilolifika sio kwamba ni trained enough. Yeye anapatiwa sehemu ya juu na wewe unapatiwa ya chini. Ambapo hayo ni maonevu sana. Hata pia ile kazi sijui atafanya nini. Hiyo nafikiri si jambo nzuri sana. Na kama uko nayo hiyo post uwe ni acting ambayo hupati allowance yeyote ni wewe unatumika pale. Wewe bado uko stage ya chini, yule aliyeandikwa juzi amekwenda juu. Hiyo si

vizuri.

Kwa hivyo yule anayehusika yafaa kuangaliwa. Aangalie yule mtu wa zamani ni mimi. Ama kama ni kwa habari ya pengine education sawa lakini pengine ukiangalia education yake pia hayuko firm vile. Mtu alitoka standard four amepita huyo mtu wa eight ama form four. Hiyo ningetaka iangaliwe. Kwa hivyo hapo tunaomba wale wanaohusika waangalie sana Serikali. Wafanyikazi ni muhimu sio kuwanyanyasa ama si kuangalia kwa sababu yule alinipigia kura hawa wengine hawafai. Hiyo si vizuri kuangalia yule mwingine.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Una nyingine?

**Sauda Ali:** Hiyo ndio nilikuwa nayo. Kweli inaniumiza.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Na wanawake?

**Sauda Ali:** Wanawake imeongewa.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Imeongewa?

**Sauda Ali:** Naam. Imeongewa na watu kule. Sio eti kwa sababu sisi ni akina mama tuwe tunabeba mimba, akina mama sijui ndio walevi. Kwanza sisi akina mama hasa ukiangalia upande wa akina baba, mama wakati mtoto ni mchanga mpaka anakua* yuko shuleni huwa ni mtoto wa mama. Akipata kazi ni mtoto wa baba. Ambayo hiyo huwa si vizuri. Hata akifanya kosa anaambiwa 'kwenda mueleze mama'. Lakini akiwa ni mkubwa anajitegemea ni shida yake. Hiyo pia hatupendelei. Kwa sababu yule mama haoni raha kuwa eti mtoto wake atamhimili .

Lazima na wewe upate faida ya mtoto. Ama kama amefanya makosa lazima ukae na mtoto umuelezee sio kusema …akina baba wanatwambia 'hayo makosa yote ni yako'. Kama msichana amepata mimba atakuambia ni mamake. Lakini huyu mvulana akimtia msichana mimba, kwa nini sisi akina bibi hatusemi ni baba ndiye aliyekosea. Lakini msichana tunaambiwa mama mwenye makosa. Hiyo si vizuri.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Sio vizuri.

**Sauda Ali:** Yangu ni hayo nashukuru. Nimekaa muda mrefu nikisubiri.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey asante sana.

**Joseph Muchele:** Media upande wa siasa: Tunasema Kenya ni nchi iko huru iko democracia lakini utashangaa ukienda kuangalia matangazo KBC inazungumzia ile Serikali ambayo iko mamlakani saa hii. Ni Moi atazungumziwa dakika kumi na tano. Vitu ambavyo vinahusiana na Serikali au wanadamu wengine ambao pia ni wanasiasa na wako katika nchi ambayo iko na democracia hawatambulikani. Mikutano ya kisiasa wa kipanga hawasaidiwi.

Mwisho mikutano ya mwisho mwisho inafanya nini? Inaambiwa hiyo mikutano ikavunjwe. Polisi wanaletwa pale. Je ni kwa nini tume-register hivi vyama vyao? Ni kwa nini tumeleta hii multi-party? Tumeleta multi-party ili tuje kujaribiana tuone nani ana nguvu ya kuweza kumpiga mwenzake hilo jambo likaweze kuangaliwa. Jambo lingine kuhusu elimu tunayozungumzia Kenya.

Kusema kweli mimi nimesoma katika elimu ya 8-4-4 lakini nataka kusema hivi elimu hii haijakuwa na maana yeyote ya kusaidia raia wa Kenya. Tumekuwa na watu ambao vile ndugu yangu Swaki amesema ni wasomi wamefundishwa kutoka kwa vitabu ambavyo vinabadilika mwaka baada ya mwingine lakini hawana matumaini. Kwa sababu gani? Tunasoma tu na hatujui kwa nini tunasoma. Elimu imeletwa Kenya ile ya 8-4-4 haina mwelekeo wa kuweza kuelekeza watu kwa hivyo hiyo elimu ikaweze kuchunguzwa ikaweze kuwa ni elimu ambayo inakuwa na future ni kwa sababu ya watu wa Kenya.

Jambo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia kama raia wa Kenya ni uhuru wa kuabudu. Mimi ni mkristu na sio mkristu peke yake mimi ni mu-Adventista Seventh Day Adventist. Mwaka mwingine nikaona tuna……kulikuwa kunahesabiwa watu wapendwa. Nilishangaa kuona kitu kimoja nikaona kwa ile form wanasema muislamu, mu-katholiki, mtu mwingine halafu hizi dini zingine wanaweka neno 'others'. Yaani hautambulikani wewe. Na una Mungu unamwabudu. Yaani wewe dini yako imewekwa 'others' na wewe unaambiwa sasa ui-identify. That is very bad. Natunasema tuna uhuru wa kufanya nini? Wa kuabudu. Hiyo ni kitu inaumiza.

Huu uhuru wa kuabudu ukaweze kuwekwa……ukiwekwa ni uhuru wa kuabudu muislamu apatiwe ijumaa ijulikane ni siku yake ya kwenda msikitini akazungumze na Mungu wake mambo yake yote siku hiyo yote. Hata kazini asiende. Yeye asichanganye mambo mawili kumwabudu Mungu na kufanya kazi. Akamwelekea yeye mtu anayeabudu sabatu mimi hapa. Sabatu ikifika ijumaa jioni niwe na hiyo freedom kama raia wa Kenya nipumzike nifurahie.

Mungu ameniumba ameniweka katika nchi ambayo iko huru. Kuna watu wengine wanahangaika nikaweze kufanya nini? Kuabudu. Nimekuwa na shida hata saa hii huwezi kupata kibarua kama mimi nimekaa three years ninatafuta kazi unaambiwa uchague kati ya kazi na huyo Mungu wako. Na huyo ni raia wa nchi ya Kenya mwenzako anaye kwambia hivyo. Utaambiwa uchague kazi ama nani? Mungu. Na nimechagua Mungu na amenisaidia. Kwa hivyo nataka kusema Katiba itupatie uhuru wa kuabudu kabisa kabisa tusiwe na vikwazo. Mtu apatiwe nafasi ile siku anayomuabudu Mungu.

Wabunge wasipatiwe ofisi kule Nairobi kule headquarters za Parliament huko ndio wanazunguka anakuja huku kama hana kazi

ya kufanya. Wapatiwe maofisi pale katika maeneo ya uakilishi wa bungeni. Hapo awe na ofisi hapo ofisi yake kubwa iwe ni hapo. Hata kule ambapo ninasema ni Bunge ndio awe anaonekana kwa muda muchache.

Lakini kwa sababu hawa watu alichaguliwa awahudumie, akae nao ajue wamelala namna gani? Nani ni mgonjwa? Ni barabara gani imeporomoka ni daraja gani imeharibika? Si kusikia daraja imeharibika mahali ndio unakimbia kutoka huko na watu wako wameangalia. Naomba Mungu akaweze kutusaidia tunapokuwa tunafanya kruekebisha Katiba tena tukaanza kumtegemea huyu Mungu na tukaweze kuomba uongozi wake kwa sababu tukitaka pia kutumia uongozi wetu sisi tukaweka Katiba ambayo pia itakuja kutuangamiza. Naomba Mungu akaweze kutubariki.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Tafadhali andika register yetu kwamba umetoa maoni. Kuna mmoja wetu ambaye alikuwa ametoa maoni mapema anaitwa Abdul Shabani na akasema atakuwa na ushahidi wa maagano ya mwaka sitini na tatu ya Lan Caster na sasa anayo maagano hayo anataka kutoa copy kwa Tume. Shabani mara moja.

**Abdul Shabani:** Salam Alaikum tena. Nafikiri kutokana na yale niliyozungumza mwanzo kuhusiana na mwambao wa Pwani, historia ya huku nilikuwa nina mkataba hapa ambao uliandikwa na Waziri Mkuu Bwana Jomo Kenyatta na Waziri wa Zanzibar Bwana Mohammed Shamuti. Naningewazilisha ili ukawe mswada anaozidi kujadiliwa na haki itimizwe. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Muhammed Juma Kizuri.

**Muhammed Juma Kizuri:** Salam Alaikum (islam). Nafikiri kwapo kiapo ambapo tumefikia wazungumzaji wamegusia sehemu mbali mbali mimi langu nitazungumzia sehemu chache. Kwanza, nitazungumzia kwa upande wa elimu. Nafikiri sote tunaelewa kuwa mambo ya elimu ni haki ya msingi na ambayo ni haki ambayo nafikiri inaweza kuja ya kwanza kabisa. Kwa sababu kila mwanadamu akiumwa lakini kitu cha kwanza ambacho anatakikana awe nacho ni elimu. Kwa hiyo kimaoni yangu vile ambavyo naona ni kwamba katika sehemu ambayo tuko nayo ni kwamba lazima elimu Katiba ile iwe itatilia maanani sana.

Nikisema hivyo nafikiri wasemaji wengine wamesema elimu katika Katiba iwe ni ya bure lakini la muhimu zaidi iwe ni ya bure na pia iwe ni ya sawa. Kwa sababu hii elimu ambayo tunasema iwe ni ya bure lakini katika hii elimu mimi sioni usawa wowote. Nikisema hivyo tukiangalia katika historia mji kama wa Mombasa nafikiri Mombasa ni katika ile miji ya mwanzo mwanzo kabisa hapa Kenya lakini kwa upande wa elimu ifuzwa zaidi. Utaona watu wanalia kuwa wanahitaji University, sio University peke yake unaangalia Mkoa wa Pwani mzima ama sehemu kama hii ya Mombasa ukiangalia colleges pia ni chache.

Schools: Ukiangalia pengine national schools, provincial schools pia ni chache kwa hivyo ni kwamba tukiangalia Kenya nzima huu Mkoa wa Pwani unakuwa uko nyuma sana kwa upande wa elimu. Kweli nikitaja kwa mfano colleges, unaona katika Mkoa wa Pwani nafikiri tunasifika sana kwa mambo ya utalii lakini panapoangaliwa labda college inatakikana kujengwa, tuchukulie *Utalii College*. Hapa Pwani nafikiri wageni wengi wakija wanakimbilia Pwani kwa sababu ya bahari, kuna mambo ya Tsavo

East, Tsavo West kwa sababu ya wanyama lakini *Utalii College* ikajengwa sehemu kama Nairobi.

Kwa hivyo ndio pale nasema katika mambo ya elimu hakuna usawa wowote. Lakini kama kungekuwa na usawa ni kwamba college kama ile tungekuwa nao pia hapa na pia mpaka dakika hii kwa sababu katika town ama miji Mombasa ni katika ile miji ya zamani kabisa. Lakini mpaka dakika hii kielimu imekuwa iko nyuma kwa sababu hakuna usawa wowote. Kwa hivyo elimu iwe ni ya bure na pia kuwe na usawa.

Jambo lingine katika elimu ni kwamba kuna kitu chengine kinaitwa specialization. Nafikiri kuna mwenzetu hapa amekuja akasema kuwa degrees za hapa Kenya ukienda sehemu zingine unaambiwa hizo ni fake. Sasa degrees kama zile zinakuwa labda zinatambulikana kama ni fake, sio fake lakini mfumo wa ile elimu yenyewe ndio inafanya mtu kama yule elimu yake inakuwa ni ndogo sana.

Kwa hiyo tukiwa na specialization nafikiri wakenya watakuwa na elimu ya hali ya juu. Tukichukulia mfano kama nchi za magharibi ama wazungu. Wanakuwa na specialization. Mtoto anasoma miaka kidogo, anachunguzwa na anajulikana huyu mtoto labda ni mzuri katika masomo fulani kwa hiyo anaangalia yale masomo sio kurundikwa masomo yote kwa jumla. Sasa mwisho atakuwa amesoma sana lakini hajashika kabisa lile ambalo linatakikana.

Lakini kwa hiyo katika mfumo wa elimu yetu pia kupatikana specialization kwanzia Primary school, Secondary school na kwenda huko juu. Jambo lingine ambalo Serikali katika hiyo Katiba liangalie ni kwamba nafikiri tukiangalia saa hii, elimu imegeuka imekuwa ni ya matajiri. Maskini wanasoma lakini kwa kiwango kidogo sana na pia kwa dhiki.

Kwa hivyo katika hiyo Katiba inone Serikali itasaidia vipi wananchi ambao ni wanyonge wataendelea kimasomo vipi? Lakini ikiendelea vile ambavyo imeachwa hivyo ni kwamba wale ambao watafaidi kila siku ni matajiri na maskini watakuwa ni maskini, pesa hawana na umaskini wengine ambao tutawapata pia ni kwamba elimu watakuwa hawana. Nikiingilia upande mwingine haraka haraka kwa upande wa ardhi hapa nafikiri kuna mwenzetu mwingine amesema sisi watu wa Pwani tunalia lia sana. Sio kuwa tunalia lia sana. Ni vile ilivyokuwa na ile hali ambayo tuko nayo ndio ni ngumu zaidi.

Kwa hiyo kwa maoni yangu vile vifungu ambavyo vinasimamia mambo ya ardhi vipitiwe katika hiyo Katiba na viangaliwe viwe ni vyenye manufaa kwa watu wote lakini sio watu kidogo. Tukitoa mfano nafikiri hapa katika makao makuu ambayo inashughulikia mambo ya ardhi, unaweza uko na tatizo lako hapa lakini uende Nairobi. Sasa unaona shughuli kama hizo ndio inakuwa ni dhiki kabisa. Kwa sababu ukifika kule unaenda kukumbana na mambo kama corruption. Kwanza wewe umetoka huku mbali labda centi zako ni kidogo.

Kwa hivyo ingekuwa ni vizuri katika hiyo Katiba ambayo itakuja headquarters kama zile za mambo ya lands, mambo ya ardhi ziwe kwenye mikoa ili wananchi iwe ni rahisi kufika pale na kuangalia shida zao kuliko kwenda kule na ukifika kule unachelewa,

pesa zimekuwa kidogo unarudi kabla shida yako haijaangaliwa.

Na jambo lingine ambalo nafikiri nitamalizia hapo ni kwamba nafikiri tumeona watu wamewasilisha matatizo aina aina lakini kimaoni yangu nafikiri kila ugonjwa huwa uko na dawa yake. Na hii Katiba ambayo saa hii tunazungumzia hapa ni Katiba ambayo itabidi iandikwe. Lakini kabla ya hapo tujiulize 'Je Katiba ilikuweko, iliandikwa ama haikuandikwa.' Je kivitendo ilikuwa inafanyika. Kwa mfano kwenye hiyo Katiba nafikiri katika haki za mwananchi, utapata kuwa mwananchi yuko na haki ya elimu ya bure.

Hiyo Katiba ambayo tayari ndiyo inafanya kazi iliandikwa kutoka wakati huo. Lakini ni kwamba ilikuwa haifuatwi hivyo. Katika hiyo hiyo Katiba inasema mwananchi yuko na haki ya kutembea sehemu yeyote hapa Kenya. Je ilikuwa ikifuatwa. Ilikuwa haifuatwi kwa sababu unaweza kupatikana labda hata sio usiku lakini pia unaulizwa 'unaenda wapi? Lete kitambulisho, umetoa lakini unaambiwa hapana na labda ni saa mbili za usiku unaambiwa kwa nini unazurura.

Kweli ni kwamba katika haya ambayo tunayazungumza ni kweli tunatoa maoni, itawekwa katika maandishi lakini kazi kubwa yale maandishi kitu ambacho sisi tunaomba ni kwamba yawe yatatumika. Sio kuandikwa tu halafu iachiliwe mbali. Itakuwa sisi hapa tumepoteza wakati wetu bure. Na sisi tuwe tuko tayari kwa sababu usiwe na uhakika ukasema ' aah tumesema hivi itakuwa hivo. ' Kimaandishi itakuwa hivyo. Lakini kitu ambacho tunalilia iwe kivitendo.

Ile Katiba ambayo itakuja ambayo saa hii tunajadiliana iwe ni kivitendo sio kimaandishi tu ni jibuku limewekwa ati ndio ukipatikana na makosa linafunguliwa. Aah, iwe kama ni kweli iliandikwa pale elimu ni ya bure, iwe ni ya bure kweli. Mwananchi ana haki ya kutembea pale anataka iwe ni kweli. Mwananchi yuko na haki ya dini ama ya kuabudu iwe ni kweli kwa vitendo. Na kuna watu waliotangulia nafikiri wamezungumzia mifumo ya Serikali. Hii Serikali ambayo tuko nayo saa hii mfumo wake ni kwamba ni Serikali ya mseto. Lakini nafikiri tumetaja maradhi. Kuna mmoja wetu amesema hapa kuna matatizo, Kenya nzima secondary school ni moja tu ya walemavu, nafikiri vipofu.

Wengine wanakuja hapa wanazungumza, wanaongea matatizo ya ardhi. Wengine wanakuja hapa wanazungumza wanaongea matatizo ya elimu. Lakini kimaoni yangu hiyo Katiba ambayo inakuja nafikiri kwa gua ugonjwa huu ama tatizo hili itakuwa vyema kama tutakuwa na Serikali ya majimbo. Nikisema hivyo kwa mfano elimu hapa Pwani kila siku tunalia elimu sisi hatuko sawa na wale wenzetu. Unaangalia hii Secondary hapa *Likoni Secondary School,* hii haiko sawa na zile zingine kule.

Labda unaingia hapa pameandikwa laboratory pale, lab ile, ukiingia labda wanafunzi wote hiyo hizo vifaa ni kidogo sana. Huyu mtoto ambaye yuko Likoni Secondary hapa atafanya mtihani ule ule ambao mtoto yuko Nairobi Boys huko atafanya ama Lenana. Lakini shule zao ziko tofauti na hizi. Hapo kutakuwa na usawa?

Kwa hivyo nafikiri usawa utapatikana baada ya majimbo, Serikali zikiwa na majimbo. Kwa sababu kila jimbo litaangalia elimu

kwa watu wake itaenda vipi. Hiyo ni faida moja ya majimbo. Humu humu unatembea utaenda kuona kijishule labda primary school yaani kinaanguka kabisa ambapo hii Mombasa iko na rasilimali nyingi sana. Mombasa iko na utajiri mwingi sana.

Lakini utapata shule ambayo iko hapa Mombasa ukiangalia ile hali yake utasikitika sana. Kwa nini iwe hivyo na rasilimali ziko hapa. Mtamu wa kutengeneza cement uko hapa Mombasa ama hakuna? Ulianza lini si ni kitambo sana? Sasa tukipata majimbo itakuwa rasilimali kama zile tunazitumia kwa sababu wale tunawafuata tunawaambia sisi tunataka cement, mitambo ya kutengeneza mabati iko, tunawaambia kuna shule kule inavunja leteni mabati. Watatupatia. Na sehemu nyingine pia endapo kama kuna rasilimali zao watazitumia hivyo hivyo.

Kwa hiyo sioni dawa nyingine. Lakini dawa katika hiyo Katiba  Serikali ambayo itakuja iwe hivo. Ndio dawa ipatikane ili watu wakisema watu wa Pwani wanalia lia labda kuna chuki aah. Haya kitu chengine mara ngapi tumepata ripoti either kwenye magazeti, tunasikiliza kwenye redio mambo mengine yanatutokea sisi wenyewe kwenye miili yetu tunayaona. Chuki za kikabila. Mara unasikia Molo sijui watu wamechomana. Mara sijui wapi.

Hii yote ni kwamba wakenya wote yaani kila mtu anachukulia ule ukabila lakini sisi watu wa Pwani ndio tunadanganywa hakuna ukabila, hakuna ukabila. Kwa hiyo ni kwamba ukabila upo na hauna dawa ila …….si mtu anataka kabila lake, haya apatiwe sehemu yake lile *jimbo*. Nchi ni hiyo hiyo moja lakini anapatiwa jimbo lake ili asije akatuua. Apatiwe sehemu yake na sisi tupatiwe sehemu yetu *jimbo*. Lakini Kenya ni hiyo hiyo moja sheria zitakuwa zinafuatwa. Hapo kutakuwa kuko na ubaya?

Faida nyingine ya *majimbo* ni kwamba leo labda Kenya imekatwa katwa *majimbo* manane, je hapo watashindana hawatashindana. Si watashindana? Kwa hiyo katika kule kushindana watu watapata faida. Kila mtu atataka awe juu kiuchumi. Wewe hautakubali jimbo lako kiuchumi liwe chini. Hautakubali katika ile hali ya *majimbo* kushindana, itapatikana maendeleo ya nchi nzima ambayo itatuletea faida sisi kama wakenya.

Kwa hivyo hizo ni faida ambazo ukisikia mtu akisema *majimbo* si kuwa ati anataka watu sijui wahamishwe, sijui watu wapigane. Hapana. Haya mambo ya kimajimbo ni mambo ambayo inaweza leta faida kubwa. Wewe kama hujafanya uchunguzi kwanzia leo ukifika nyumbani kama uko na rafiki zako ambao labda wanajua vizuri geographia na historia ya ulimwengu mzima. Uliza uliza lakini utapata nchi nyingi kabisa zile ambazo ziko na mifumo ya *majimbo* ndio ziko msitari wa mbele kimaendeleo.

Kwa sababu majimbo yanashindana na huwa hakuna chuki zozote. Maanake saa hii lazima chuki itokee mimi; babu yangu mimi yeye alipozaliwa alikuwa hakuna Kenya. Babangu pia alipozaliwa alikuwa hakuna Kenya. Sasa imekuwa ni ajabu mimi mjukuu nimezaliwa, naambiwa pale nilipo pia sio ardhi yetu ni ya Kenya.

**Com Prof. Wanjiku Kabira:** Bwana Juma tafadhali try to wind up. You have made the point tafadhali.

**Muhammed Juma Kizuri:** Thank you. Kwa hiyo mimi nikiambiwa kuwa labda pale sina ardhi nitashangaa kwa sababu babu yangu alizaliwa pale, baba yangu akazaliwa pale na hii Serikali ilikuja hawa wote walikuwa wamezaliwa. Kwa hiyo nafikiri kuondoa matatizo na kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Kenya nafikiri kitu ambacho kitasaidia kabisa ni kwamba tuwe na Serikali za majimbo. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Juma. Tutamuuliza Rehema Boru. Rehema ako? Hayuko. Yuko. Okey. Mwingine aendelee. Okey tutamuuliza John Rotich.

**John Rotich:** Mimi naona salamu zangu hazitasaidia kurekebisha Katiba mimi naenda tu moja kwa moja. Mimi ile ningependelea ni kwamba sauti ya Serikali peke yake ndio iwe inatisha. Kama sasa tuseme hii kuwa na silaha. Unapata kuna raia wana silaha ambapo sehemu zingine vita vinazidi na Mheshimiwa ambaye anaishi sehemu zile wakati au wavamizi wanaenda kuvamia sehemu ingine.

Serikali inatakikana ichukue hatua ya kwenda kunyang'anya wale watu silaha. Lakini unashtukia saa zingine wakati Serikali inatoa amri kuwa wale watu wenye silaha kinyume cha sheria waende wanyang'anywe. Unaona mjode anasema 'aah hiyo haiwezekani'. Na ndio sababu wenzetu bado wanaumia umia huko Marakwet, Turkana, Pokot, vita haviishi huko kwa sababu hao watu wenye tunawachagua hao ndio wanajaribu kutu……naona ni njia ya kutupunguza. Sawasawa. Kwa hivyo ile nilikuwa nataka kusema ni kuwa Serikali peke yake ndio iruhusiwe kuwa na silaha. Asante.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana. Bwana Rotich. Rehema uko tayari? Okey.

**Rehema Boru:** Salam Alaikum. Mimi sitasema mengi lakini nitasema machache niliyo nayo ambayo naona yatatufaa sisi wananchi wa Kenya. Kwanza kabisa kwa upande wangu nimeonelea kwamba siku hizi kuna ukabili mwingi sana kila mahali unapokwenda. Kwa hiyo kuondoa huno ukabila ni nchi yetu ipate maendeleo sawasawa bila kujali kabila kubwa wala ndogo lazima Serikali yetu itupe Serikali ya majimbo. Kila watu wawe na jimbo lao. Na tukisema hivyo ni kwamba sitakuwa ni majimbo ya vita mbali ni majimbo ya ushirikiano. Majimbo yote yatakuwa yakishirikiana pamoja. Wanaopata matatizo wanakutana wanasuluhisha. Tutawasaidia hawa kivipi? Na hawa tutasaidia kivipi?

Kwa upande mwingine ni kuhusu mambo ya usalama wa taifa. Yaani kama vile wanajeshi, askari polisi. Ningependa kuelezea kwamba kwa mfano kama hapa kwetu Pwani kuna watu wa tabaka mbali mbali Wajaluo, Wakikuyu, Wakisii, Wadigo na hali kadhalika. Lakini kama tunavyojua na wenyeji pia wako ambao ni wazaliwa wa hapa hapa Pwani.

Kwa hivyo wakati watu wanapochaguliwa ama Kizungu wanapokuwa recruited, lazima waangalie watu wazalendo wa pale. Sio kuwa mimi ni Mkikuyu na nimezaliwa Mtongwe basi nikienda kwenye recruitment, Mndigo aachwe achukuliwe Mkikuyu. Na ukienda kule kwa Wameru yule yule Mkikuyu amechaguliwa. Sisi watu wa Pwani tunakuwa under-mined. Pia wakati mwingine

sisi wasichana tunaposoma tukimaliza kidato cha form four tunapokwenda interview huwa hatufaulu. Ati wasikia 'huyu ni Mpwani'.

Kwa sababu ni Mjaluo lakini baba yake amezaliwa hapa, mamake amezaliwa hapa. Na sisi Wapwani tutakwenda wapi ikiwa hao ndio watu wakuchaguliwa. Ndio maana unaona siku hizi ukienda mahospitali, Wapwani hakuna. Ukienda mapolisi Wapwani ni kidogo. Kila mahali wametuzidi. Kwa hiyo wakati wa recruitment nataka wahakikishe kwamba kila mahali ni wazalendo wa sehemu ile wanaochaguliwa. Ikiwa ni Kisumu, wachaguliwe watu wa Kisumu. Ikiwa ni Pwani wachaguliwe watu wa Pwani. Ni Umasaaini watu wa Masaai. Sio Pwani tukiakangalia kwa watu ishirini katika hao ishirini wote watu wa bara.* Sisi wapwani ni watatu. Mambo kama hayo hatuyataki.

Jambo jingine ni kuhusiana na mambo ya elimu. Ningependa kwamba Serikali yetu ihakikishe kwamba imetoa elimu ya bure. Siku hizi tunasikia eti elimu ni ya bure lakini kwa hakika si ya bure. Mimi ni mwanamke maskini ama labda bwanangu amekufa na yu yatima. Nikiondoka kumpeleka mwanangu shule kwanza nitaambiwa nitoe admission fees. Hiyo admission fees mimi nitaipata wapi? Na ijapokuwa Serikali imesema elimu ni ya bure hawajaitilia maanani.

Lazima Serikali itilie maanani hizo vikwazo ndio sisi wananchi wanyonge tutafanyiwa mambo yetu. Lakini ikiwa watasema tu Serikali elimu ni ya bure na ukifika hiyo bure hauipati. Itakuwaje? Kwa hiyo Serikali lazima ihakikishe inalosema linatenda kwa vitendo. Sio kusema bure na ukifika basi unaanza kufukuzwa. Mpaka uje na pesa.

Jambo jingine ni kuhusu sisi akina mama wanawake. Sisi wanawake twanyanyaswa sana na sisi ndio watu wengi hapa Kenya kuliko wenzetu wanaume. Kwa hiyo ningeomba Serikali itutengee sisi wanawake viti vyetu special. Ikiwa kule Bunge kunatakikana asilimia mia moja, basi asilimia thelathini ya zile viti za Bunge lazima tuwe na representative ambao ni wanawake.

Jambo la pili ni kuhusu sisi wanawake. Katika dini yetu ya kiislamu mtu anaruhusiwa kuoa bibi wawili, watatu mpaka wa nne. Kwa hiyo wakati wa uridhi ni lazima kila bibi agawanyiwe uridhi wake. Si kwamba aah huyu ndiye bibi mkubwa basi atapata kila kitu. Mambo kama yale yawe hayako. Kila mtu apate haki yake vile inavyohitajika.

Jambo jingine ni kwamba punde mtu akiwa amefiliwa na mumewe, kuwe na rights za kuwa huyu amefiwa na mumewe na hii ni haki yake. Kusiwe na yale mambo yetu ya kuwa 'ooh huyu aondoke aende kwao'. Sijui hivi na hivi. Serikali ituekee law ambayo itakuwa inatupa sisi uwezo wa kuridhi mali za wanaume wetu punde wanapokufa.

Jambo jingine ambalo nilikuwa nataka kusema ni kuhusu uongozi yaani kama vile Rais. Katika Katiba ya Kenya inasema ya kuwa Rais ni above the law. Kitu kama hichi mimi nakipinga binafsi. Hakuna mtu aliye above the law. Rais ni mwanakenya na sisi sote ni wanakenya. Kwa hiyo hakuna mtu anaweza kusema mimi niko above the law. Yeye pia ana haki ya kuwa amefanya makosa na yeye ahukumiwe kama wananchi wengine. Sio kusema above the law.

Jambo jingine ni kuhusu ya ino citizenship. Kuna watu ambao huwa si wakenya mfano; Wazungu, Waarabu na nini na nini. Mtu atakuja hapa Kenya kimagendo. Akija kimagendo ataishi ataishi huku achunguza tu mambo ya pale Kenya halafu baadaye atasema ati yu ataka kununua citizenship maanake asha kaa Kenya miaka saba. Baadaye watu kama hao hao ndio huwa wanakuja wanakuwa ni wale majambazi. Kwa hiyo mambo kama hayo lazima yachunguzwe.

Jambo jingine ambalo nataka kusema ni kuhusu mambo ya ardhi yetu. Mimi ni mtoto sana kiumri lakini kwa wale wazazi wangu walio wakubwa na mababu zangu waliotangulia, sisi watu wa Pwani twanyanyaswa sana na ardhi yetu. Kila mahali unapokwenda unaambiwa kuwa sisi ni ma-squatter.

Na jambo la kushangaza mimi mwenyewe ni mzaliwa Mtongwe lakini naishi Shikadabu. Lakini kule Mtongwe kila nikiuliza mzee mwenye title deed unaweza ona ardhi ni ya nani? Wambui na Mhindi na huyo Mhindi anayo title deed. Itakuwaje Mhindi awe na title deed na sisi wenyewe wazaliwa hatuna hizo title deeds. Kwa hiyo jambo kama hilo lazima lichunguzwe.

Pia kuna jambo lingine ambalo nilipata fununu kutoka kwa babu yangu aliyekufa kitambo ati  hicho kipindi cha nyuma kilichopita kulitokea amri kuwa Mtongwe ipigwe bomu kwa sababu Mzungu mmoja aliuawa. Basi katika kule kulia kulia kuliambiwa kuwa ile sehemu yote ya ufuko wa Pwani uchukuliwe na family ya waarabu. Alipewa huyo Sultani aliyekuwako hapo akaambiwa basi hii sehemu yote itakuwa ni yako. Mambo kama yale lazima yachunguzwe na sisi Wadigo tupewe haki zetu.

**Clapping from the audience.**

Jambo jingine ambalo nilikuwa nataka kusema ni kuhusu mambo ya health. Watu lazima wapewe haki zao katika mambo ya matibabu siku hizi ukienda hospitali hata kama una mtoto ni mndogo ukifika kule waambiwa kwanza mpaka unipe shilingi ishirini ndio huyu mtoto aandikiwe kadi. Sasa wewe huna hata hizo shilingi ishirini ndio imaanisha kuwa yule mtoto wako hatapata matibabu. Shilingi ishirini ndiyo yamaanisha ya kuwa yule mtoto wako hatapata matibabu kabisa.

Kwanza Serikali lazima ipasishe kuwa kuna kiwango cha mtoto akiwa kwanzia mwaka mmoja mpaka kama miaka kumi na nane awe atapata matibabu ya bure kwa sababu kuna wengine huwa hawana uwezo na sisi tushaona sasa wakati waenda hospitali waambiwa wewe hutibiwi mpaka pesa. Kwa hiyo Serikali ihakikishe kwamba imetupa madawa ya bure.

Jambo jengine ni kwamba kuna hizi rasilimali kama vile kule mbugani ambapo huwa watalii wanaenda ama kama hizi bahari zetu za huku Pwani. Utaona kama kwa kule wenzetu wa bara* sehemu nyingi kama vile mbugani watalii wanapokwenda kuna kiasi fulani cha pesa ambacho huchukuliwa kuwafaidi wale wananchi wa ile area.

Lakini hapa kwetu Pwani mambo kama hayo hayako. Kwa hiyo na sisi twataka kile kiwango kinachopatikana kutokana na zile

bahari zetu na sisi wananchi tupewe percentage fulani. Interest ambayo inapatikana pale, tupewe sisi wananchi ili iweze kutufaidisha sisi wenyewe. Maana ikiwa ukienda kama kule sehemu zile utakuta wengi si wazaliwa wa Pwani na wanaajiliwa makazi. Lakini ile percentage lazima itoke. Ili imini kuendeleza ile ile area ya pale. Kutokana na nini? Na zile bahari.

Jambo jingine ambalo nilikuwa nataka kusema ni kuhusu Serikali zetu za wilaya. Serikali zetu za wilaya lazima ziwe huru kujisimamia zenyewe binafsi. Sio kuwa hapa ni shirika la Municipaa ya Mombasa lakini pesa zinazokusanywa zipelekwe Nairobi. Halafu watu wa Nairobi wakae chini waseme hichi kiwango fulani sasa ndio kitapelekwa Mombasa kiende kikawasaidie watu wa Mombasa. Mambo kama haya tungependa yarekebishwe. Kila baraza ya wilaya kama ni municipaa ni wapi ni wapi, iwe itajisimamia kivyake. Ikisha fanya mambo yake, ikisha collect zile pesa wenyewe wakae chini wajue tutafanya vipi ili wilaya yetu iweze kuendelea. Sina mengi ni hayo.

**Clapping from the audience.**

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bi. Rehema. Utajiandikisha tafadhali. Tafadhali jiandikishe. Okey asante sana. Na sasa tunamuuliza Mwinyi Juma. Okey. Na huyo mwingine ni Abdallah Okey. Ameenda. Na mwingine ni Hassan Juma. Kizuri Juma. Omar Tenga. Yuko.

**Omar Tenga:** Asante sana Bi. Commissioner na wananchi wenzangu. Yangu si mengi sana, ni machache na maoni haya ni yangu binafsi. Jina langu Omar Tenga na ningependa kuanza kwa kusema kwamba ningependelea na ni maoni yangu kwamba Serikali ya Kenya iwe ya mfumo wa majimbo. Na ningeuliza pia majimbo hayo yawe majimbo sita katika hii Kenya yetu. Tuache mambo yale yetu ya administration provision. Ile hatutaki hayo.

Tunataka majimbo yawe sita. Wale ambao watatengeneza wafikirie hivyo. Na majimbo haya ningependelea ya kwamba yaweze kusimamia rasilimali zake na uchumi wake bila kuingiliwa na Serikali kuu. Katika mfumo huo ningependelea kuwe na Serikali kuu. Na Serikali kuu hii isimamiwe na Rais lakini huyu Rais pia apawe uwezo wa kuchagua wizara na wizara zenyewe ziwe kumi na mbili peke yake katika Serikali yetu ya Kenya.

Hivi sasa kuna mpango wa kwamba Rais akifikiria tu kutengeneza wizara, yu aenda tu asema hii wizara itakuwa wizara fulani. Zinaenda mpaka zinakuwa karibu ishirini na tatu. Nyingine sijui kumi na sita. Mtindo huo sio mzuri na Katiba yetu kama ingetoa fursa ya kwamba wizara ziwe kumi na mbili peke yake itakuwa vizuri sana. Na sasa wizara hizo pia ni pendekezo langu kusema kwamba waziri hawa watoke wawili, wawili kutoka kila jimbo ili watengenezewe zile wizara kumi na mbili.

Tukifanya hivyo itakuwa tumepata nafasi ya kila mtu kuwa katika Serikali hiyo kuu. Mtu kutoka kila jimbo. Na pia mawaziri hawa wapawe nafasi wao pia. Yaani katika majimbo kuwe na hao mawaziri wandogo. Kama wizara ni kumi na mbili basi mawaziri wandogo watoke katika jimbo kuwe na mawaziri wandogo kumi na wawili na itakuwa ni jukumu la jimbo wenyewe

kuchagua hao mawaziri wandogo kumi na wawili. Hayo ni maoni yangu.

Naendelea kwamba hapo kuna jambo ningependa kusisitiza ya kwamba Katiba ya Kenya ile ambayo tunasema iwe ya majimbo. Pia kwa sababu ya uhuru wa wananchi, wananchi wapewe uwezo wa kujichagulia jinsi watakavyoendesha lile jimbo lao na ikiwa inafika wakati ya kwamba jimbo linataka kujitenga, wananchi wapewe uwezo wa kufanya hivyo.

Nachukua mfano wa wenzetu kule Zanzibar, wakati fulani kulikuwa kuna wakati ambapo hawa watu walikuwa wanataka kujitoa kutoka jamhuri ya Tanzania lakini wakaambiwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu Katiba yao haisemi hivyo. Walikuwa wanataka waende pengine kujiunga na Serikali nyingine mahali fulani. Hakuweza kufanya hivyo.

Kwa hiyo ningependelea katika Katiba yetu, jimbo lipawe uwezo wa kutafuta mahali ambapo linaweza ku-join. Mfano; kama jimbo la Pwani linataka kuungana na jimbo la North Eastern basi kuwe na uwezo huo wa kufanya. Au kama jimbo la North Eastern linataka kuungana na Serikali ya Somalia, hii ni shauri yao.

Hii ni kwa sababu ya kusema kwamba huo ni uhuru mkubwa sana wa mwananchi ambaye anahitajika. Ingawaje katika hayo yote ningesisitiza ya kwamba kama jimbo linataka kufanya kitendo kama hicho lazima 90% ya wale watu ambao wako katika jimbo hilo wapige kura wakubaliane kwamba wanataka kufanya jambo hilo. Si watu 25% au 30% au 40% kusema hivo tu halafu watu waende. Hapana. Lazima 90% wapate nafasi kama hiyo ya kuzungumza na kupiga kura.

Kitu chengine pointi yangu ya tatu ningependa kusema kwamba hivi sasa katika Kenya mtu ambaye anaweza kuwakilisha kesi mahakamani. Ni kama Attorney General, hawa ma-state council, hawa akina public prosecutors so on and so forth. Mimi ningeomba kama Katiba yetu inaweza kuonyesha kwamba mwananchi wa kawaida pia naye apate nafasi ya kupeleka kesi mahakamani hasa kwa upande wa criminal cases.

Hivi sasa mwananchi wa kawaida anaweza kupeleka mambo ya civil cases katika mahakama lakini upande wa criminal ni lazima upitie through police ili ukaandike statement huko halafu prosecutor aje achukue kesi yako wapi? Kortini. Ningependa Katiba yetu itoe fursa ya kwamba mwananchi wa kawaida anaweza kumchukua mtu kortini moja kwa moja.

Jambo hili litasaidia sana kuvunja corruption. Kama mimi Omar Tenga ninafanya mambo ya corruption na wewe umeligundua hakuna haja wewe upate maneno ati 'nenda polisi kwanza ukapige report au uandike statement huko. Hapana. Wewe chukua lawyer wako, mashahidi wako watatu peleka kesi kortini. Moja kwa moja corruption intapungua kwa sababu sisi wenyewe tutakuwa tunajilinda kwamba wewe unamwangalia huyu na huyu anamwangalia yule.

Na mfano mmoja mzuri mdogo sana vitu kama hizi trade licences za watu wa kawaida hapa. Kuna maduka ambayo hayana licence na tunajua licence ndio uchumi wa nchi yetu. Lakini huyu mtu ambaye hana licence wewe na mimi na mwingine tunajua

huyu hana licence lakini hatuna uwezo wowote wa kumfanya. Maana ni lazima polisi aje au mtu wa manicipaa aje amwambie ‘ wewe huna licence’.

Na jamaa akijua huyu ni mtu wa manicipaa hana licence baas, hapo umefungua ufisadi maana mwenye duka anapeana pesa kwa mtu wa manicipaa, mambo imekwisha. Licence hana na pesa imeenda na bado mambo yana…..lakini kama leo huyu Odhiambo anaweza kuona lile duka halina licence, halafu Salim pale ajue pia hilo duka halina licence. Hao watu wanaweza kushikana na mara moja watakuwa wanaondoa ufisadi katika nchi yetu.

Pia katika utumishi wa umma: Kuna watu wengi sana katika utumishi wa umma ambao hawa watu ni wazembe kabisa. Uzembe wao ni kwamba; anaweza kuwa yeye ni veterinary officer au agriculture officer lakini kazi yake hafanyi hata kidogo. Watu kama hawa ndio tungependa Constitution yetu itupe uwezo wa kuwachukulia hatua kwamba wewe so and so unahitajika kufanya kazi fulani lakini wewe hiyo kazi hufanyi. Kwa hiyo sisi wanakijiji tunakupeleka mahakamani ukajibu kwa nini hufanyi kazi hiyo.

Halafu mfano; mtu kama mzee wa mtaa au chief. Wale watu ambao wamezoea tu kushika kuku za wenyewe hapa na pale. Mimi nikiona wewe ni chief unakuja kushika kuku wangu hakuna haja ya mimi niende moja kwa moja mpaka polisi nikapige ripoti eti chifu amenionea. Hapana. Ni sisi watu wanne watano tuende moja kwa moja mahakamani tukashitaki na kesi yetu isikilizwe.

Kwa upande wa elimu pia ni maoni yangu kwamba elimu katika Kenya iwe ya bure. Na elimu ya bure ianzie elimu ya msingi, elimu ya upili hata elimu ya chuo kikuu. Na ikiwezekana pia vyuo vyote vya ufundi pia viongezwe katika mzululu huu wa elimu ya bure. Tukisema elimu ya bure tuna maana ya kwamba mtu yule asiojiweza na yule mtu ambaye anajiweza wote wawe katika hali moja ili elimu hii isambaze kila pahali. Ingawaje elimu kama hiyo isisitizwe kwa upande wa majimbo maana majimbo yenyewe watakuwa wanasimamia rasilimali yao na uchumi wao. Kwa hiyo kila jimbo liangalie mambo kama hayo.

Hayo ni mapendekezo yangu na nikiendelea kidogo ni ule umilikaji wa rasilimali hasa rasilimali kama ardhi. Pendekezo langu ninasema ya kwamba huyu mwananchi wa kawaida ashilikishwe wakati wowote katika hii mambo ya ardhi. Mwananchi apawe uwezo wa kushiriki au ashirikishwe kwa rasilimali yeyote itakayopatikana chini ya ardhi yake anayoimiliki kisheria. Hapa nina maana ya kwamba hivi sasa sheria zetu zinasema mwananchi anaruhusiwa kumiliki futi sita tu ya chini ya ardhi.

Lakini huko kwingine kwote kutoka hapo mpaka huko kuziimu hana haja ya kukumiliki. Mimi maoni yangu nasema ya kwamba mwananchi huyu apawe fursa ya kumiliki hiyo nchi yote moja kwa moja mpaka chini. Nina maana ya kwamba in case katika ardhi yake, shamba lake kumepatikana madini bahati nzuri nini yako imepatikana dhahabu. Bahati nzuri mafuta, bahati nzuri diamond. Imepatikana katika ardhi yako.

Kwa mfano kule kwetu kwa upande wa angazi kule kumepatikana titanium. Hao watu hawa kama hiyo madini yako chini sana

ambapo wewe mtu wa kawaida huwezi kuyafikia. Basi Serikali au company lazima ikushilikishe ya kwamba wewe ni milikaji wa hiyo kitu. Hivi sasa kuna yale mambo ya kufanyake? Kumepatikana kitu hapo halafu wanakuja wanakupa ridhaa. Wanakwambia 'eeh hapa sijui kuna nini kuna nini', unapewa ridhaa shilingi zako elfu mbili, haya toka. Wao wanakuja kufanya mining. Hilo ni jambo moja mbaya sana.

Kama mining hiyo itafanywa wewe pia uwe hapo hapo na kama ni faida itapatikana ili pia nawe mwananchi wa kawaida upate faida hiyo. Pia ingawaje nimesema mambo ya majimbo hapa kuna pointi kidogo ambayo nilikuwa nimewacha kando na ninasema ya kwamba kuwe na Bunge katika kila jimbo na jimbo lichague wakuu wa sheria na mahakama kwa kila jimbo.

Yaani nasema kama jimbo liko, jimbo hilo lipewe fursa ya kuchagua commissioner wake wa polisi, lichague mkuu wake yaani Chief Justice na pia kama ikiwezekana achaguliwe Attorney General katika jimbo hilo. Hiyo ni ya nini na kama huko juu katika Serikali kuu kutachaguliwa mwingine awe chifu wa chifu wote haya sawasawa. Lakini kwa jimbo kuwe na nafasi kama hiyo.

Mwisho ningesema katika Katiba yetu ya sasa kuna ule uwezo wa Rais kusamehe wafungwa. Yaani kwa Kizungu ni prorogative of mercy. Uwezo huo ningependelea au ningependekeza ya kwamba utolewe kabisa kutoka kwa Rais. Rais asiweze kabisa kusamehe mfungwa yeyote. Hapa kuna maana ya kwamba ikiwa mtu mfisadi ni rafiki wa Rais, mnaweza tu mtu huyo kupelekwa hapa jela mnasikia tu 'ooh amefungwa jela miaka mingapi?' Miaka tano. Halafu wakienda kule wanakaa wenyewe huko kando wanasema 'si Rais anaweza kusamehe mtu'. Inachukuliwa karatasi inawekwa sign na Rais mara moja unapewa huyo mtu.

Na wewe hapa hutaambiwa utakuja tu kusikia katika mikutano leo kuna wafungwa mia tatu au elfu kumi, wamefunguli? Wamefunguliwa. Kumbe katika wafungwa hawa mmoja alikuwa yule sugu kabisa mfisadi ambaye pengine alikuwa nini? Ni rafiki wa Rais. Hiyo ni moja ambayo ningependelea Katiba yetu itoe kabisa hiyo kifungu katika nini…..na isimpe Rais mamlaka hayo. Nafikiri Bwana Commissioner mpaka hapo nimemaliza maoni yangu. Asante sana.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Omar lakini kabla hujaenda ningetaka kukuuliza kama waweza kutambua kidogo juu ya zile jimbo sita. Ulisema unataka jimbo sita?

**Omar Tenga:** Nimesema ninataka majimbo sita. Hivi sasa tunajua zile provinces ni nane lakini sasa hizi sita nimesema sitazitaja ni gani au ni gani. Lakini kwa fikira nilikuwa na mfano wa North Eastern pamoja na Coast. Hizi zikiunganishwe pamoja zifanywe jimbo moja. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu ya mambo ya kidini. Watu wa Norht Eastern pamoja na watu wa Coast Province wengi sana ni waislamu. Na watu kama hawa kama wanaweza kuwekwa pamoja wanaweza kunini. Kwa hiyo unaona katika zile saba tayari moja nimeunganisha na nyingine zinakuwa sita tayari.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Hujaunganisha ingine?

**Omar Tenga:** Bado sijaunganisha ingine. Ni hiyo tu.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Omar. Si utaandika majina na utatupatia hiyo note?

**Omar Tenga:** Yes.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey. Asante sana.

**Com. Zein Abubakar:** Halima Kavanga?

**Halima Kavanga:** Salam Alaikum. Mimi jina langu ni Halima Ali Kavanga kutoka Ndimbwini. Chairlady wa Umoja ni maendeleo. Nasimamia kikundi cha watu ishirini. Waniambia nije niwakilishe. Kuwakilisha ni hivi: Wao wataka Serikali ya majimbo. Kwa sababu kuwa wataka Serikali ya majimbo, basi kwa kunyanyaswa na Serikali ya umoja. Serikali ya umoja tuliichagua kitambo lakini hakuna kitu ambacho ki…..siwezi kusema mahali kwingine nasema Likoni. Likoni ndio hatuna maendeleo yeyote. Hasa sehemu ambayo niko mimi tuna matatizo. Hata ukiwa mgonjwa pia hatuna hospitali mpaka tubebane na mikokoteni tupelekana hospitali. Kwa hivyo sasa sisi twataka majimbo kwa maana tukipata majimbo ndio tuta…pengine tutajisaidia wenyewe watu wa Pwani.

**Com. Zein Abubakar:** Wewe ukiendelea hivyo sasa hivi tutakuchukulia hatua wewe. Tutakuchukulia hatua wewe. Endelea mama.

**Halima Kavanga:** Sisi twataka majimbo kwa sababu hiyo kwa maana watu wa Pwani kutoka tulipopata uhuru, hatujatambulikana kama tu wakenya. Kwa hivyo twataka majimbo. Mimi sina mengi yangu ni hayo kuwa sisi twataka Serikali ya majimbo kwa sababu hatutaki majimbo ya vita. Twataka majimbo ya amani. Watu watembeleane kila pahali pote. Rasilimali zetu za Pwani tuwe tunazo si wenyewe watu wa Pwani. Yangu ni hayo.

**Com. Zein Abubakar:** Asante mama. Ignatius Gikware. Swale Hamisi. Abdullah Liseso. Daniel Omondi.

**Daniel Omondi:** Asante Bwana Commissioner Abubakar na wananchi wenzangu hamjambo. Kwa majina naitwa Daniel Omondi nawakilisha 'Wazo self-help group' kutoka Likoni. Yafuatayo ndio mapendekezo ya kikundi cha Wazo. Pendekezo la kwanza ni kuhusu elimu. Katika Katiba ya Kenya, Katiba itakayokuja tunapendekeza elimu ya msingi iwe ni ya bure katika shule za umma. Kwa sababu gani? Tumeona saa hii wazazi wengi wanakumbwa na matatizo kwa upande wa umaskini. Ikiwa elimu itakuwa ya bure wazazi wengi watapata nafasi ya kupeleka watoto wao shule na nchi itakuwa na viongozi bora.

Pili, utawala wa mikoa: Tumependekeza kuwa utawala wa mikoa uchaguliwe na raia kwa kura kwanzia kwa chifu hadi kwa PC. Kwa nini? Kwa sababu wakichaguliwa na raia, watawatumikia kwa njia ipasavyo.

Tatu, upande wa Chief Kadhi: Katika kikundi chetu ni mchanganyiko tuna waislamu na wakristu. Tumependekeza kuwa Chief Kadhi awe akichaguliwa na baraza la waislamu na pia Chief Kadhi huyo apewe uwezo kutatua kesi hadi kiwango cha korti kuu au korti ya rufani.

Kuhusu upande wa vikundi yaani self-help groups. Tunapendekeza katika Katiba itakayokuja, iseme kuwa vikundi vya wananchi yaani self-help groups zihusishwe katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mfano ikiwa manicipaa wamekuja na mradi wao na wanataka kuanzisha katika kile kijiji, itawapasa watafute kikundi gani ambacho kiko karibu pale. Wawahusishe. Kwa sababu wale wenye kijiji ndio wanajua matatizo ya pale kwao.
Tumependekeza kuwa Mayor awe akichaguliwa na wananchi kwa kura na awe akitumikia kwa kipande cha miaka mitano kama vile wabunge ili uchaguzi ukifika wachaguliwe pamoja na wabunge.

Na tatu tumependekeza kuwa kipindi cha kutawala kwa upande wa Rais, iwe ni awamu mbili yaani awamu mbili za miaka mitano mitano. Mtu akipitisha hapo asiongezewe muda hata kama alikuwa ni mzuri vipi.

Katika upande wa uteuzi, Katiba ya Kenya inampatia Rais mamlaka ya kufanya uteuzi. Sisi tunapendekeza kuwa Katiba itakayokuja Rais asihusike katika uteuzi wa wakuu wa mashirika. Kwa upande wa Mkuu wa Sheria tunaona kuwa Rais huwa ndiye mwenye kumteua Mkuu wa Sheria tunapendekeza kuwa Katiba itakayokuja Mkuu wa Sheria awe akichaguliwa na kamati ya ma-judge na kuidhinishwa na Bunge. Tukifanya hivyo itakuwa ni kama upande wa Serikali kumetokea makosa fulani. Itakuwa ni vigumu mkuu yule wa sheria kufanya upendeleo kwa sababu amechaguliwa.

Tunapendekeza kuwa katika Katiba itakayokuja, mwananchi wa kawaida asisumbuliwe kwa uwekaji wa rasilimali. Iwapo atasumbuliwa apewe ridhaa. Kwa mfano; kuna baadhi ya ndugu zetu wasiojiweza, walivunjiwa vibanda vyao. Na mpaka saa hii hawajapata ridhaa yeyote kutoka kwa Serikali. Kwa hivyo tunapendekeza ikiwa mtu yeyote kama huyo atakumbwa na matatizo kama hayo, Serikali impe ridhaa. Na kufikia hapo nimewasilisha memorandum hii kwa Tume ya urekebishaji wa Katiba na ni matumaini yangu kwamba mtatekeleza majukumu ambayo yako mbele yenu kuhakikisha kuwa maoni ya wananchi yametekelezwa ipasavyo. Asante sana.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Daniel. Aggres Sindani. Joseph Gitonga. Juma Shabi. Nani mwenzangu? Okey. Joseph Gitonga.

**Joseph Gitonga:** Okey nashukuru sana nazungumzia hasa kwa upande wa dini nikiwa nawakilisha katika upande wa Seventh Day Adventist church.

**Com. Zein Abubakar:** Ndugu taja jina lako kwa sababu ya ku-record.

**Joseph Gitonga:** Jina ni Joseph Gitonga. Sehemu ya kwanza najaribu kuweka mkazo hasa kwa mzungumzaji wa kwetu wa kwanza ambaye alikuwa ameanza hapa alikuwa ni Kadhi ambaye amezungumzia juu ya vitabu. Katiba iweze kutambua hasa vitabu vya Mwenyezi Mungu kama vile Koran na Biblia takatifu viwe vimewekewa kipa umbele.

Halafu katika upande mwingine ambao waliozungumzia naweka mkazo ni ule ubaguzi wa dini. Waona ya kwamba wengine waweza kutendewa hivi na wengine pia hawawezi kutendewa. Halafu kitu kingine ambao naweza kuwekea mkazo waliozungumza ni upande wa kuapishwa kama pale vile kortini, may be unainua kama Biblia. Na Biblia yenyewe inakataa. Sijajua sana kwa undani kwa kitabu cha ukorani lakini hasa najua Biblia inakataa mambo ya kuapa. Kwa hivyo vitu kama hivyo viweze kuondolewa katika Katiba inayokuja.

Halafu kitu kingine katika sehemu ninayotia mkazo ni upande wa unyanyasaji wa watu wengine wa dini, kama vile kutokuwa na nafasi bora ya kuweza kuwa na nafasi ya kuabudu. Kwa mfano nikijaribu kumnukuu kijana mmoja ambaye aliyekuwa amefanya mitihani yake, alisoma miaka miwili pale Shanzu. Baadaye kufikia mwisho wa mtihani ikafanywa siku ya jumamosi na alikuwa lazima aweze kuenda kwa ibada lakini akatupiliwa mbali baada ya kutumika miaka miwili kwa sababu hawezi kufanya mtihani siku hiyo ameenda kumuabudu Mungu. Kwa hivyo vitu kama hivyo viweze kuangaliwa sana.

Hata pia nimekumbuka juzi kulipokuwa na kura sehemu zingine hizi za northern, utapata kuona ya kwamba uchaguzi uliweza kufanywa siku ya jumamosi ambapo watu wengine wakanyimwa haki zao kwa sababu hangeweza kwenda kupiga kura na walikuwa wanaenda kwa ibada. Kwa hivyo hata tukiangalia vitabu vya Mwenyezi Mungu, tuangalie tuone ya kwamba kama vile Biblia inakazia ibada ya siku ya jumamosi na ikitaja ya kwamba inaanza kutoka ijumaa jioni hadi jumamosi jioni. Kwa hivyo Katiba iweze kuiweka wazi iwe inaweza kueleweka.

Kitu kingine ambacho naweza kuzungumzia sasa katika Katiba iweze kuhusika, nazungumzia upande wa elimu. Tabia imeweza kuharibika sana katika ulimwengu mzima hasa hapa kwetu Kenya na sababu mojawapo ni elimu imerundikana kwa watoto. Kwa hivyo hata watoto wanapokuja shuleni hawana nafasi ya kufundishwa maana wana huu mwaka kwa hivyo hakuna nafasi ya kuwapa elimu ya kimisingi ambayo ni ya kawaida. Kwa hivyo elimu hii iweze kupunguzwa ili watoto wetu waweze kuwa na nafasi hasa ya kupata misingi ya kidini na misingi ya kitabia za kiasili.

Kitu kingine ambacho ningependa kiweze kukumbukwa katika Katiba yetu ni Seventh Day Adventist church iweze kuwa iko kivyake kama vile Catholic church, Protestants na pia Islamic. Kwa hivyo Seventh Day Adventist si kwamba si mojawapo wa protestants, bali wako kivyake Seventh Day Adventist Church.

Kwa hivyo Katiba inayokuja ikaweze kuiangalia kivyake na kunapokuwa na jambo linalotaka kutuzurura kidini, hata hiyo ikaweze kuhusishwa kama Seventh Day Adventist Church. Kitu ingine ambacho naomba tuweze kuangalia kwa Katiba ni kama vile uvutaji wa sigara. Uvutaji wa sigara umekuwa ni jambo janga kali sana hata mataifa mengine wamejaribu kuwaondoa katika mataifa yao. Lakini utapata kuona ya kwamba uvutaji umekuwa ni kwazo hata kwa mikutano, kwa watu ambao wamekusanyika.

Watu wengine ambao hawataki zile harufu zile zinaanza kuvutwa katikati kwa hivyo inakuwa ni kuhatarisha hata kiafya, hata furaha yao inakuwa inaondolewa. Kwa hivyo Katiba iweze kuangalia jinsi ya kushughulikia kifaa hiki sigara na madawa mengine ya kulevya. Halafu kitu ingine ambacho ningependa Katiba yetu iweze kuangalia ni kama vile magazeti ambayo yaliweza kuvurutana na mmoja wetu hapa. Ambao ndio inachuzia zaidi kuweko na usherati katika Kenya hii yetu. Kwa hivyo yanatandikwa yanaonyeshwa huu utupu wa akina mama. Hata ni kuwakosea akina mama adabu. Kwa hivyo naomba ya kwamba magazeti haya yaweze kuwa ni marufuku katika Katiba yetu ya Kenya.

Halafu pamoja na hiyo mavazi. Hapo nitaweza ….ni mkristu lakini naweza kuongea sana waislamu kwa sababu ya nidhamu na mavazi. Kwa sababu wanawake hata mwanamke akipita inaonekana nidhamu. Hata akitaka kuinama anaweza kuinama tu. Lakini wako ndani ya wakristu na wengine ambao si wakristu wameleta desturi ambayo ni mbaya ambayo inaaibisha. Kwa akina mama hata akiinama hivi hawezi kuinama mpaka achuchumae. Nguo zingine ambao zinakatwa ambao zinatoa aibu. Kwa hivyo Katiba yetu iweze kuangalia hata upande wa mavazi kwa upande wa watu wetu. Unaona ya kwamba may be tabia hizi zimeletwa na kizungu tumeona ya kwamba wasichana wetu wanatoa tabia kama hizo ambazo sizakupendeza. Kwa hivyo Katiba iweze kuangalia na kushughulikia vilivyo upande wa mavazi kwa watu wetu.

Kitu kingine ambacho ningeweza kuomba Katiba iweze kukiangalia ni upande wa polisi. Polisi wamekuwa kazi yao tu ni hongo. Kwa hivyo hata ukifanya kosa gani, magari yanatembea bila licence lakini wakitoa mia anapita. Kwa hivyo Katiba iweze kushughulikia hasa hawa mapolisi wanaokaa njiani na kuangushiwa mia, mia. Kupangwe jinsi ya kuweza kupata watu hawa ili ya kwamba kufanya usawa katika barabarani.

Kitu kingine ambao ni cha mwisho ni upande wa miziki. Miziki inakuwa ni kama imeanza kushida Serikali kwa sababu ukienda kwa matatu saa ingine mtu amechoka miziki imewekwa kwa hali ya juu, inaripua inaripua hata inakuwa huna amani. Kwa hivyo kitu hiki kizingatiwe na kuwe katika magari yanayotembea yanayobeba abiria watu wakitaka miziki wanasikia katika manyumba yao lakini si ndani ya magari. Kwa hivyo hivi mtu anapotembea hata kama anaongea na mwenzake anapowaambia 'nishukishe' mtu anapitishwa na gari kwa sababu unaambia manamba asimame na anasikiza habari ya miziki. Kwa hivyo jambo hili naomba pia liweze kushughulikiwa katika Katiba yetu. Kwa hivyo nashukuru sana macommissioner ambao wameweza kushughulika na Mungu aweze kuwabariki mnao shughulikia jambo hilo.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Bwana Gitonga. Tafadhali sign register hapo. Bwana Juma Shambi. Hamisi Mwanga.

Karibu bwana.

**Hamisi Mwanga:** Mabibi na mabwana Salam Alaikum. Ama kwa hakika mimi nimesimama mbele yenu kama mwalimu na pia ni mzee wa mtaa katika Migombani village. Ama kwa hakika sisi tuna masikitiko mengi sana.

Mzee wangu taja jina ndio tu-record jina lako. Mimi ni Hamisi Muhammed Mwanga kutoka Migombani ama kwa hakika raia wana masikitiko mengi sana katika hii sehemu ya Likoni. Ama hakika hii sehemu ya Likoni imegeuzwa njaa. Kila mwenye machafu yake anasukumiza Likoni na sisi watu wa Likoni tumevumilia sana. Na tumevumilia hali ya juu kabisa na masikitiko mengi. Kila upande, kwanza tufika upande wa elimu. Masikitiko ya elimu. Utafika watoto waliofanya mitihani karibu watoto wote tukija orodha zetu ya mitihani katika sehemu ya Likoni, unaona watoto wako chini.

Na pia tuna masikitiko sana Serikali yetu, kila jambo inatusahau katika sisi. Nafikiri jambo moja ama kuna wafadhili ambao wanatoka sehemu mbalimbali. Kuna wenzetu ambao ni wa sehemu za nyuma, sehemu Kilifi, Kaloleni juu ya wafadhili wamefaidika vizuri sana. Lakini huku ukija upande wa Likoni wafadhili wa Likoni wametupwa. Hawakusaidiwa kitu chochote mbali walifanywa kama sanamu tu. Kwenda kupiga gwaride haya mpeleke kwao basi.

Hii kitu inasikitisha sana. Ama kwa hakika hili jambo sisi watu wa Likoni tulifanya nini? Kila kitu kwa wenzetu kinakuwa safi sana. Nilitembea upande wa Kaloleni (inaudible) wafadhili wa akina mama wa vikundi, wazee wa mtaa, wa kibalu balu watu walifaidika vizuri sana. Lakini jambo likishafika Likoni linakuwa sasa hilo jambo linasahauliwa kabisa watu wazee hawana maana watu wa Likoni.

Kwa hivyo ningeomba watu wa Katiba ili wazingatie……Serikali izingatie maneno hayo na pia tunakuja tena sasa ama kwa hakika mimi nataka kuwafahamisha watu wa Likoni sasa waamke. Hivi sasa kumekuja siasa wakati wa siasa wa kuchagua watu sasa tunaletewa maneno mengi kabisa. Tunavurugwasishwa kila upande, kila nini kila mtu anasahauliwa ili kuchafuliwa akili zetu. Lakini mpaka dakika hii watu wa Likoni muwe macho. Mchague yule mtu ambaye mnamtaka mmpeleke wa kisawasawa ambaye hafai atupwe nje.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee wangu.

**Hamisi Mwanga:** Naam. Kwa hivyo mimi sina mengi nimefikia hapo asante sana.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Mzee wangu. Tafadhali andika jina lako kwenye register. Ashatoboa yamekwisha. Sasa namuomba Mzee Mwinyi Zula. Kumbe ni wewe.

**Mwinyi Zula:** Asante sana Bwana Commissioner, mabibi na mabwana Salam Alaikum. Hapa jina langu naitwa Mwinyi Salim

Zula. Mimi nawakilisha kikundi cha Kukacha youth group of Likoni nikiwa kama chairman. Kwa hivyo tumekuja na memorandum yetu kidogo hapa ya points kama kumi hivi lakini nitagusia gusia. Kwa sababu nimeitoa hapo.

Kitu cha kwanza, hapa pazungumzwa maneno mengi lakini paguswa guswa lakini kila mmoja ajua pahali atakaa. Kwa hivyo Bwana Commissioner nasema wazi bila kuficha, sisi watu wa Pwani tumekata shauri Serikali tunayoitaka sasa ni ya majimbo. Hakuna hili wala lipi? Serikali tunayoitaka sasa ni ya majimbo. Na tungeitaka ni kwa sababu ya maonevu mengi ambayo tumefanyiwa. Kwa hivyo kutoka tulipopata uhuru mpaka leo tuna kidonda ambacho chazidi kukua badala ya kipungue lakini chazidi. Tena kamwe sasa chanuka.

Nasikitika kusema ndugu zetu wa bara mlio hapa tukisema majimbo sio kuwa eti twasema tuwafukuze. No, twasema kwa sababu ya uchungu na pia hatuwahesabu nyinyi kama ni watu wa bara. Kwa sababu watoto wenu twasoma nao hapa wasoma na watoto wetu. Tukisema watu wa bara twa-mean hasa wale walioko Nairobi. Ndio ambao watutesa sisi. Sio nyinyi. Kwa hivyo msishutike mukaona twasema hivyo kwa kuwafukuza. Na tukisema twataka majimbo hasa tuna-mean ile iko Rais. Kila Province watu wake wapate ule usawa.

Kama ni kazi tupate 90% ya vijana wetu wawe watapatiwa kazi. Ile kumi kwa mia tutasema nyinyi ndugu zetu tunaokaa na nyinyi hapa, haya mtoto wako wewe alisoma na wangu na yeye aende pale. Hiyo ndio tuna-mean. Lakini leo tukiangalia democracy hii tulioko nayo twaumia ndugu zetu. Hatuwezi kuvumilia tena. Imefika wakati hatuwezi kuvumilia. Kwa sababu ferry ile Mzee Mwajikaka yuko pale ajua vizuri sana historia ya ferry ile. Ferry zilikuwa za taabu. Lakini angalia leo ferry za leo watoto wetu hawapati kazi pale. Kwa nini? Hatuwezi kuvumilia twasema. Ferry ni za raha vile leo. Kwa kuwa na ferry matushali* tu na lodge huku na huku hawa wazee wanajua wote.

Kwa hivyo kulingana na hali iliyoko sasa sisi hatuwezi kuvumilia. Kilindini, watoto wetu wa wapi? Na tukija hapa twaambiwa education, education gani bwana? Form four ni form four. Standard eight ni standard eight. Kama vile mtangulizi alivyosema hapa kwa hivyo tusidanganyane. Sisi twataka jimbo letu na kazi yenyewe tutazimiliki kama zilivyokuwa zikimilikiwa wazee wetu na sisi leo twaweza kuzimiliki kazi zile. Na nasema hivi Bwana Commissioner, nasema bila ya uoga kabisa twataka majimbo Bwana. Nafikiria Tononoka aliwaambia Bwana. Kama hamtatuletea Katiba ya majimbo, mzee tutawaroga nakuhakikishia tutawaroga.

Ndugu zanguni tuangalie upande wa ardhi tumeumia vibaya sana mzee. Kwa hivyo naomba kuwe na law na right ya mwananchi. Kuwe na nini? Na sheria. Kama hivi sasa twatengeza Katiba nini? Sheria. Lakini nataka haki ya yule mtu wa pale ipatikane pia iwekwe ndani hapo. Haki. Kuna sheria na haki. Kama ardhi ya Coast ni yetu bwana, ni haki yetu tulipewa na Mungu bwana. Nyanza ni ya Wajaluo walipewa na Mwenyezi Mungu. Rift Valley ya Wanandi. Ukambani ni ya Wakamba. Na hakuna mtu anaweza kuwafukuza Wakamba pale, hakuna mtu anayeweza kumfukuza Mjaluo.

Kwa hivyo twataka right itumike katika mambo ya mashamba. Umekuja 'Bwana we nipe goodwill bwana'. Lipa kama five hundred thousand shillings. That is all the goodwill I am not selling my land. Ukishindwa biashara zako, rudisha shamba yangu shika njia uende zako. Ukioa bibi waenda wapi we bwana? Ukioa bibi wachukua bibi uende naye wapi bwana? Si kweli? Kama wewe ni ardhi umeinunua mbona hauibebi ukaenda nayo kwenu. Kwa hivyo tunasema sheria za land lazima right iweko. Tumekwenda kortini lakini korti iangalie right ya yule mtu ni ipi.

Hii ardhi ni right yake huyu mtu. Na hatuwezi kukubali kama mtu achukue elfu moja acres. Acres elfu moja kutoka ferry mpaka wa. Waambiwa wako chini ya …..ni ya Mkikuyu huyo. Ni haki hiyo? Kwa hivyo bwana hizi sheria zote zilizowekwa zilikuwa ni za ku-defend wale watu. Ma-tycoon binafsi sio za hawa wananchi wanyonge. Kitu chengine kama machiefs, ma DO's tungeomba wawe watu wa hapa.

Kwa mfano leo wanileteа DO atoka Pokot tutaelewana vipi? Mtu amekuja kitambulisho ni Msomali akipewa shilingi mia mbili tatu atoa kitambulisho. Leo hapa ni kweli hakuna wasomali. Au zamani tulikuwa na Wasomali hapa kwetu? Lakini leo kuna ………tutaishi nao vipi? Kwa hivyo naomba Katiba ikiwa ni Chifu ni DO awe ni mtoto wa Mwanganaza, awe ni mtoto wa Mwakuria, awe ni mtoto wa kaka tunataka namna hiyo bwana. Tusidanganyane bwana.

Kitu chengine kuna hizi haki kama za wokfu. Tunaita nini? Public Trustee Funds. Hizi ni za waislamu. Tatizo ukienda kule utasalimiwa na wakristu au vipi mambo haya? Haki ile ni ya waislamu isimamiwe na waislamu, wakristu, wakristu. Tusidanganyane bwana kwa kuwa pana kula linaekewa Rotich. Ukisha-sign vi-cheque akila pesa za watu wa kufa tu pale.

Hapana hatutaki hiyo bwana. Hatutaki bwana hiyo. Afadhali aliyemsihonga bwana. Atajua mwenyewe na Mwenyezi Mungu bwana. Kuna swala kama la Chief Kadhi pia. Tunaomba waislamu pia wenyewe wamchague Chief Kadhi. Hatutaki habari ya kuwa Njonjo sijui ni Home affairs Minister atuchagulia Chief Kadhi. Hatutaki. Tutachagua wenyewe. Walimu misikitini au kama ni sisi waislamu Chief Kadhi tutachagua sisi wenyewe bwana.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee Mwinyi, dakika tano zimekwisha yaingia ya sita nakupa fursa umalize.

**Mwinyi Zula:** Namaliza maliza maanake nagusia gusia. Kwa hivyo tunaomba pia Chief Kadhi tuchague wenyewe bwana. Waislamu bwana. Kuna swala la wafanyaji kazi. Ni kitu cha aibu sana leo Kenya miaka thelathini au arobaini ya uhuru tuliopata wapata mtu ana mshahara wa elfu tatu. Ni haki jamani? Nyinyi mlichagua watu wakawatetee, mlichagua watu wakakae kule wajiongezee mapesa. Leo mbunge wako anapata seven hundred thousand. Wewe mwenyewe jiulize unapata nini? Peanuts, you are getting peanuts. Nothing. Waziri wako anakula one million. Miaka mitano uliyomchagua wewe amekufanyia nini? That is a question. Zerograzing. Wananchi umefika wakati sio kuonewa bwana mna macho bwana. Hutaki kupeleka pajero wewe jaduong'. Hutaki kupeleka pajero wewe.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee Mwinyi mapendekezo wanipa mimi si janduong'.

**Mwinyi Zula:** Kwa hivyo ndugu zanguni wakati umefika tuchague viongozi…ooh sorry nilikuwa nazungumzia habari ya mishahara ya wafanyajikazi. Kwa hivyo ni aibu sana leo. Juzi waziri wetu wa labour anatangaza 7% yaani kila mia wapata shilingi saba. Sasa ikiwa wapata shilingi elfu tatu ujue utapata shilingi ngapi? Ishirini na moja hapo.

Kwa hivyo naomba Katiba hii iwe maswala yake makubwa iangalie mfanyajikazi kwa sababu mfanyajikazi katika nchi ni shareholder mmoja mkubwa sana. Kwa hivyo hiyo Katiba naomba pia iangalie mambo kama yale. Kwa hivyo mwisho kabisa nasema, with these few points on behalf of people of Likoni, I would like to thank you the chairman and you Commissioners kwa kututembelea hapa. Thank you very much. Asanteni wazee.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Mzee Mwinyi. Kama waweza kuandika jina lako pale. Sasa mimi ningependekeza nitaje majina watu kama watano, wengine wawe wanajitayarisha wajue namba yao inakuja. Naomba nimuite Ali Arumi. Mbaya Hamisi Mbaya. Akimaliza Mzee Mbaya, aje Elisha Oyoya akifuatiwa na Mzee Muhammed Abdullah Kaka.

**Mbaya Hamisi Mbaya:** Salam Alaikum bwana. Jina langu bwana ni Mbaya Hamisi Mbaya. Mimi ni mzee wa mtaa wa Kibuyuni. Lakini pendekezo langu juu ya Katiba, ajabu ni moja mimi ni mzee wa mtaa polisi waje hapo nyumbani, amshika mtu bila ya lolote bila ya kuonana na mimi. Nataka Serikali ijayo polisi kwanza ikiwa wamempata mtu kwa mtaa amuone mzee wa mtaa.

Huja yangu ya pili leo twapelekwa kortini, yule aliyekupeleka kortini ukifika humuoni. Waona wakili. Shahidi hatakikani. Serikali ijayo aliyofanyiwa madhambi na aliyefanya madhambi wawe na mashahidi kortini. Baas, nishamaliza sitaki kuchukua muda mrefu bwana.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Mzee Mbaya. Namuita Elisha Oyoya. Kama Elisha hayuko nilisema anafuatiwa na Mzee Muhammed Abdullah Kaka.

**Abdullah Kaka:** Shukrani Bwana Commissioner Abubakar Zein. Mabibi na mabwana sasa fungueni masikio kwa sababu nitakayoyazungumza Mungu atanijalia yatakuwa si yangu binafsi yawe yetu. Usihesabu haya nitakayoyasema kwa sababu nataka kuwaambia hawa wananchi waliofika hapa waelewe kwamba kwanzia uhuru uliotawalwa na Kenyatta mpaka Bwana Moi, hakujaundwa tume iliyo huru kama hii inayotengeneza Katiba. Tofauti ya tume zote zilizoundwa na tume hii, zote zilizoundwa Kayambombo, Molo, nini, ni za Rais. Lakini Tume ya wananchi wa Kenya ni yako Bwana Zein. Kwa hivyo tutoeni maoni tukiamini yote tunayoyazungumza baada ya kuchukuliwa maoni yetu tuna miezi miwili twaja soma yale tuliyoyazungumza hapa. Msiwe na wasiwasi.

Ngoma yaanza nihesabie sasa. 1904, mpimo wa hizi ardhi ndio ulianza tukiwa twatawalwa na Waingereza Kenya nzima. Kwa hivyo katika Coast, waliopima ardhi ni wale waliofahamu kupima ardhi ni nini. Babu zetu hawakujua kamwe jambo hilo. Ndio sababu 1963 wale walio elewa katika Kenya watu sisi twaangalia kupata uhuru ni kukaa ndani ya maghorofa. Kupata uhuru sasa sijui tuta ninino wenzetu ndipo walipoanza kunyakua maaridhi. 1963 ndio mwanzo wa kunyakuzi wa ardhi katika Kenya na ni mahali peke yake pwani palipokuwa na ardhi ya kupawa asanta waliopigania uhuru. Ndio sababu mwanzilishi wa taifa ni Ngala lakini katika history tuliambiwa ni Kenyatta.

Maana Ngala ndiye aliyeunda Serikali ya mseto Kenyatta yuko ndani. Na mwalimu Ngala alitufundisha na Waingereza wakitusaidia kwamba uhuru bora ni kila mtu kutawala mahala pake. Hilo nalo Bwana Kenyatta alitumia hekima za uongozi kwa sababu alibahatika kuongoza wengi wajinga, waelevu kidogo. Bwana Moi alipoingia swala hili akalifikiria akaleta district focus. Ilijaribiwa maana district focus ilikuwa mtu wa Likoni ndio apatiwa uchifu.

Mtu wa Mombasa ndio apatiwa u-DC. Ilishinda ndio huku huku ya 1965. Katika special paper number ten ya Parliament. Sisi wakenya ni milioni thelathini. Mtu akisimama hapa asema kiongozi awe na elimu, kiongozi awe na elimu. Huu uongozi wa wewe utakwenda ongoza waliosoma peke yake. Sasa mwasemaje mtu mpaka ajue Kizungu ndio achaguliwe? Moi hakuwa na makosa alipochukua Mulu Mutisya hajui kusoma akawa hakuingia Bunge? Lilivunjika lile Bunge lilipasuka. Kiongozi ni wa kuzaliwa na kipawa cha Mungu.

Kwa hivyo mimi naona katika Katiba katika lugha mbili za kitaifa. Mtu akiijua moja kwa ufasaha ni kiongozi. Mkinichagua nikaenda Bunge nitasema Kiswahili na yaandikika na yasomeka. Si lazima nijue Kizungu. Huyu Mwahima hajui kusoma na ni kiongozi wa peke yake aliyevunja rekodi yangu kuleta maendeleo area hii. Na namshinda kusoma.

Nilikuwa nikijivuna nimeweka record. Mwahima ameleta…… watu wengi wamepelekwa kazini, ile power ya succession iliyopitisha kule aliinyakua Nairobi. Ninino Shikadabu, Mwawenje ile niliipitisha aliipeleka kule. Hakusoma. Mwerevu. Kwa hivyo mimi nasema katika Katiba lugha mbili zitiwe na zipawe heshima sawasawa. Ikiwa wewe wajua Kizungu chako cha University, najua Kiswahili cha kuzaliwa. Wajua Kizungu hujui Kiswahili? Wasema saa hizi, kuna saa hizo, watu hizi. Nipatie tu Bwana Abubakar nitakutoa.

Sheria baina ya polisi na raia: Katiba iliyoko yamwaambia polisi mrongo ndiye mkweli. Imeleta mpaka kuna ufisadi. Serikali katika Katiba hii impe ukweli mwananchi polisi apawe urongo. Tushindane pale Diani akiwa atakanishika mpaka nijue anishika na nini. Kwa hivyo kikatiba mwenyewe mwananchi ndio apige kura, mwananchi ndiye ajuaye haki kwa hivyo haki kubwa iliyo na polisi sasa Katiba ya sasa tunayounda uwezo wa polisi upawe raia.

Bunge likivunjwa. Bunge limevunjwa Rais aliyoko bendera yapepea. Afanya campaign na magari ya Serikali, mawaziri wake wapepeza bendera wafanya campaign na uwezo wa uwaziri. Haki hii ife. Limevunjwa Bunge. Kama vile diwani ambavyo naye

hana mamlaka, mamlaka yachukuliwe na Town Clerk. Lile Bunge likivunjwa mamlaka yachukuliwe na Chief Justice ama Bunge liweke mtu huyo. Kwa sababu Rais akishapita kura huapishwa na nani? Nani anayemuapisha Rais kwa Katiba ya sasa? Chief Justice.

Kwa hivyo Bunge likivunjwa bendera iende kwa Chief Justice na Chief Justice ofisi yake iwe huru. Sio Moi Bunge lilivunjwa bado apeperusha bendera. Atashindwaje jamani mtu huyo? Sio Waziri aliyoko Bunge ni Mbunge wa bado Sheriff Nassir ni Waziri utamshindaje? Kama twakubaliana kwamba nchi hii ina vyama vingi. Bunge likivunjwa livunjike. Sio mtu kutumia mali ya Serikali kwa kampeni zake. Hatoshindwa na ufisadi hautokwisha. Kwa hivyo ndugu zangu mimi linaloniudhi ni ufisadi. Kila siku Rais wa nchi anavyojaribu kusema polisi waangalie ndio ufisadi umezidi. Mpaka sisi raia saa hii polisi wetu hatuwaamini. Kwa hivyo Katiba inavyoundwa ni lazima korti hawa ma-judge katika Katiba yetu mpya wawe wanatokana na mahala pengine na hakuna mahala pengine isipokuwa kikatiba.

Katiba yetu ianzishe Wizara ya sheria ambayo itakuwa na Minister wa sheria na siasa. Atasimamia, Attorney General yuko chini yake, mahakama ziko chini yake, Chief Justice yuko chini yake. Lakini Bunge likivunjwa Waziri huyo huyo naye pia amevunjika bakia Chief Justice. Kwa hayo Bwana Commissioner naonelea Katiba ikienda hapo tukivunja nafasi za Serikali kujitetea kikura haki itapatikana. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Mzee Kaka. Nitaita majina mengine manne. Sauda Ali ni mwenyewe, Abdullah Mwachai, Bakari Kandi, Hamisi Saidi na Fredrick Ondawa. Hao wajipange kwa kufuata mpangilio huo. Sauda Ali.

**Sauda Ali:** Salam Alaikum. Mimi kwa jina naitwa Sauda Ali. Nawakilisha makundi ya akina mama ya Likoni location. Kwanza naanza Katiba ya Kenya ina umuhimu na marekebisho. Pili twataka mfumo wa majimbo. Tatu, twataka tuwe na haki ya kumiliki ardhi zetu. Ya nne, kilicho juu ya ardhi ni chetu na pia kilicho ndani ya ardhi pia ni chetu. Rasilimali zetu ziwe zatufaidisha sisi wenyewe. Ni lazima tutekeleze sheria za majimbo.

Kanuni za uongozi: Rais awe chini ya Katiba ya wananchi. Twahitaji sheria ya kusimamia au upigaji kura anayegombea kiti awe ni wa jimbo lake. Rais awe ameoa kisheria. Akina mama tunataka haki ya kusimamia viti vya uongozi kama Councillor na pia kupata nafasi ya kuwa Councillor maalum. Tungependelea sisi akina mama ambao…..tungependelea siku ya akina mama ambayo huwa ni tarehe nane, mwezi wa tatu iwe ya kitaifa.

Hii nitafafanua kidogo. Kuna siku ya akina mama ambayo huwa ni tarehe nane mwezi wa tatu. Lakini siku hii haijulikani kwa kitaifa ambapo wenzetu wa Uganda na pia Tanzania huwa iko kwenye calendar. Ni sikukuu kama vile inavyojulikana Moi day ama Kenyatta day. Ajabu yake Moi day inajulikana na huyo Moi amezaliwa na akina mama. Leo akina mama hao siku yao haijulikani. Kwa hivyo tunaiomba iwe ya kitaifa. Mayor achaguliwe na wananchi wa jiji lenyewe.

Uradhi: Uradhi wa kiislamu uamuliwe kiislamu. Rufani ziwe za kiislamu pia.

Uamuzi bora wa kiislamu: Chief Kadhi achaguliwe na ma(imam) wenyewe. Korti ya kiislamu twataka ma-judge wawe na elimu mbili. Kwanza ya dini, pili ya dunia yaani ya Kiingereza. Tunataka walimu wa kiislamu wa kutosha katika mashule yetu.

Elimu: Watoto wa kike na watoto wa kiume wapate elimu sawa. Elimu ya nursery hadi ya upili iwe bure. Ma-sub-chief wawe ni wananchi wa area ama mtaa ule ule. Sio tuletewe ma-sub-chief watoka umbali huko. Ma-sub-chief tunataka wawe wanawake walio na mabwana na pia wanaume walio na mabibi. Mfano; hii nitagusia katika Likoni. Ukifika Kisauni kuna ma-sub-chief wanawake, Ireland kuna ma-sub-chief wanawake, Changamwe kuna ma-sub-chief wanawake. Lakini Likoni hii hakuna ma-sub-chief wanawake. Kwa hivyo pointi hii akina mama wameweka ili ma-sub-chief, Tume inayokuja ama hii mabadilisho ya Katiba tupate ma-sub-chief wanawake.

Wazee wa mitaa walipwe mishahara na Serikali ili wasiweze kuagadamiza wananchi wa mitaa. Wale wanaonajisi watoto ama akina mama wapate adhabu ya kufinywa mishipa ya uzazi. Waajiliwa kwenye viwanda wapate percentage ya sabini na tano kwa wale wakaaji wa jimbo lile.

Uraia: Raia wa Kenya ni yule ambaye kizazi chake chote kiko hapo alipozaliwa yaani kwenye hilo jimbo. Kupitia wazee wa mitaa na machifu. Mume aliyeoa ambaye ni Mkenya ana haki mke wake kuwa Mkenya. Raia wa Kenya ana haki ya kupata kitambulisho cha Kenya bila vikwazo vyovyote. Raia wa Kenya ana haki ya kugombea kiti na pia kupiga kura kwa mtu anayemtaka. Katiba inaruhusu uraia wa Kenya wa nchi moja. Asante. Kwa jina Sauda Ali, nawakilisha akina mama wa Likoni. Asante.

**Com. Zein Abubakar:** Bi. Sauda Asante sana. Abdullah Mwachai. Yupo Abdallah Mwachai? Hayupo. Bakari Kandi? Hayupo?. Hamisi Saidi? Hayupo. Fredrick odawa? Yupo. Karibu bwana.

**Fredrick Odawa:** Nawasalimu nyinyi wote macommissioners….

**Com. Zein Abubakar:** Mzee mwenye kofia mbona* uchokozi mwingi hivyo. Ziweke moyoni hizo raha zako usisalitiwe na ulimi.

**Fredrick Odawa:** Mimi kwa jina naitwa Fredrick Odawa lakini nawasalimu Bwana Commissioner na wananchi ambao wamefika hapa kijumla. Enyewe mtanisamehe kidogo kwa sababu enyewe mimi kusema kweli huwa najaribu sana. Kiswahili ni ngumu kidogo mtanielewa. Sasa huwa tumezoea Kiingereza sana sana. Nakumbuka wakati tulikuwa shule tunachapwa kabisa. Ukiongea Kiswahili unachapwa na wanataka uongee Kiingereza kila wakati.

Sasa nitajaribu kwa uwezo wa Mungu kwa hivyo naomba msamaha. Ndiyo. Sasa jambo ni hili mimi kwa upande wangu

ningependelea Serikali ambayo itakaye kuja iwe Serikali ya majimbo. Kwa nini nimesema hivyo. Watu wamepata shida sana. Kwa mfano hawa watu wa Coast, naweza patia wewe mfano mmoja ndio mtanielewa vizuri.

Kuna mahali nilikuwa kama mimi nafanya Nairobi kwa huyu Mkikuyu mmoja anaitwa Chris Kirubi. Na huyu Mkikuyu alikuwa kama ….enyewe mahali tulikuwa kama tunafanya pale kampuni, hakuna watu wa Mombasa. Kulikuwa na mtu mmoja tu na alikuwa Mndigo. Na pale alikuwa kama amewekwa mkubwa anasimamia watu pale kufanya kazi kama tuseme kama supervisor. Sasa pale ilikuwa mbaya sana mpaka ukabila uliingia pale mpaka hao Wakikuyu mbinu juu chini wakamtoa pale. Kwa sababu anatoka Coast na wanasema eti mtu wa Coast hajasoma. Na pale tulisikia uchungu sana. Hata mimi pia vile nilionolea kukaa pale ilikuwa shida.

**Com. Zein Abubakar:** Pendekezo lako nini Fredrick?

**Fredrick Ondawa:** Pendeleo langu ni hili: Serikali ya majimbo itafaa kusudi utoe hii ukabila. Hilo ndio pendeleo langu. Ukabila unajua uko kwa sababu hakuna Serikali ya majimbo. Lakini tungekuwa na hii Serikali ya majimbo hii ukabila ingekoma kwa sababu wale watu wanaleta ukabila macho yao itafunguka, watasema ‘ Ooh kumbe hawa Wadigo pia ni watu tuwaheshimuni’. Kumbe hawa Wagiriama pia ni binadamu kama sisi tuwaheshimuni. Kama wanataka kazi wapewe. Kama wanataka kazi wapewe. Kama wanataka kusoma wasome. Kama wanataka shamba ni haki yao kuwa na shamba. Unanielewa hapo?

**Com. Zein Abubakar:** Nafahamu.

**Fredrick Ondawa:** Sasa hii itasaidia sana. Majimbo itasaidia sana. Sana sana nilikuwa nataka kugusia upande wa masomo. Kwa mfano mwajua kuna watoto wengine wajeuri enyewe hawasikii wazazi na huenda pale kama wanasoma walimu huwa wanawachapa. Lakini kuna walimu wengine hawajui kufundisha watoto vizuri. Unaona walimu wanachapa watoto sana. Unajua mtoto pia ukichapa sana hakuheshimu anakosa heshima kwako na tena hata hawezi kusoma kisawasawa kwa ile njia ya sawasawa. Sasa ile ilikuwa kama mimi naomba kuna njia ambayo wanaweza tumia kama mtoto amefanya makosa.

Kwa mfano kuna miti pale kama hizi. Mtu akikosea anaweza pelekwa pale ili a-split firewood kama iko hii axe. Anakata hii firewood ama kuna slashing anapatiwa as a punishment badala ya kuchapa mtoto hivyo. Si mzuri. Kuna watoto wengine wanaweza wagonjwa uchape na afe hapo hapo. Sasa utafanya nini, utasema nini sasa. Sasa hii kuchapa mtoto sio mzuri sana na haisaidii. Na kama itawezekana huyu mtoto achapwe mimi kwa upande wangu naomba hivi, mzazi wa huyo mtoto aitwe na huyo mzazi achape mtoto wake mwenyewe. Sio eti walimu wanapatiwa jukumu ya kuchapa mtoto kwa sababu kuna walimu wengine wanachukua watoto naturally.

Kuna ile hatred ambao walimu wako naye kama anafundisha mtoto. Pengine mtoto hajapatia yeye kitu anataka. Pengine kama ni mtoto wa kike amekataa urafiki na yeye. Sasa ile hatred itakuwa hata akifanya vizuri namna gani ataangushwa kwa nguvu

kwa sababu ya hii masomo yake. Vile amefanya vizuri kwa mtihani watamwangusha kwa nguvu kwa sababu alikataa kufanya urafiki na yule mwalimu. Sasa ndio itakuwa namna hiyo.

Lingine ni hili, kama itawezekana headmaster ndiye pia pengine anaweza patiwa jukumu ya kuchapa mtoto kama itawezekana lakini sio mwalimu yeyote. Hata sio deputy. Headmaster ndiye apewe jukumu ya kuchapa mtoto. Na ajue jinsi vile anachapa mtoto. Si kuchapa kuua. Kuna jinsi vile unaweza chapa mtoto. Analala chini unchapa yeye kiboko vile zinastahili. Sio sana ile inaumiza yeye. Hapana. Iko pia vile una-discipline mtoto. Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa tumeifahamu hiyo.

**Fredrick Ondawa:** Sasa nyingine ambayo nilikuwa nataka kugusia ni kuhusu waislamu sasa kwa upande wa waislamu mimi ningeonelea namna hii. Enyewe mmesikia malalamiko yao ni kweli. Hata tukiangalia Coast Province, all over Coast Province ni waislamu sasa mimi naona kama hii Katiba itawekwa, Coast iwe Islamic state kama itawezekana. Coast Province the entire Coast Province iwe Islamic state na enyewe wataelewa kuna wakatoliki, kuna wa-christian pia watapatia wao uhuru wao kama wadini wengine lakini pia wachunguze wasilete makosa kwa hao waislamu. Kwa sababu hii iwe Islamic state kwa sababu Coast enyewe ukiangalia bila kudanganyana karibu Coast yote ni Islamic. Mahali popote ukienda unasilimiwa kiislamu. Mahali popote hata mimi huwa nasalimiwa kwa Islam. Wakati wowote hata marafiki zangu, they assume that I am a Muslim but in the real sense I am a Christian. Sasa ni hayo tu machache nashukuru.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Ungeenda pale uandike jina lako kwenye register. Cleophas Chelongo. Wale watakao fuatia Cleophas ni Rashid Hamisi, Abedi Juma, Patrick Ouma na Joseph Oluseli.

**Cleophas Chelongo:** Bwana Commissioner asante kwa hii nafasi umenipatia ya kutoa pendekezo yangu kuhusu Katiba yetu ya Kenya. First of all may be we should feature to the preamble of the Constitution. I do believe may be if the ……..Katiba iwe na kielelezo cha kumsifu Mungu na uhuru wa kisiasa, kiuchumi na sociologia.

**Com. Zein Abubakar:** Songeza microphone karibu na mdomo tafadhali.

**Cleophas Chelongo:** Katiba yetu iwe na kielelezo cha kumsifu Mungu, uhuru wa kisiasa, uhuru wa kisocialogia na kiuchumi. Pamoja pia iwe na kusisitiza umoja wa nchi. Halafu katika vipengele vitatu vya Serikali ambavyo ni Parliamentary, Legislature, Executive na Judiciary. Maoni yangu, Parliament should be supreme and should be above the Executive and Judiciary.

Halafu Judiciary pia itengewe commission yake iongozwe na kama Judicial Service Commission. Kuhusu on the President, we do see a fact here by; the President should be mandatory to him or her to be religious and in addition to that he should have a stable marriage so as to serve as an example to others. Age is of no (inaudible) where somebody has got a stable marriage and

is living with his family thoroughly.

Kwa upande wa Local Government, napendelea Mayor awe akichaguliwa na wananchi moja kwa moja. Awe na uwezo wa kuajili Town Clerk pamoja na hao wakubwa wake katika councils ambapo sasa macouncillor nao wawe wakimwangalia mienendo zake na kumuangalia kwamba ananufaishi hiyo mji wote kwa jumla. Machifu waondolewe kabisa na macouncillor wasimamie upande wake.

Kwa upande wa ardhi nimeonelea mtu yeyote ameoa Serikali impatie ardhi kitu cha kwanza. Halafu ninaonelea kuwe na kiwango cha ardhi ambayo mtu anaweza miliki ambako zaidi ya hapo kama mtu anataka kwa mfano kama ardhi hiyo iko kama ni ekari kumi kwa kila mtu. Zaidi ya ekali kumi ziwe zinafanywa tax na Serikali. Iwe mtu ana-taxiwa. Na kama mtu anaacha hiyo shamba kama zaidi ya ekali kumi bila kuilima bila kui-develop he should be taxed even excessively.

Halafu kuna katika upande wa marriages. Naona ile marriage certificate has to be supreme. So long as its authenicity and validity during the term of date can be registered. Na pia kusumbua wananchi sana hii mambo ya petition kwa Government, kwa High Court, mambo ya kutaka letters of administration na nini ziondolewe. What we need this new marriage certificate should replace the letters of administration or something like that.

Halafu kwa upande wa dini kuna jambo moja hapa naona ni nyeti sana ambalo ningependelea katika Katiba lisisitizwe sana. Huu uhuru wa dini wenzetu wanauomba ni mzuri lakini pia nao waheshimu dini zingine kwa mfano kama haya mambo tuna ya mwembe tayari mara unakuta ndugu zetu wengine wakristu wanakashifu ninio Koran. Ama pengine wakuta waislamu nao wanaketi wanakashifu Biblia mimi sioni kama ni jambo mwafaka. Hilo ni jambo latakikana ….haliwezi leta sheria na utangamano wakati watu wanaishi mahali pamoja.

Kwa upande wa elimu naonelewa (inaudible) ambayo yakuambatanisha elimu hiyo ambayo inaambatana na mabadiliko ya information technology pamoja na hali ya dunia vile inavyokaa. Ni hayo tu yangu kwa ufupi Bwana Commissioner.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Cleophas. Sign register tafadhali. Rashid Hamisi. Abedi Juma. Patrick Jacob Ouma.

**Patrick Jacob Ouma:** Asante sana Commissioner na wananchi ambao wako hapa siku ya leo. Mimi sitarudia yale ambayo tayari ambayo yashapendekezwa na wenzangu.

**Com. Zein Abubakar:** Ndugu yangu taja jina lako kwa sababu tuna-record.

**Patrick Jacob Ouma:** Jina ni Patrick Jacob Ouma. Yangu ni ya kuhusu elimu kwa sababu mimi ni mwalimu. Pendekezo langu la kwanza, ofisi la director of education. Napendekeza ofisi hiyo ipewe security of tenure. Ni kwa nini napendekeza hivyo.

Mfumo huo wetu wa 8-4-4 ni mfumo ulioletwa na wale wakubwa bila ku-consult education experts. Education expert ambaye yuko katika Serikali ni director of education. Ikiwa director of education atapewa security ya ofisi yake ataweza kui-advise Serikali bila uoga. Tuna ule uoga wa kusema. Nikisema kwamba mfumo huu hauko sawa, kesho nitapoteza kibarua. Kwa hivyo tunaomba hiyo ofisi, tunapendekeza hiyo ofisi ipewe security.

Nitakuja katika Teachers Service Commission. Hii ni commission ambayo hivi sasa iko chini ya Ministry of Education. Napendekeza Teachers Service Commission ipewe budget yake bungeni. Twapendekeza hivyo kwa sababu hatutaki budget ya Teachers Service Commission iwe chini ya Ministry of Education. Kwa sababu mnavyojua nyote, Teachers Service Commission ndio mwajili wa walimu na ikifika upande wa fedha, mara kwa mara watasema hatujapata pesa kutoka kwa ministry ama hatujapata pesa kutoka kwa treasury. Tunapendekeza Teachers Service Commission, Bunge iwapatie zao wawe nazo wazipange wao wenyewe.

Mwisho kusema ukweli wananchi wa Kenya hawana uhuru. Uhuru …freedom of movement. Hivi sasa nikiuliza wananchi wangapi hapa wana passport, tutapata labda ni mmoja ama wawili. Wamenyimwa uhuru wa kutembea nchi zingine through being denied to have this document passport. Mimi napendekeza passport iwe ni document ambayo unaweza kwenda kwa ofisi yeyote hata ofisi ya chief na ukapewa passport bila shida yeyote ambayo uta-apply passport na utangoja miaka ndipo uipate. Why is it so? Hapo wananchi wame….they have been denied uhuru wa kusafiri hapa na pale.

Nitaongezea pia civil servants na walimu pia hawana uhuru wa kwenda nchi zingine kwa sababu kabla civil servant hajatoka hapa kwenda Uganda ama Tanzania, ni lazima upate kibali kutoka kwa Permanent Secretary. Ni kwa nini upate kibali ikiwa unaenda kutembelea rafiki yako hapa Tanzania. Kwa hivyo tunaomba, tunapendekeza kusiwe civil servants ama walimu wawe na freedom ya kwenda pahali popote bila kupata kibali kutoka kwa permanent secretary wa ministry yake. Tuwe huru kutembea mahali popote. Asanteni.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Tafadhali andika jina kwenye register. Joseph Oluseni. Sharia Nyange. Upo? Halafu wajiweke tayari, Seif Mohammed Manuali, Rajab Shumba, Hamisi Luguwa na Alois Sindigu. Wajiweke tayari hao.

**Sharia Nyange:** Nashukuru sana Bwana Commissioner na wananchi wote ambao wamejitokeza siku ya leo. Yangu machache sio mengi sana lakini kwanza mimi nitazungumzia kuhusu…..

**Com. Zein Abubakar:** Taja jina lako tuna-record.

**Sharia Nyange:** Ndiyo. Naitwa Nyange Sharia Allan. Kwa hivyo mimi nitaanza moja kwa moja na kuzungumzia mambo ya uraia. Sasa siku hizi ukisha maliza pengine form four ukiwa watafuta kitambulisho utaambiwa 'ooh sijui uende uchukue living certificate ya shule, ooh sijui uje na birth certificate, sijui nenda ukatafute sijui'…mambo mengi kweli ambayo wafaa uwe nao

ndio upewe hiyo ID. Na bila ID hiyo mwenyewe wajua kwamba huwezi pata kazi mahali popote utaambiwa 'kitambulisho chako kiko wapi'? Hata kama kumetokea kibarua mahali hupewi kwa sababu gani? Hauna ID. Ushaona. Hauna ID, utapewaje kazi.

Kwa hivyo mimi yaani napendekeza kwamba mambo haya ya ID yasiwe eti sijui mambo ya kufanyiwe Nairobi, you wait for sixty days. Mambo hayo mimi naona afadhali kama ni kwa chifu pale umwelezee kila kitu. Kila kitu ambacho wewe wafaa kuwa nacho pengine ni ID, photocopy ya ID ya mzazi wako mmoja. Hakuna mambo ya birth certificate ama nini. Kama wewe pengine hukusoma utapeleka nini pale. Kwa hivyo mimi naona uraia mimi napendekeza kwamba iwe ni photocopy ya mzazi mmoja ya ID hiyo imetosha. Halafu mambo ya kungojea sixty days hakuna. Wewe waenda pale kwa chifu wamaliziwa kila kitu, wapewa ID yako waenda zako na mambo yanaishia hapo hapo.

Halafu tena mimi nikiangalia kidogo upande wa mambo ya elimu. Utaona siku hizi kwamba kuna kitu ambacho naona watu wengi wamesahau, kuna ile ilikuwa ni elimu ya ngumbaru* ile ya wazee wale wa kitambo. Ushaona pengine babu yangu ama babangu hakuenda shule kwa hivyo kulikuwa kuna haya masomo ya jioni jiioni yeye aende akafundishwe pale ajue kuandika kidogo au sijui kama ni kutia sign aweze kutia sign babangu.

Kama twataka kununua plot mahali hatapigwa chenga ushaona sio mpaka eti mimi niwe pale niwe nikimsomea gazeti kila siku. Yu aniuliza mwanangu nini chaendelea. Leo naja nakaa pale namsomea babangu gazeti. Mimi napendekeza kwamba wazee wetu pia waelimishwe. Au siyo? Wapata yale mafunzo hata kama ni kidogo, kuandika kidogo. Au siyo? Wajifunze. Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa.

**Sharia Nyange:** Halafu jambo lingine ambao nilikuwa napendekeza ni kwamba utaona kwamba Serikali hii ambayo tunayo Rais ndiyo kama mambo yote. Yeye ndiye mwenye filimbi, yeye ndiye mwenye mpira, yeye ndiye mwenye kiwanja. Mkosana naye akuja achukua boli* lake, filimbi yake, huyo huyo aenda zake na uwanja pia yu aufunga yu aenda na uwanja wake pia. Ushaona?

Kwa hivyo mimi napendekeza kwamba haya mambo kama haya yabadilishwe kwama eti sijui the President is above the law, kitu kama hicho kiwe hakiko tena. Mambo ya sijui yeye ndiye Chancellor wa all public Universities. Mambo kama hayo yapunguzwe. Ushaona? Kwa hivyo jambo lingine ambalo ningechangia hapo hapo ni kusema kwamba kama mtu ambaye ni Rais yeye afaa kuwa ni mtu pia ambaye record zake ni safi. Background yake iko clean and clear. Hakuna mambo sijui alishtakiwa, sijui ni ufisadi, sijui mali zake zingine aliiba iba kitu kama hicho hakuna. Twataka yaani tuwe na mtu ana track record ambayo it is clean.

Halafu pia nikichangia mambo ya…..hapo hapo pia kuna mwenzetu ameongea hapo juu kidogo kwamba utaona Rais

mwenyewe yu ataka atumie zile rasilimali za wananchi afanye nazo campaign. Mtu ajapo ana helicopter atutie mapepe ati yeye ni Rais ama nini. Mtu sijui afanyiwa campaign na pesa za Serikali. Hakuna mambo kama hayo. Mtu kama asimamia mambo ya campaign ama ajitafutia mwenyewe kura atumie pesa yake asitumie taxpayers money, asitumie pesa za Serikali asituangushie uchumi sisi.

Halafu kidogo nikigusia mambo ya ministries zile ambazo ziko utaona Kenya enyewe uki-compare na United States, Ministries zenyewe nyingi kuliko za kule United States. Ministry of Water, Ministry of Public Health, sasa Public Health na Ministry of Health kuna tofauti gani? Kwa nini kuwe na waziri wawili sijui Minister of Public Health na Minister of Health? Mambo haya ya kazi gani bwana. Ministry kama ni ya Health, ni ya health mara moja. Mambo ya sijui Ministry of Education na Ministry sijui of vocals sijui nini. Hakuna mambo kama hayo. Mimi napendekeza yaani zile ministries they should be as minimal as possible. Ziwe kidogo iwezekanavyo.

Mimi nikizungumzia jambo la mwisho nikisema haki za kibinadamu mimi napendekeza hivi kwamba wafungwa wote, watu wote ambao wamefungwa wapewe uhuru wa kuangalia TV, wakusikiza redio, kusoma magazeti. Ushaona? Na pia kama mtu ni mgonjwa apelekwe hospitali asifungwe kama mbuzi kwenye kitanda pale. Kila mtu akiingia ajua si huyu mtu ni mfungwa. Mambo yale ni ushamba yaani eti sijui mtu afungwa na frame ya kitanda pale na ninio. That is primitivity mimi naweza sema hivyo.

Halafu pia mimi naweza sema pia watu wote ambao kama wewe ni mfungwa and then pengine wewe ni mwalimu ama ni daktari kitu kama hicho, yafaa pia upewe nafasi ya kuhudumia jamii and the community (inaudible) kitu kama hicho. Ili zile huduma zako zisi….watu wananchi wasinyimwe zile huduma zako za kuwatumikia.

Halafu pengine nikimalizia si jambo la mwisho niseme kwamba mambo ya kama mambo ya kortini haya, watu wasaidiwe. The Judiciary should assist people legally. Kama mimi pengine nimeshtakiwa ama nina kesi kortini lazima Serikali initolee wakili na kama mambo yale mimi siyaelewi nielezewe vizuri vile sheria ilivyo. Pengine babangu kama ninasema hakuenda shule, yeye ni mzee hajui chochote ameshtakiwa pale pengine kwamba kuna shida fulani kuna mgongano juu ya ardhi fulani pale na twataka tupeleke kesi kortini. Lazima apewe assistance which is required. Asante.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Sharia Nyange. Tafadhali andika jina lako. Seif Muhammed Manuali. Hayuko. Rajab Sumba. Hayuko. Hamisi Rubua. Hamisi Rubua? Alois Sindigu. Ngui Mutiso. Mwajaa Shilingi. Mwinyi Bakari Malao. Naam. Malachu. Ndio mzee wangu. Pole limeandikwa kidogo kidogo hapa.

**Mwinyi Bakari:** Salam Alaikum

**Com. Zein Abubakar:** Alaikum Salam.

**Mwinyi Bakari:** Mimi sina mengi ya kuzungumza hapa au nitaje jina tena.

**Com. Zein Abubakar:** Tafadhali mzee wangu.

**Mwinyi Bakari:** Mwinyi Bakari Malachu. Tayari bwana. Mimi sina mengi ya kuzungumza hapa maanake mengi yashazungumzwa. Kuhusu naotaka mimi ama wanataka wenzangu waliozungumza. Hususa bwana ni uhuru wa majimbo. Kama ulivoletwa kule Lan Caster house mpaka ukaja Kenya halafu ukabadirishwa hapa hapa Kenya na wenye kujua. Kujua kwingi maanake kusudi wagadamizi wengine. Kwa hivyo mwawacha mabubu nao wasema.

Huu ugadamizi namna hii mwawacha mabubu nao waseme. Kwa sababu ilikuwa sisi wengine hawatufiki hapa. Lakini twafika kwa uchungu. Kenya hii tunaambiwa Kenya hii, Kenya moja, uhuru mmoja kila kitu kimoja mbona University nane zote zimejengwa pahali pamoja. University nane haikupelekwa mbona haikupelekwa University moja moja katika kila mkoa. Zilijengwa University nane pahali pamoja. Bara. Kila kitu bara kila kitu bara.

Hapa kwetu 'zi.' Ukiulizwa ambao hamjui kusoma, hamjui kufanya nini lakini hatujui kusoma kuja waja. Akija hapa waingiza kuvaa buibui nayo. Basi kwa hivyo bwana mengi yashasemwa nikisema ni mengi. Uhuru wa majimbo maanake tukishapata jimbo hayo mengi yaliyosemwa na wenzangu yatapatikana lakini ikiwa huna majimbo tutasema bure pale ndani ya karatasi na hakuna lolote litakalofanyika. Utakuwa ni huo huo ugadamizi ule ule. (inaudible) kumfanya nini. Na hivi sasa uandikapo hayo maandishi lakini ikiwa ni ya majimbo ikiwa hakuna bwana ni hali ni hiyo hiyo ni hiyo. Rais above the law, sijui Rais chini yeye kila akate kila kitu yeye.

Hivi sasa ukishikwa wewe, mimi na wewe ukishikwa polisi aandika the statement wewe wenda fungwa, yeye umwone, washitakiwa kwa Judge, Judge akuhukumu wewe polisi aliposhika hayuko. Maanake iliandikwa ni malaika. Polisi wa Kenya ni malaika hawaandiki urongo. Kwa hivyo bwana mengi sitasema na nikisema yatakuwa ni uchungu nitalia bure. Na hakuna lifanyikalo. Kwa hivyo haya ni yeye mlizoea kutudanganya hivi hivi na hakuna litakalofanyika. Mimi nasema kabisa. Mimi naitwa Mwinyi Bakari. Langu la mwisho ni hilo. Halifanyiki lolote hivi. Ni hapa kudanganyana tu bure.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Mzee Mwinyi Bakari tafadhali andika jina kwenye register. Shakombo. Hebu msaidiane apate fursa afike huku mbele. Hebu mjaribie kumfikisha microphone hapo.

**Shakombo Mohammed:** Habari zenu. Kwa jina naitwa Shakombo Mohammed mwenyekiti wa chama cha Muungano group for the disabled. Niko hapa kwa niaba ya chama cha walemavu. Maoni yao katika sisi walemavu maoni yetu sote kwa ufupi tulikuwa tunaomba Serikali itupatie nafasi kwa upande wa Bunge ili tuweze kujitetea kwa urahisi kwa sababu tunapata matatizo mengi sana. Kiasi ambacho hata hawa wabunge wenyewe tukiwafuata au viongozi wengine katika Serikali inabidi watupatie

matatizo sana. Kwa sababu utakuta kama pengine walemavu wameakilisha mradi wao.

Kila wanavyokwenda wanaambiwa 'njooni kesho njooni kesho' na kule kwenda kwenyewe ni tikiti kwa huyo mtu pengine. Inabidi tunaghalamika tikiti kikundi kizima kwenda kwa mtu mwaka unaisha. Halafu baadaye ule atwambia mimi sina chochote, mimi sina uwezo wa kusaidia. Kwa hivyo tulipochunguza sana tukakuta kwamba huu ni unyonge mkubwa kwetu sisi. Ndio tukaomba tuweze kupata hii nafasi ya Bunge ili tuweze kujieleza sisi wenyewe moja kwa moja badala ya kupitia kwa mtu fulani tuwe tuna mtu wetu ambaye tunamwendea direct halafu yeye anapeleka maombi yetu mbele. Kwa sababu matatizo ya mlemavu, mlemavu mwenyewe ndio ambaye anajua matatizo yake yeye mwenyewe. Hiyo ni number moja.

Number ya pili, tumechunguzwa sana katika hizi mambo za harambee harambee. Harambee nyingi tunapozisikia tunakuta ni za watu ambao ni normal. Unasikia harambee za elimu, unasikia harambee za akina mama, unasikia harambee za vijana lakini walemavu huwa si sana kufanyiwa harambee. Na ni ya kuwa walemavu pia nao wana matatizo yao kibinafsi.

Kwa sababu utakuta kama pengine sisi walemavu tumesomea katika shule za ufundi. Na mtu baada ya kuwa ameweza kusoma ule ujuzi wake inabidi anakaa nao nyumbani na ni ujuzi ambao unaweza akajipatia riziki yake yeye na familia yake. Lakini inabidi sasa ule ujuzi wake anakaa nao. Na hali ya kuwa hawa viongozi wetu wana uwezo wa kufanyia walemavu harambee wakaweza kusimamia miradi yao wenyewe kikamilifu. Hiyo ni namba mbili.

Namba tatu, tulikuwa tunaomba Serikali iweze kushughulikia walemavu kwa upande wa vifaa. Kwa sababu utakuta kwa mfano kama vengine mtu ni kiziwi na kuna vile vifaa ambavyo viziwi vya kuwasaidia wasikie. Na kwa upande wa walemavu wa viungo. Pengine kuna kama hizi calipers nikizungumza Kizungu. Hizi vyuma vya kumsaidia mlemavu ili aweze kutembea. Na kwa mfano kama hizi baiskeli. Utakuta kwamba saa ingine baiskeli imeharibika mtu hana uwezo wa kurekebisha ile baiskeli. Mpaka ile baiskeli inapoharibika inabidi yule mtu sasa anatumia kutambaa. Na hali ya kuwa iko misaada ambayo huwa inatumwa ya kusaidia walemavu kwa njia tofauti tofauti.

Sasa hapo tunaomba Serikali iweze kufikiria sana kuhusu upande wa vifaa. Mlemavu wowote anapokwenda katika ofisi akizungumzia kuhusu vifaa. Akisema mimi pengine nimekuja lakini mguu wangu unaendelea kukunjiwa kwa vile caliper yangu iliharibika.

Hao viongozi waweze kufikiria sana. Wamwangalie yule mlemavu mwenyewe na yale matatizo yake. Halafu waweze kumsaidia kama ni kifaa cha miguu ama kama pengine ni kipofu anahitaji miwani waweza kumsaidia kikamilifu. Hiyo ni namba tatu imeisha.

Namba nne. Sasa nataka kuzungumzia habari ya polisi. Polisi kwa upande wa sisi walemavu pia wanatuonea. Kwa sababu kwa mfano kuna kama ile utakuta kuna ndugu zetu ambao ni vipofu. Saa ingine kama hana ile miwani unaweza kuwa unazungumza

naye hivi lakini Mungu amemjalia yale macho yake, ukimwangalia ni kama anaona.

Lakini Mwenyezi Mungu mwenyewe alimuumba hali ya kuwa haoni. Yale macho yako sawa lakini haoni. Sasa utakuta pengine saa ingine polisi wanatokezea wameshika watu sasa yule kipofu kiasi ya kushtukia kuna nini kinachoendelea, inabidi anatandikwa yule kipofu pale. Wewe huwezi kupisha watu barabarani. Halafu baadaye yule polisi anakuja kushitukizia kwamba huyu mtu ni kipofu.

Halafu na kisa chingine pia kwa upande huo huo wa polisi, kuna wakati mmoja kulikuwa kuna polisi fulani wanafukuzana na watu. Sasa katika ile kufukuzana fukuzana ikawa kuna kijana mmoja yeye ni deaf na ni dumb na hawezi kuongea kwa vile ni bubu. Ikawa amesimama pale sasa katika hali ile ya heka heka kusukumana huku na huku, yule bwana akawa yeye anashangaa kuna nini kinachoendelea. Yeye pia akaja akatandikwa akatiwa ndani ya gari. Wakifika kule wakashitukizia tayari mtu wamempiga kumbe hawezi kuzungumza na hasikii.

Kwa hivyo katika maombi yetu tulikuwa tunaomba Serikali iangalie yule mlemavu ambaye anaonekana katika kumwangalia kama ambaye yuko sawa iweze kumpatia kitu ambacho hawa polisi wanapotembea wajue kwamba huyu kweli yuko sawa lakini kulingana na hichi kibali alichokifaa kinaonyesha kwamba huyu mtu hatustahili kufanya kitendo fulani. Kwa ufupi tulikuwa tunahitaji kitu ambacho kitaonyesha mtu ambaye ni mlemavu kwa njia ambayo wakiangalia watakuwa wanajua.

Halafu nikiendelea kusonga mbele. Sisi walemavu kwa wakati huu, sisi ambao tuna miradi tayari kuna vitu vingine ambao kama hizi shule za walemavu au ukichungulia sana katika Mombasa shule ya Primary ni moja ni ile ya Port Reitz. Halafu Secondary iko Bamburi sasa inabidi pengine kuna wanafunzi ambao ni disabled wanahitaji nafasi. Hizi shule mbili zote zimejaa. Inabidi sasa mlemavu akae nyumbani mpaka atafutiwe nafasi.

Sasa vile anavyozidi kuwa nyumbani ndio wakati nao unaenda na pengine ile skuli inachukua kama watu pengine elfu moja. Na watu ambao wanataka nafasi za kusoma ile idadi yao imepita. Kwa hivyo tulikuwa tunaomba Serikali ikiwa itatuhurumia ituongezee at least shule moja ya Secondary na shule moja ya Primary ili tuweze kufaidika upande wa elimu.

Halafu kwa upande wa chuo cha ufundi. Pia tulikuwa tunaomba Serikali ituongezee chuo kimoja cha ufundi ambacho kitakuwa kinasimamia miradi ya walemavu ili walemavu wazidi kuchukua ujuzi baada ya kuwa wamesoma. Kwa sababu ukichunguza kama chuo cha ufundi cha Likoni huwa kinachukua wanafunzi kumi na mbili kwa mwaka kila baada ya miaka miwili. Huwa wanachukua wanafunzi kumi na mbili ambapo kama kungekuwa na chuo chengine at least tungekuwa wale ambao wamekosa nafasi huku wangeingia huko. Kwa ufupi yale ndiyo niliyokuja nayo ni hayo.

**Com. Salim Mwakusuma:** Asante sana. Mzee Rashid Hamisi. Abdallah Ali K. Abdul Abdallah. Omar Salim. Rehema Juma. Salim Mwakusuma. Salim ndio wewe? Haya Salim.

**Salim Mwakusuma:** Mabibi na mabwana salam alaikum. Kwa majina kamili naitwa Salim Mwakusuma. Mimi ndiye branch chairman wa Ford People Likoni constituency. Kwanza kabisa Bwana Zein na wajumbe wako nataka kuwapatia shukrani kubwa kuja at least kututembelea hapa mara ya pili. Tulikuwa na wewe hapa siku ya civic education na sasa at least utuahidi kuwa umekuja. Kwa hivyo already umeshatupatia motisha ambao pengine uwe utatusaidia. Wengine hu-promise and they do not come. Asante sana.

Mtaniwia radhi jameni. Mimi yangu nimeandika kwa Kiingereza nitasoma mara moja halafu nitaongea Kiswahili tafadhali. With your permission please. Mambo mengi ishaongewa hapa lakini ingali yale twayaregea yale yale. Hakuna mengine mapya. Kama hapa wameandika vitu kidogo kidogo. Wamesema mambo ya ardhi. Wamesema mambo ya ardhi, the indigenous to have more say on all land related issues. Environment should be as above.

Presidency: The Presidency should be rotational on Provincial basis i.e. Central and Rift valley have had their share. Now the next President should be elected from the rest of the Provinces so that each Province should enjoy a fair share of the national cake. Thorough vetting to be done on all Presidential candidates to ascertain their track records so as to avoid electing corrupt Presidents.

Presidential candidates should be knowledgeable persons both on national and international affairs. Presidential candidates should be married and be between fifty and seventy years old. Presidential candidate should be neutral persons void of any political party affiliation to avoid unnecessary wrangling and discrimination which lead to undue favours and upper handedness in handling national issues. We need at least only two political parties to make the political wave very competitive indeed.

Judiciary: Judiciary should be independent of the executive. Judiciary should finalize cases soonest possible to avoid unnecessary suffering of the suspects and remand which are already over congested.

Parliament: All MP's should have a minimum education of form four pass and not failures. i.e Grade C or Division Two of Kenya Certificate of Secondary Education. Parliament should have powers to suspend or sack habitual absentee MP's. Simnajua kuna ma-MP's wengi huwa twawachagua hapa lakini wakienda kule kila siku hawko kazi yao kuingia kule na kula keki na kutoka. Sisi twamchagua atuangalilie masilahi yetu lakini akienda kule class huwa ako nje. Such people Parliament should have powers kuwafuta kazi kabisa hatuna haja na watu kama hao. Kama umechaguliwa hapa uende kule kutufanyia kazi yetu. Si kula mshahara laki tano laki saba.

MP's to be eligible for pensions only after having one two consequtive five-year terms. Unajua sasa ukichaguliwa Mbunge tu, ule mhula wa mwanzo tu miaka mitano already mtu anapata pension. Hiyo ni very unfair. Kuna watu wengi hapa ambao hawana kazi ukiangalia pesa wanapewa, halafu wakitoka miaka mitano wanapata pension sasa ni kama waonevu. There is a

lot of money involved kwa hao ma MP's. Sasa inakuwa mtu akipata MP ni kama sasa he is more or else like a small god kama mungu kidogo. Mambo kama hiyo inaonekana kama si halali kabisa. Salaries and allowances of MP's to be reviewed by independent professional bodies and not by MP's themselves as is the case of now.

Mnaona juzi ile mishahara yao ilikuwa. Walitengeneza wenyewe hapo bungeni mara moja mara moja within two days mshahara umepitishwa. Na hapa ndugu zetu walimu wamepata taabu kila siku mishahara ina shida mpaka leo hawajui watalipwa namna gani. Wao wamerundikiwa rundo rundo ya pesa kila siku. Hii maneno si mzuri hata kidogo haya ni maonevu. Na ukiangalia watu wote hizo kazi kubwa kubwa wanazipata wanaanzia kusomeshwa na mwalimu kwa nini unamdharau mwalimu. Mwalimu ndiye ameanza kazi zote madaktari, ma-engineer, wa-MP, ma- Minister, everybody starts from mwalimu. Kwa nini huwa mwalimu wanamdharau. Hiyo si haki hata kidogo. Lazima walimu watendewe haki zao.

The President should not have powers to prolong Parliament until its lifetime is over.i.e. five years. Huyu President zile powers zake sasa anaweza ku-decide wakati wowote kuvunja bunge. Vile mwenyewe anafikiria. Hiyo si haki. Kama amechaguliwa kwa miaka mitano hiyo bunge lazima ifanye kazi mpaka miaka yake mitano iishe. Sio kuvuruga vuruga watu namna hivi vile nataka kama vile sasa wanafanya. Hii Parliament ni ya wananchi, Parliament si ya President. Hata yeye President yeye mwenyewe amechaguliwa na wananchi kwa hivyo lazima Parliament ifanye kazi ile imechaguliwa kwa miaka mitano kamili.

Sio kuwa mtu akifikiria tu leo pengine kuna upinzani mahali fulani, vunja lile bunge kesho tayari kura kesho tayari ashaingia amerudi President hapana. It must finish its five-years term. Nomination of MP's should be scrapped. Hii mambo ya wabunge wa kufanya kuteuliwa iishe. Kama mtu ataka kwenda bungeni, huyu mtu mpaka aende achaguliwe na wananchi.

Mambo ya kuchagua chagua watu pembeni pembeni u rafiki yangu, u ndugu yangu jamaa yangu enda huko sijui nominated MP nini. Hiyo si haki hata kidogo. Twataka ile Constitution ambayo inakuja sasa mtu akitaka kwenda Bungeni ajitoe kwa arena achaguliwe na wananchi. Mambo ya kungojea eti nomination hiyo is very unfair.

Watu wengine wanaingia tu kwa sababu ya undugu, urafiki na whatever. That is very unfair. Parliament should have powers to sack a corrupt President and take him or her to court on mis-conduct or abuse of office. Pia Bunge inatakikana ipewe mamlaka. Kama President amekuwa corrupt ama ametumia ofisi yake vibaya, Parliament iwe na jukumu la kuweza kumtoa huyu mkazili na ashtakiwe. Sasa President is above the law. Hata fines zote vile anataka hakuna mtu anaweza kufanya.

Sasa imekuwa kama President kama ni Mungu. There is only one person. ….mtu mmoja ambaye ni above everybody, Mungu peke yake. Lakini mudanda mwenzetu hapa hawezi kutubabaisha babaisha hapa. President akifanya makosa awe na haki ya kufutwa kazi na apelekwe kortini. Na kama iko makosa atiwe ndani. Any President hatusemi anybody in particular. Any President according to the Constitution that is coming.

**Com. Zein Abubakar:** Bwana Salim muda wako umeisha ungekuwa unafupisha sasa.

**Salim Mwakusuma:** Mbona wanipeleka mbio Bwana Zein.

**Com. Zein Abubakar:** Nakupeleka mbio kwa sababu pengine nirudie yale masharti niliyotoa kwamba ukiwa una mswada kama wako ulioandika, dakika tano, ukiwa hauna mswada dakika kumi.

**Salim Mwakusuma:** Sasa umechanganya changanya kidogo. Tafadhali Bwana Zein. Kwa ruhusa yako bwana. Kwa ruhusa yako tafadhali. Hapa kuna ingine tunasema, once Parliament is prorogued the President should hand over the running of the State to the Speaker of the national assembly until elections are held. Hii mambo Bwana (inaudible) ashasema hapa. Bunge likivunjwa President anafunga vilago anaenda kwao. Anawacha magari, anawacha mapolisi na kila kitu chini ya Speaker yaani inakuwa kama mtu mwingine anakuja kung'ang'ana na elections kama mtu mwingine. Lakini sasa si hivo.

Unakuta President Bunge imevunjwa anatembea na hiyo gari ya State, anakaa Statehouse, mapolisi wako chini yake kila mtu ako chini yake sasa mtu yeyote ambaye anapingana na yeye kama kwa upinzani wa elections inakuwa ni ngumu. Kwa sababu sasa anakuletea mapolisi, anakuletea nini. Wewe sasa huwezi kufanya kazi yako sawasawa. Lakini kama ni President anataka fair game. Iende kwao, kila mtu awe kwao halafu tukutane kwa arena.

As a good example, MP's salaries and allowances should be reduced to Kenya Shillings two hundred thousands due to the economic hardships the country is undergoing. The hefty allowances and salaries they get now make our country a laughing stock by the donor countries which we always bend and kneel for funds only for the same funds to be misused by a few disgruntled and very corrupt political officials.

Tumeshuhudia hii maneno. Unaona kama donor countries sasa wale ambao wanatufadhili, wanatucheka kwa sababu unaona kunakuja pesa mingi nchi ya Kenya imekuja halafu hizo pesa zote zinaisha namna hiyo. Zimeingia kwa mifuko ya watu kidogo. Halafu unasikia mtu ameenda kuomba. Mpaka mtu unamwomba pesa kila siku na hizo pesa ana mis-use unafikiri yeye ni mjinga atakupatia kila siku. You can't get that money everyday. Sasa bado Kenya sasa tunaomba tu pesa zikija zinaingia kwa mifuko ya watu kidogo.

Kwa hivyo hiyo mambo kama hiyo sio mzuri kabisa. Tena unaona mtu kama MP, MP sasa anakaa karibu na Kisaba na kuna watu sasa ambao hata wengine wamevunjiwa vibanda hapa juzi. Watu wengi hawana makazi. Watu wengi hawana makazi. Watu wengi wanapata shida hakuna maskuli hata wewe huwezi kuenda ukiumwa na malaria hauwezi kuenda hospitali na unakuta MP mtu mmoja anapiga mshahara wa laki saba.

Chief Justice anapiga one million shillings in thirty days. Milioni mzima mtu mmoja na hapa kuna watu maelfu hapa hata saa hizi

kuna wengine hapa hawajakula. Wamekuja hapa wawekewe chai na hawajui wataenda kula nini nyumbani. Na tuko wengi majority kama hiyo. Hiyo si haki hata kidogo. Kwa nini mtu mmoja anaweza kupata pesa mingi namna hiyo na bado wengine wanapata shida. Hiyo sio democracy hata kidogo. It is not fair. All parastatal chiefs to be appointed by Parliament for the use of period of twoyears as opposed to the current appointments by the President and practices which promote corruption.

Unakuta hao wakubwa wa haya ma-parastatal haya,unakuta mtu anakuwa appointed by the President. Sasa huyo akiwa appointed by the President, President kwa sababu he is the employer and he is the one who has appointed him lazima yeye hawezi kumpinga. Akiambiwa apeleke milioni kumi atapeleka. Maanake anajua asipotoa atafutwa kazi mwingine anawekwa hivi. Lakini kama ni Parliament inafanya hivyo at least kutakuwa na discipline. Unakuta kuna mambo mingi inaendelea kwa maparastatal kwa sababu yeye anapigiwa tu simu 'fanya hivi leta milioni tano.' Sasa atafanya juu chini mpaka hii milioni iende asipofanya hivyo ajua kesho atafutwa kazi. Sasa hiyo inakuwa si haki hata kidogo ambazo hizo pesa zingetumika pengine kwa mradi wa muhimu zaidi.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa Bwana Salim. Ukitaja mambo hayo bila kuyafasili utakuwa unaenda mbio. Ikipita dakika zingine mbili mimi nitakufungia time. Tafadhali dakika moja.

**Salim Mwakusuma:** Mambo ya Local Government tunasema ma-councillor at least mtu kuchaguliwa councillor awe form four. Tena amepita, sio form four peke yake na umepita. Sio only form four lakini umepita. Tukubali tusikubali elimu ni kitu muhimu sana jameni. Tukisema ati sijui ilikuwa ilikuwa …..ulimwengu tuliyo nayo sasa elimu ni kitu muhimu. At least minimum education. Utakuwa kama councillor kama hujasoma ndugu yangu utakuwa na shida.

Mayors should be elected by the people as opposed to the current mayoral elections by councilors only. Ma-mayor wachaguliwe na watu wenyewe sio councillors. Tukuwe ishirini kumi wamekaa kwa hoteli wanachagua Mayor hiyo ni makosa. Tumchague Mayor sisi wenyewe. Sisi wenyewe tumchague. Kwa sababu hapo utakuwa unakwenda powers vizuri. Lakini ma Mayor wawili watatu kukaa kwa hoteli hapo wanakula sambusa hapo halafu wanaenda kuchagua Mayor that is not fair. Nomination of Councillors to be scrapped. Ma-Councillors wao huchaguliwa hivi hivi kuwa appointed waondolewe.

Tupate Councillors, kama anataka kuwa Councillor asimame kwa jukwaa atafute kura kwa watu. Salaries and allowances of Mayors and Councillors to be reviewed by independent professional bodies. Current minimal salaries for Mayors should be Ksh. 100,000 while honoured Councillors should receive a minimum salary of at least Ksh. 80,000 per month ku-avoid corruption. Kwa sababu hawa watu wana shida nyingi sana nyumbani nyumbani huko. Saa yote waenda kwa Mayor, kwa Councillor kama hana kitu ataleta shida. Kwa hivyo at least tuangalie mambo ya mishahara yao.

**Com. Zein Abubakar:** Bwana Salim mambo mawili ya mwisho.

**Salim Mwakusuma:** Asante. Elections: Elections to be held every five years as is the case at present. Nominations to be held on the same day and time to avoid unnecessary grasshopping to other political parties. Elections to be held separately for civic, parliamentary and the presidential. So as to avoid unnecessary confusion as is the case at present. Electoral Commission should be independent of the Executive. Votes to be counted at the polling stations to avoid throwing, hijacking, stealing or inclusion of ballot boxes during transportation to counting centers.

All party nominated aspirants to be funded by the State indiscriminately. There should be a level playing field for all political parties during campaign period as opposed to the current system where the ruling party scores the shots. Cabinet appointments should be done according to education qualifications as opposed to the present appointments which has taken on board illiterate or semi-illiterate politicians just because they are cycle fans or protegious. Parliament to undertake the appointments. Hizo appointments zote zifanywe na Parliament. Si mtu mmoja afanye appointments kama vile inavyofanyika sasa.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Bwana Salim. Ukiandika register yako jina pale, tutausoma mswada wako. Umeshapitisha dakika kumi na sita. Mtu wa kwanza kupewa dakika kumi na sita katika siku nzima. Na kwa vile ulizungumzia mambo ya haki sana, nadhani utafanyiwa wenzako haki nao wapate fursa ya kusema. Asante mzee wangu.

**Salim Mwakusuma:** Asante Bwana Zein. Pole bwana kwa kuchukua muda mrefu.

**Com. Zein Abubakar:** Hakuna wasiwasi.

**Salim Mwakusuma:** Wajua tuna kasiasa kadogo hawa ma-legislators.

**Com. Zein Abubakar:** Na ndio sasa ukitia mashaka na ….. asante. Zablon Zilo. Mwanaidi Ali. Said Abdallah. Hamisi Juma. Bick Mang'ondi.

**Bick Mang'ondi:** Nashukuru kwa nafasi. Majina yangu yameandikwa mawili lakini usijali kwa vile yote hayo ni yangu. Mimi nina majina matatu. Penhart Bick Mang'ondi. Niliangalia nafasi ya karatasi nikaona haitatosha hayo matatu. Nimeangalia hiki kitabu ambacho niko nacho na ndani yake vile nimetia maoni ya wazee, watu wa umri tofauti tofauti.

Sijamsikia mmoja akitaja mambo ya kuhusiana na rights za wanawake. Na mimi ninaongea …..sijui hata kama nimechelewa ni sawa. Lakini ipo haja ya sisi tuelewe ya kwamba mwanaume na mwanamke kuna utofauti wa mamlaka. Mimi ninasema hivyo nikiwa ni mkristu na ninasoma Biblia ya Mwenyezi Mungu. Sijui kwa mwenye anasoma Koran tukufu, sijui anayapata mawazo yapi kwa mawaidha yake. Sijui. Lakini ninaona inasema mwanamke na amtegemee mwanaume.

Leo hii with our Constitution, mwanamke jamani ukishtakiwa na yeye hautoboi. Na hata mpaka imebidi mwanamke amdharau

mumewe. Na ninaongea hivo nikijua mnasikiza redioni hata juzi tu haijakuwa hadithi. Mwanamke amemwambia mume wake hivi ‘ haufai kitu’. Maanake wamekorofishana kule na mambo ya familia na halafu mwanaume amempiga ndiyo halafu anaambiwa wewe ‘you have done something wrong’.

Na hata hilo mmelisikia kwingine. Simply because huyu mwanamke ndiyo tumempa mamlaka ya kwamba atutawale lakini imepita mpaka amedharau hata mumewe. So, mimi ninafikiria kutoa pendekezo langu ya kwamba iwe ndio hatutaki yale mambo ya kumkanyangia mwenzetu chini. Maanake pasipo na mwanamke ukweli mwanaume, wewe si mwanaume. Lakini kuwe kuna kuheshimiana. Mwanamke ajue ya kwamba ni sharti amheshimu mwanaume. Na mume abaki kuwa ni mwanaume.

Jambo lingine, kuna uhuru wa ibada na hili jambo wenzetu wamelisema lakini inaelekea ni kana kwamba ni kwa upande mmoja kwingine hata hili jambo limesemwa tu na ni kwamba halionekani. Ninajua ya kuwa Serikali yetu inafunguliwa maofisi starting from Monday to Friday. Hata mpaka siku ya sabatu, itafanywa kazi mpaka saa sita na inawachwa. Kama hata ni benki au whatever. Lakini waislamu ambao wanafanya kazi hata na ijumaa inafaa wawe mskitini waswali waongee na Mwenyezi Mungu.

Dua zao wazipeleke kwa Mwenyezi Mungu wajibiwe vile Mwenyezi Mungu atawakubalia, ako ofisini na anatakikana saa hiyo aende akaswali. Mtu mkristu wa jumamosi anatakikana ofisi na huku imani yake inampeleka kwamba angekuwa anafanya ibada kwa Mwenyezi Mungu siku mzima. Mtu yule ambaye labda anaabudu siku ya jumapili inafaa awe ako pale mahali pa ibada afanye ibada takatifu kwa Mwenyezi Mungu.

Hivi vitu sijui kama Katiba itaziangalia namna gani maanake imeelekea kuwa kuna siku tatu zimeidhinishwa kuwa ni za ibada. Na kwa hivyo tukiwa tunamtambua Mwenyezi Mungu kwamba ametupa mamlaka ya kuishi, ametupa kipawa hata yule ambaye yuko Bungeni amtegemee Mwenyezi Mungu. Yule ambaye anaongoza, na aongoze akijua uongozi wake amepewa na Mwenyezi Mungu wacha hizi kura zetu eti tumemchagua mtu. Mambo mengine, wanadamu hata kwa kura saa hii najua watu wameshika cards zao hata mimi nikiwa mmoja wao. Lakini it is very unfair enough ya kuwa ile kadi yangu haitamchagua mtu.

Na ninasema hivi nikijua ballot box inakuja ikiwa ina makaratasi ambayo tayari yamepiga kura na iko hapo hapo. Na halafu tunaambiwa vitu vinaenda vya systematic. Unaambiwa hii shughuli imeenda mpaka imefika usiku. Na ule usiku unaambatana na mambo ya giza na kuanza kuleta ballot boxes zingine kwa ile station ya kuhesabu kura. Vitu vinafanyika vya namna hiyo na nimeshuhudia mwenyewe nikiwa nimesha kula hizo pesa za Electoral Commission nikisema mbele yenu vitu vinafanywa vya giza na havistahili. Ni vizuri vitu vifanywe mwangazani ili atakayechaguliwa awe amechaguliwa nuruni.

Jambo lingine kumekuwa mimi na askari basi ni mtu na adui wake. Na hili ni jambo ambalo wengine wanadamu wenzangu wameshaligusia. Na ningeonelea ya kwamba basi Katiba iruhusu hawa maaskari wawe wana ujirani mwema na raia ambao wanamtawala. Maanake kama kwa mfano, mkiniangalia mimi ni mtu ambaye nimetoka sehemu ambazo unaweza ukasikia tu

wamelipuana, wameanza tu kupigana. Na ukipeleka Serikali pale unaambiwa wameenda kutuliza waweke amani na kumbe sivyo. Simply because wanaenda kuua na si kuleta amani.

Hali kama hiyo huwa si nzuri. Inafaa kama wamesema ni amani, iletwe amani. Na kama basi ni vita hayo ni mengine. Na Rais akiwa atachaguliwa Rais wa kuchochea vita hilo wazo litakuwa lina laana machoni pake. Maanake hapa saa hii sikosi kusema mbele yenu ya kwamba ule utawala uliopo umemwaga damu vya kutosha. Na hata ni vitu ambavyo vinaendelea tu kuangaliliwa.

Mtu hajui chanzo lakini anapata anapigana na mwenzake tu. Anapigana na mwenzake na mtu ni jirani wako na unapigana naye. Chanzo ikiwa ni yule yule ambaye anakuongoza ati nikimchagua huyu awe ni kiongozi wangu lazima nimuue mwenzangu. Hicho ni kitu ambacho ni kibaya na ni cha kusikitisha kabisa. Sijui kama mengine jameni ….muangalie vizuri ya kwamba kila tendo la haki linasemwa kuwa tendo la haki.

Na haya mambo hasa ya kunyanyasa mfanyikazi. Kunyanyasa mfanyikazi. Nimelisikia na limeenda muda sana watu wakilisema lakini saa hii ninajua kwamba tunaendelea na ukoloni mamboleo. Watu walikuwa wanasema tu kihadithi kwamba tunatafuta uhuru lakini bado. Bado kabisa. Ni kunyanyasa mtu ili kwamba hata hapati haki yake. Na kuna jambo lingine ambalo ……

**Com. Zein Abubakar:** Bick. Muda wako umeisha ungekuwa unafupisha sasa.

**Bick Mang'ondi:** Sawa tafadhali dakika moja. Kile kitu basi ningeweza nimalizie ni iwe kuna hukumu ya haki kortini. Maanake leo hii kama nitashtakiwa na may be diwani. Najua ninaregelea kwa kitabu cha *Kusadikika* ya kwamba watu wanaamini yale mambo ya kipumbavu kwamba chifu kama amenishtaki basi he is right, hata akaninyanyasa, hata iwe amenikosea mimi. Mambo kama hayo jameni iangaliwe. Ya kuwa mtu kama hana na yule ambaye anavyo basi wote wawe ni sawa. Nashukuru.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Bick. Hussein Idi Mwasina. Mwita Cosmos. Okey. Fosi Hamisi. Richard Osubo.

**Richard Osubo:** Kwa jina ni Richard Osubo. Mandugu zangu, mababu zangu na wenzangu ambao mmeketi hapa na ma-commissioner. Yangu nitagusia labda upande wa labour wafanyikazi. Sababu mengi yamesemwa ningeanza kwa kusema kwamba kulingana na ile unyanyasaji wa mapolisi ama kulingana na ule unyanyasaji wa wale ambao waliokuwa juu, nilikuwa naomba public demonstrations ziwe legalized. Kwa sababu hii ndio njia peke yake tunaweza teta sisi wanyonge na tukasema ' hapa tumeonewa, hapa tunakosewa'.

Ya pili, kuna watu tunaita expatriates ama nikiwaunganisha na wengine niwaite investors. Nikianzia investors unapata kuna kampuni nikitoa kama mfano; hapa Mombasa sana sana tunafanya biashara na tourism industry. Kuna hoteli moja inaitwa Hilton

International. Natoa kama mfano. Iko Kenya, zingine ziko in the developed countries. Tuna Hilton Paris and such like. Ningekuwa naomba kwamba wakati investor anafanya application kuja kufanya investment within the country, ahakikishiwe ya kwamba kama ni waiter ambaye anafanya Hilton Paris apewe haki sawa na yule mtu atafanya kazi kama waiter Hilton Kenya. Ndipo sa tupate kupata ile manufaa ya ile kampuni na ile investment. Kwa sababu anapata pesa nyingi kama faida halafu zote zinapelekwa nje sisi twabaki tukilia umaskini.

Na upande mwingine ukihusiana na hapo hapo upande wa investors ni expatriates. Unapata mtu ametumwa kutoka the other side amekuja kama expatriate. Let me say ametumwa hapa kama ecologist, ameandikwa na kampuni after a short time tuseme kama ni yule General Manager alikuwa wa hiyo kampuni within the country, akishafika wakati wake wa kwenda retire halafu unapata what we call ‘promotion from within’. Unapata mtu anapewa kutoka ecologist ikafika G.M. Kulingana na sheria nilikuwa naonelea ya kwamba mtu kama huyo kama anataka kazi kama hii ni afadhali hata arudi kwa nchi yake tena afanye application ikuje vizuri kama GM sasa awachane na ile work permit ya kuitwa ecologist.

Na kulingana na hayo machache, kuna wakati tunapigia watu kura. Maoni yangu yalikuwa kwamba in Kenya we have forty two tribes. Kama ingewezekana na najua itawezekana kama itapitishwa kama Katiba kama wewe umetoka from another country, umekuja umeuliza citizenship ya Kenya, uwe burred by the Constitution kwamba hauwezi shikilia any elective post. Wewe ni uje ukae pale uongozwe na wale watu wenyeji wa pale wafanye kazi yao. Wewe tulia kama umekuja umefungua labda ni biashara zako ama kuna kazi umepata mahali, wewe fanya kazi yako elective posts uwachie wenyeji. Na hapo naona kwamba hapo tunaweza endelea vizuri.

Another thing I go to Parliament. Kuna wabunge wengi tunachagua wanaenda wanalala Parliament. Labda kama ni budget inasomwa mtu amelala amekata usingizi anakuja kusituliwa watu wakipiga makofi. Ukimuuliza budget ilikuwa vipi? Atakwambia ilikuwa nzuri sana kumbe mtu hakushika kitu hata kidogo. Nilikuwa naomba Parliament proceedings iwe covered live. From there we can be able to access ni nani ambaye ameenda kutufanyia kazi, ni nani ambaye ameenda kulala so that the next time tunamtupa tuna-replace somebody ambaye anaweza kutufanyia kazi ya maana. Ni hayo tu Bwana Commissioner.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Tafadhali andika register yetu huko u-sign. Godffrey Lavusa. Kwa sababu muda unazidi kwenda, tujaribu kuyafupisha mambo na kuyafanya haraka haraka tafadhali.

**Godfrey Lavusa:** Ma-Commissioner na wananchi wenzangu waliokuja kusaidiana katika hali ya Katiba nawasalimu hamjambo. Sasa mimi yangu yatakuwa machache kwa sababu mengi tayari yameshazungumziwa. Na kabisa nitaanza na our security. Police officers inatakikana wawe marafiki wakubwa sana wa wananchi lakini wananchi tukiwa pamoja na hao ni kama maadui paka na panya. Kuna wakati waweza kushikwa bila sababu kutoka kwako unaitishwa kitu kidogo. Mimi naonelea tuwe na Katiba ambayo itaruhusu mtu akishikwa bila sababu akilala kule huyo polisi apate kufuatwa na amlipe yeye na pesa zake hata kama ni siku moja ama ngapi amlipe wakati wake amempotezea huko.

Tukija upande wa vyama: Kuna mtindo mtu anaunda chama yake kusudi yule aliye na chama kikubwa amnunue. Ningependekeza ya kuwa tuwe na kiwango fulani cha pesa yatakikana mtu aonyeshe anazo ndio aruhusiwe kusajili chama ndiposa tuwe na vyama size tusiwe na vyama vingi sana. Na upande wa defection, nataka tuwe na Katiba ambayo itasema hivi; yeyote ambaye ata-defect wakati bado ako ofisini alipe na aende asiruhusiwe kusimama tena. Aende nyumbani atulie huko. Yule aliyekuwa number two achukue nafasi yake. Na tena by-elections mimi naona ni kama kupoteza wakati na pesa. Ikiwa tulijua huyu alikuwa number one ndiye huyo ako Bunge, huyu akawa number two, in case of anything ambayo inaruhusu by-election tunachukua number two mara moja tunamwambia 'ingia bungeni'.

Upande wa walemavu: Mimi ni mshiriki wa Salvation Army, kuna mwenzangu mmoja hapa alisema kuwa hawatambuliki. Sisi tunafanya juu chini hata alimweleza kuwa ile skuli ya Secondary hapa peke yake ya vipofu ni ya Salvation Army iko Thika. Na kuna Primary hapa. Sasa ningependa Serikali itilie mkazo sana itusaidie huu mzigo. Sisi ndio huwa tunafanya juu chini kile kidogo umepata una-submit ndiposa hao watu wanapata kusoma, wanapata na mambo mengine. Sasa Serikali itusaidie angalao hawa walemavu waandikishiwe pesa fulani ambazo zitakuwa zinawasaidia kwa mambo fulani fulani.

Kuhusu President, naona President wetu wa Kenya tumempatia kazi ngumu sana hata mimi huwa namhurumia. Mara ndiyo huyu huku, mara ndiyo huyu huku. Naona apunguziwe kidogo kazi. Awe ni Mkuu wa Serikali tu asije kupewa kazi zingine nyingi sana zile naona anazo sasa. Na kuhusu Presidential qualifications, naona awe thirty and above first of all. Awe Mkenya na awe hana makosa yeyote. Halafu mwishowe awe hajashikilia post yeyote kwa Serikali. Na mbunge naye awe eighteen and above na awe hana makosa yeyote na awe hana shughuli zingine.

Atoke tu kule kama mtu ambaye ako *tarmac*. Asiwe ametoka kazi nyingine anaingia kwa kazi nyingine. Councillor naye awe eighteen and above na awe amefika kiwango cha chini form four. Halafu tukaonelea miaka ya kuchukua kitambulisho ishukishwe kidogo kufika miaka kumi na sita.

Kwa sababu siku hizi vijana wana-mature haraka sana. Wanaweza kushughulishwa katika shughuli fulani fulani that is the age of sixteen. Hata wengi wanamaliza shule at the age of fifteen, hawatakikani wakae sana idle wakingoja kitambulisho upto eighteen. Ni hayo tu. Nawashukuru wote.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana. Umetumia exactly dakika tano. Unge-sign register pande ile. Shuhudi Abdallah. Patrick Wafula.

**Patrick Wafula:** Ma-commissioner na wananchi wenzangu habari ya jioni. Mimi kwa majina naitwa Patrick Wafula. Kwanza nitashukuru sana wenzetu ma-commissioner kwa kuchukua nafasi hii kuja kusikiza matatizo yetu ambayo Katiba tunayo sasa imetuletea.

Kwa kweli mengi yamesemwa na tunaomba yatiliwe maanani na yale machache ambayo pia tumesahau tunaomba wengine wajaribu sana kutukumbusha. Moja kwa moja Katiba ambayo tunayo sasa ni Katiba imbayo imekalia ngumu mwananchi wa kawaida na ni Katiba inapeana nafasi kubwa sana kwa matajiri. Sababu ya kusema hivi ni kweli kwamba mwananchi wa kawaida ambaye anajua tamaduni hasa za kuzaliwa kwao ama kule alikozaliwa ndiye anaumia. Na anaumia vipi?

Kwa sababu hana sauti ya kufika katika zile ofisi zinastahili kulinda haki yake kwa urahisi. Sababu hana pesa hana jamaa yake huko ambaye siku hizi wanamuita godfather. Kama hauna godfather Kenya hii ndugu yangu ama kaka yangu hauoni lolote lile ambalo unastahili kuona. Ukweli uliopo ni huu, polisi ambao tunao sasa katika Katiba tunayo saa hizi iruhusu polisi kwenda college ya polisi zaidi ya miaka miwili kuliko miezi sita wanaenda.

Maanake kwenda miezi sita tu ni kujifundisha lugha ile wanatumia ' unatoka wapi nani, unatoka wapi hii'. Sasa hii you cannot imagine mtu ambaye anaenda ku-deal na public mwananchi achukue miezi sita peke yake college. Ataenda kufanya nini? 'kama hutafanya namna hii…sikiza nani….hii mambo umefanya ni mabaya sana'.

**Com. Zein Abubakar:** Patrick tumesikia pendekezo lako ni polisi wafunzwe miaka miwili badala ya miezi sita. Endelea.

**Patrick Wafula:** Mtu mwingine ambaye anastahili kwenda course ama muda mrefu wa ku-deal na mwananchi ni hizi ofisi za ma PC's na ma DC's. Watu hawa wanastahili nao pia wawe ni watu wametoka katika maeneo yale yale wanaenda kuhudumu ili wawe wanaelewa kabisa tamaduni ya pale pale. Huwezi kuniambia mimi utatoka hapa Ndigo* uende kwetu ubaluhya uniambie mimi natumia pombe ya kiasi fulani ama ya aina fulani nikitaka kumuoza binti yangu. Itawezekana hiyo? Haiwezekani.

**Com. Zein Abubakar:** Patrick tumeelewa. Songa mbele.

**Patrick Wafula:** Jambo lingine ni hili. Kama kuna mtu yeyote ambaye amechaguliwa bungeni na akawa mtu huyu ashatumika katika kama kiongozi wa shirika lolote ama mkuu wa shirika lolote. Mtu huyu hastahili kupewa tena wizara ambayo inalingana na lile shirika ashatumia. Mtu ambaye ashaachishwa ofisi kama Mkurugenzi wa Shirika la Posta, Mkurugenzi wa Shirika la Porti hastahili tena kupewa any other public office. Akae nyumbani achunge watoto wake.

Jambo lingine ni hili, mtu akisha enda bungeni mara mbili hiyo tosha. Mara ya tatu aachie mtoto wake yule ambaye ashasomesha pia yeye kama hakuna mwingine. Jambo lingine Bwana Commissioner walimu ambao wako chini ya TSC, budget ya kushughulikia mwalimu ndipo tupate elimu tosha Kenya hii, ipewe TSC direct kutoka kwa Bunge. Ipewe TSC budget yake. Isipitie kwa waziri. Iwekwe ng'ambo, iwekwe Busia hapa mwalimu anateseka mwanaye hajapata pesa ya kwenda shuleni, waziri hajaidhinisha hatujapata hizo pesa, mpaka lini?

Kwa hospitali, Mkenya anastahili kuwa na afya. Afya. Wakati huu tunaambiwa cost sharing. Hizi cost sharing mbona hatu-share ule ushuru Serikali inapata katika hizi mambo mengine. Hakuna habari ya cost sharing katika afya. Hiyo iondolewe kabisa. Tubakie ni Serikali ichukue jukumu la kulinda mwananchi kiafya, kielimu, vile imechukua jukumu la kuchukua ushuru kutoka kwa huyu mwananchi. Presidential escort. Wewe bwana binadamu kama mimi, sioni ni kwa nini anapewa gari hasa kama mfano wa ile magari yale. Yale magari ile engine system tu….five hundred shillings mafuta ishapotea. Hii magari inaenda moja, mbili, tatu na ni mlolongo hapa na ile gate na speed kali. Gari hii limebeba mtu mmoja mmoja, hiyo ni kali. Hiyo ni kali kabisa hiyo. Hiyo ndio kuharibu uchumi kabisa.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa endelea.

**Patrick Wafula:** Tuna watu mashuhuri ambao wanastahili kuwa na ile protection. Kwa kweli ukiwa mkubwa lazima ile security uwe nayo. Lakini uwe with a limit. Polisi ni mlangoni ni wa Serikali, mfanyikazi jikoni ni wa Serikali, mama jikoni anakula mshahara wa Serikali. Mtoto shuleni analipa pesa ni za Serikali sababu baba ni mfanyikazi wa Serikali. Why all this? Kama hufanyi kazi hufanyi kazi. Twautegemea ule mshahara peke yake. Nafikiri mnanielewa hiyo pointi vizuri.

Tuna scholarships zinakuja Kenya hii kutoka nchi zikija hapa. Jinsi inavyotumika ama ile njia inayotumika kutafuta mbinu za kupeleka watu ng'ambo kusoma ama nini na nini, zisipitie katika mikono ya wanasiasa. Hawa wanataka kura kutoka kwa wananchi. Lazima watachukua nafasi hii kutumia kwa kunyanyasa wengine ambao wanahitimu. (inaudible). Mimi nilipata scholarship ya kwenda India by then miaka ile iliyokwisha. Lakini sababu si kukuwa mfuasi wa yule mbunge wetu, niliambiwa nenda Ford Asili itakupa hiyo nafasi. Nikasema sina lingine.

Kwa hivyo scholarship ikitoketezea either ipitie kwa makanisa ama kwa misikiti. Wale ambao wana-qualify Mungu awajalie warudi watusaidie Kenya hii. Wakati tusha….sijui muda wangu kuwa umeisha. Saidia tatu tu. Wakati tumekuwa nao mgumu wa sasa ni wa uchumi. Uchumi huu haujaletwa na mwananchi wa kawaida, mwananchi wa kawaida ule anajaribu kwa vyovyote vile kukokota uchumi kwa sababu ya uvumilifu wa kazi ngumu anazozifanya.

Kwa mfano watchman, a mere watchman ambaye analinda magari kama hii kwa compound fulani, gari moja ni millioni kadha ile gari mwaona moja ile. Mtu anakesha usiku mzima kungoja lile gari lisiibiwe tairi moja. Alipwa shilingi elfu mbili na mia tano. Kwa sababu ya privatization ya kampuni za watu binafsi. Serikali iingilie kati na itilie sheria kamili kwamba mfanyikazi wa mwisho kabisa hata kama watchma, itaje kama watchman afaa apewe shilingi elfu kumi ama juu zaidi ya hapo. Si elfu tatu, elfu tatu hatakula leo mtoto atasoma wapi bwana? Wabunge Kenya hii watu mia mbili na ishirini na kitu weka nominated weka Rais, hao watu peke yao hata si theluthi moja ya a mere village.

Lakini hao watu wote wamekalia dollar zote za Kenya. Akisema 'ye' yes. Akisema 'no' no. Watchman tuliyo elfu ishirini katika village mbili, mshahara wetu kwa mwezi mzima times three thousand, watu hao tunapata pesa ngapi. Watchman na kiwango ya

wafanyikazi kiasi ile muangalie. Wangalie kabisa mshahara wao utengwe na utangazwe. Sio tu kwa sababu eti'ooh Kenya gazette iko'. Hata mimi sijawahi ona hata kama nimeona si gazeti lile. Bwana Commissioner kama pengine masaa yangu imekwisha samahani nimepitisha lakini mengi nitayawachia pale.

**Com. Zein Abubakar:** Asante nimekuongeza dakika moja. Asante andika jina pale. Hivi sasa imetimu saa kumi na moja na giza linaanza kuingia sasa kwa radhi zenu na ruhusa yenu nipunguze muda wa dakika kumi uwe dakika tano kwa kila mtu. Sijui kama inakubalika hiyo. Inakubalika? Sawa. Kwa hivyo dakika tano ukiwa una mswada, ukiwa wataka kuzungumza ni tano tu. Sawa? Athmani Kabanga.

**Athman Kabanga:** Ma-Commissioner na wazee wenzangu Salam Alaikum. Nafikiri mengi yameshaongewa lakini mimi nitaongea tu kidogo. Na nitaanza na Bunge. Kwa sababu ya kuepuka Bunge lisije likawa dominated na kabila moja ama mbili, ninapendekeza kwamba mtu yeyote yu ataka apiganie ubunge lazima awe mwalati. Awe mwenyeji wa pale. Kwa sababu gani? Kwa sababu tusije tukajaza Bunge kabila mbili ama moja wengine wakakosa kuakilishwa.

Vile vile wabunge wasipewe uwezo wa kuibadilisha hii Katiba ambayo sasa twaitunga. Kwa sababu ile nyingine tunaambiwa ilibadilishwa mara thelathini na nane kwa miaka arobaini. Kwa hivyo tukiwapa tena nafasi kama hiyo hii twairekebisha hivi sasa lakini kesho wakikaa huko bungeni wataibadilisha. Kwa hivyo huo uwezo utolewe kwa wabunge. Isipokuwa kuwe wakitaka kuibadilisha mpaka tena warudi wafanye kama hivi wanavyofanya sasa.

Vile vile mishahara ya hao wabunge, kuwe na kamati maalum ambayo itakuwa inawakilishwa kutoka kila mkoa ambao watakuwa wanashughulikia marupu rupu na mishahara ya wabunge. Wasijiongeze wenyewe kama vile ilivyo sasa. Tukija kwa upande wa Rais yamesemwa mengi lakini mimi nitasema moja………na pia wakuu wa mashirika. Kwa sababu gani? Wakati wa mbele kama ndugu yetu Robert Matano hapa aliweza kupanda train hapa hata akifika Nairobi amefutwa. Alifutiwa akiwa …..nafikiri alikuwa amefika Kibwezi. Akifika kule waandishi wa habari wamuuliza 'hebu tueleze habari za kufutwa kwako'. Yeye mwenyewe hajui. Yu ajua bado yu a waziri.

Mwingine hata alikuwa ametumwa ng'ambo akifika Jomo Kenyatta yu aulizwa aeleze namna gani ana habari gani za kufutwa kwake. Na bado karatasi za mkutano anazo mikononi. Kwa hivyo uwezo kama huo utolewe kwa Rais. Tukija kwa upande wa political parties. Mimi napendekeza ziwe mbili tu kwa sababu zikiwa nyingi kama vile sasa sijui arobaini na nane sijui ni arobaini na mbili, tutakuwa hatuwezi kupata yule mwakilishi au yule Rais anayependwa na wananchi. Kwa sababu tuchukue vikiwa kumi. Sasa ikiwa kama vyama ni kumi halafu sisi tuchague hawa wa chama kimoja yaani kila kimoja kichukue nusu robo utakuta yule Rais labda amechaguliwa na watu kama wawili. Tukifanya in % utakuta amechaguliwa na 2% ambapo 98% haimtaki yule Rais. Kwa hivyo hatutapata yule Rais ambaye anapendwa na wananchi. Kama vile ilivyo hivi sasa tuliye naye.

Ukiangalia milioni tatu zilikwenda kwa upinzani, milioni moja peke yake na nusu ndiyo ilimchagua Rais. Kwa hivyo

hakutambuliwa na wale wananchi wanaompenda zaidi. Kwa hivyo tukipata vyama viwili ndio tunaweza kujua nani ameshinda. Nafikiri mwanielewa. Tukienda kwa freedom wa religion, uhuru wa dini: Mimi napendekeza kusiwe na ubaguzi wa kidini katika kupeana vyeo au kazi katika Government. Vile vile naenda mbio nafikiri.

Vile vile pia ninapendekeza katika uhuru wa dini nafikiri dini hata katika Biblia nimeisoma kidogo nikakuta inaelezea kuhusu mavazi vizuri sana. Wanawake wawe hawavai mavazi ambayo yamepita magoti, yawe yamestili magoti yao. Lakini leo utaona sisi tunajaribu kuzuia ukimwi lakini kama mwananchi amepasua mpaka vitu vingine vya ndani vyaonekana.

Nafikiri twaelewa kwa lugha ya kidini tunasema ni majaribu ambayo huwa yanatokea. Kwa hivyo tunaomba pia kama Katiba itawezekana iweke sheria ya mavazi ya watu namna gani wafae. Isiwe tu wanawake wetu wawe watatembea tu vile wanavyotaka au waume wawe watatembea uchi kwa sababu ya kuiga nchi za kimagharibi. Nafikiri mwanielewa.

Tukienda kwa upande wa elimu. Elimu utakuta kama University wenzangu wangu wamezungumza hapa. Utakuta University zote ambazo zimetengenezwa ziko sehemu ya bara. Kwa hivyo pia tunaomba ikiwezekana basi hizi Universities pia zigawanywe kimkoa. Kila mkoa uwe utapatiwa University yake. Na vile vile ma-college na ma-insitution yote yawe yatagawanywa hivyo hivyo.

Tukija tena upande wa wanawake: Wanawake wapatiwe haki zao hasa katika upande wa kuridhi. Kwa sababu kuna baadhi yetu kiislamu, wanawake wanaruhusiwa kuridhi babake anapokufa anaruhusiwa mwanamke wa kiislamu awe ataridhi. Mwanaume akipata moja yeye anapata nusu ya yule mwanaume. Mali ya babake anapokufa na vile vile mwanamke anaruhusiwa kuridhi mali ya mtoto wake anapokufa. Anapata sehemu ya 1/6 kutoka kwa mtoto wake anapokufa. Hata kama ana bibi ana nini lakini wewe ni mtoto wako na wewe ni mama lazima upate 1/6 ya yule mtoto wako. Ile mali ya yule mtoto wako. Nafikiri mwanielewa.

Vile vile anaruhusiwa kuridhi mali ya kakake ikiwa yule kakake hana watoto. Yeye anaruhusiwa kuridhi. Kwa hivyo mwanamke lazima awe atapata haki zake zile ambazo zinasitahili kupewa ambazo zimewekwa na mwenyewe aliye juu ambaye ni Mwenyezi Mungu.

Pia wanawake wawe wataruhusiwa kupewa vyeo vya juu katika idara za Serikali. Hiyo napendekeza. Sijui Bwana Commissioner kama waridhika?

**Com. Zein Abubakar:** Ni muda wangu wa kutoa warning sasa.

**Athman Kabanga:** Kwa hivyo bado dakika ngapi? Ama imekwisha. Basi hata hunipi warning ndipo sa wanipigia tu na wasema nimalizie?

**Com Zein Abubakar:** Nitakupa dakika moja tu.

**Athman Kabanga:** Kwa hivyo nimalize. Basi namalizia kwa ya mwisho. Mwanamke asiwe kama vile ambavyo kabila nyingine huwa wanalazimisha kuwaridhi na analizimishwa lazima aridhiwe. Kwa hivyo ikiwa mwenyewe apatiwe option, ikiwa yeye mwenyewe ataamua kuwa mimi sitaki kuridhiwa basi akae na watoto wake pale pale na awe ataishi vizuri. Sio alazimishwe kuridhiwa. Nina mengi lakini kwa hayo wakati umeisha asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Athman. Bi. Mwanajuma Swaleh. Hayuko? Wycliffe Omukulu. Hayuko? Bwana Hamisi Saidi. Okey. Bwana Hamisi utakumbuka ni dakika tano? Tafadhali.

**Hamisi Saidi:** Sawa. Kwa jina naitwa Hamisi Saidi na katika mapendekezo yangu katika Katiba mpya. Kwanza ningependelea Serikali iwe ya majimbo. Kila jimbo liwe na uwezo wa kumiliki rasilimali na kuwa na uhuru wa kufanya mambo yake. Pendekezo la pili kuwa katika uongozi wa Mayor kuwe na uchaguzi ambao utafanyika moja kwa moja kupitia kwa wananchi. Na upande wa katika zile haki za kimsingi, napendekeza katika Katiba iwe kutakuwa na utaratibu muhimu fulani wa kuwa haki zile za msingi kwa mfano kama elimu, matibabu, maji yawe yatakuwa ni bure. Katika maswala zile rasilimali ziwe zitamilikiwa na umma wenyewe.

Pendekezo langu la mwisho ni kuwa Bunge liwe na uwezo wa kumfuta kazi Rais na kumshtaki. Nikimalizia ningependekeza wabunge wale ambao watahama vyama vingine wachukuliwe hatua kikatiba.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Thank you very much Bwana Hamisi. Bwana Milton Oluoch. Hayuko. Bwana Juma Masina. Bwana Joseph memba.

**Joseph Oponyo Memba:** Ma-commissioner wetu, wananchi wenzangu namsalimu hamjambo. Mimi kabla sijatoa mapendekezo yangu, jina langu ni Bwana Joseph Oponyo Memba. Nitalaumu Serikali iliyoko kwa sasa kwa kuvunja vibanda. Kwa maana wananchi wana fimbo tofauti ya kupigana na umaskini na vibanda ni njia moja au ni fimbo moja ile mwananchi alikuwa anatumia kwa kupigana umaskini.

Serikali imechukua hiyo fimbo imevunja vunja, imetia kwa moto imechoma. Sasa pendekezo la kwanza ni hivi; Serikali itafute mahali kwa kila town au kwa kila pahali imevunja vibanda itafute pahali ijenge vibanda vizuri na itie number. Itafute kila mwananchi ambaye alikuwa na kibanda chake akiendeza biashara, akipata mapato ya kupeleka watoto wake kwa skuli, chakula na mavazi na njia zingine zote alikuwa anajisaidia nazo kutoka kwa kibanda hicho. Ichukue number impe aende achukue, aingie kwa kibanda hicho na impe pesa ya kuanzisha biashara vile alikuwa anaendelea. Kwa maana kitendo cha kuvunja vibanda kime-blind kabisa uchumi wa kila mwananchi ambaye alikuwa anapata hapo na imefifia maendeleo kutokana

na hicho kitendo.

Pendekezo la pili ufisadi: Ufisadi umeangamiza kabisa maendeleo ya nchi. Hakuna maendeleo shauri ya ufisadi. Agriculture imefifia, elimu imefifia, kila kitu. Kwa maana hata barabara transportation yote hakuna namna. Pesa zatolewa wanafanya ufisadi. Barabara havitengenezwi. Naomba Serikali itafute kundi kwa kila mkoa na lile kundi lielimishwe vizuri sana namna ya kupambana na ufisadi. Katika Katiba ya sasa ile itatengenezwa, kutengenezwe kundi la kupambana na ufisadi na waelimishwe kabisa.

Pendekezo langu la pili ni kuhusu ukimwi. Nitaomba Serikali iende hasara kubwa sana kwa mara moja ili iokoe nchi yetu. Idadi ya watu inaangamia na hata kuongezeka kwa idadi kumekoma au kunaendelea kukwama kwa sababu kila mwanaume alizaliwa kuzaa na kila mwanamke alizaliwa kuzaa. Lakini sasa hata wanaume wameogopa wanawake. Na wanawake nao pia wameogopa wanaume. Bibi anavaa mpira kusudi ameogopa bwanake kule anatoka kutembea nilimwona akisalimiana na mwanamke mwingine, mweupe sana amevaa buibui. Ataniambukiza. Sasa pendekezo langu ni kwamba Serikali ipime watu.

Watu wapimwe damu na watiwe crucifix. Watiwe crucifix. Ukiwa na ukimwi uwe na crucifix aina fulani. Ukiwa huna uwe na crucifix aina fulani. Ukiwa haujapimwa utajulikana. Lakini kila mtu atiwe crucifix. Crucifix ya asiye na ukimwi, crucifix ya yule ana ukimwi. Pendekezo langu ku-save the nation perishing.

Pendekezo langu la nne. Watoto: Watoto wetu watakiwa walindwe vizuri sana na wapate elimu nzuri. Ningeomba Katiba na Serikali yetu ambayo itaendeleza nchi yetu hii iangalie mpango hata kama Serikali yenyewe itaenda hasara sana lakini itumie pesa yake kwa njia ile itanufaisha watoto. Watoto wakifika miaka au klasi ya sita watenganishwe. Wasichana skuli ya wasichana, wavulana skuli ya wavulana. Kwa sababu hiyo stage sasa ni ile stage mimi naweza kuita…..ni ile stage ambayo ni ya upingamizi. Ile stage ambayo mtoto anaendeshwa na joto ya mwili.

Watoto wakifika wakimaliza Secondary school wawe na uhuru wa kusoma pamoja kwa maana hapo wako na normal akili kabisa ya kuelewa hii ni hatari, hii ni nzuri. Hii ni mzuri, hii ni hatari. Kwa hivyo ningeomba Seriali ikewezekana watoto wakifika hiyo stage ya Standard five au six, watenganishwe waende skuli ya wasichana, skuli ya wavulana. Na hiyo pia itakuwa njia moja ya kuzuia ukimwi.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana. Si umemaliza?

**Joseph Oponyo Memba:** Bado kidogo. Asante. Kuhusu polisi ningeomba Serikali iandike polisi wale wamehitimu academic standard ya juu. Sio kuchukua mtu ambaye hakusoma kwa sababu Abongo ndugu yangu, halafu wanaenda wanakuwa na indiscipline. Wawe watu ambao wanatii Mungu. Wawe watu ambao wako na understanding kufuatana na high education wamepata.

Hata ingewezekana wawe watu wa kutoka University. Na pia police training yenyewe ichukue muda kama miaka miwili au zaidi. Kusudi wawe wamepata elimu ya ku-understand environment na relationship na wenzao. Na pia polisi walindwe vizuri sana, wapewe handsoma salaries. Hata nyumba residence zao ziwe nzuri. Hiyo itawafanya wataheshimu wenyewe na hata hii uchafu ya ufisadi kuomba omba hata pesa zingine hawatumii kwa njia mzuri kwa maana ni zile wanapata ovyo ovyo. Wakipata wewe kwa njia wanakunyakua pesa, wanakunyakua pesa. Imekuwa mchezo yao. Hawatumiii hizo pesa mzuri. Wanaitumia kwa kueneza ukimwi. Thank you very much.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Thank you very much Joseph Memba. Mzee Hassan ako? Hayuko. Hamisi Mwalinda.

**Hamisi Mwalinda:** Kwanza natoa shukrani kwa Tume ya marekebisho ya Katiba kwa kuweka huru kwa mtu yeyote kutoa maoni awe mke awe mume. Na mimi nami maoni yangu ni kama yafuatayo: Kwanza napenda kusema kila kitu kiwe na mwanzo wake na mwisho wake. Nasema hivyo kwa sababu litakuwa jambo la kupoteza wakati na kuwapoteza wananchi kukiwa na kuendelea na siasa hata baada ya kuchaguana. Maoni yangu naomba baada ya kuchaguana wabunge, madiwani na Rais, siasa zikome na badala yake kuwe mawaidha ya kujenga.

Pili utamaduni wa mwafrika udumishwe na utiliwe maanani. Maana hata kabara ya kuja ukristu au uislamu waafrika wakenya walikuwa wakiheshimu utamaduni wao na mila zao. Na walikuwa wakiomba wanapata. Kwa hivyo utakuta utamaduni wa mwafrika au mila za kiafrika zimedharauliwa sana na wengine  tu wanakuja kutoka katika nchi za magharibi au ualabuni wakija kutuona sisi ni watu ambao hatuna fahamu, hatuelewi. Na ni watu ambao hatukusoma na hatujui Mungu. Hakuna asiyejua Mungu.

Kwa hivyo hili neno dharau kudharau utamaduni au mila za mwafrika ni kitu kibaya sana na wengi wa waafrika wamedhurika kimaendeleo au kijamii kwa sababu ya kusahau mila. Na kutokana na haya mambo ya mila unakuta watoto wetu hawaelewi hata ukimuagizia kwamba fanya hivi, fanya hivi utabarikiwa.

Kwa hiyo mimi naomba katika Katiba hii ambayo tunaienda sasa wale watakaongoza hiyo Katiba wazingatie sana hiyo mambo ya mila. Na kama hivi sasa inavyoonekana Kenya yetu kwamba uchumi ni haba sana. Na kila mmoja wetu hana analoweza kiuchumi. Kwa hiyo maoni yangu naonelea hospitali na mashule iwe bure ili kumsaidia yule mtu wa chini kabisa. Au yule mzazi mwenye watoto zaidi ya watano na hana hatua yeyote ambayo anaweza kufanya akaokoe ile family yake.

Nne, kuna wale dada zetu hawa wamelalamika sana katika upande wa kuwa wao wanaonewa, wanapunguziwa na mara nyingi unakuta sasa hawajaliwi kabisa. Hiyo ni kweli si urongo. Maana pale panapofuka moshi ni lazima moto uwe uko pale pale. Hawa wadada zetu wanaona mambo makubwa sana katika majumbo yao na hakuna wavumilifu kama wao. Mimi naomba katika Katiba ambayo hii yaenda sasa akina mama wafikiriwe vilivyo.

Maanake mama huyu huyu ni mamangu, mama huyu huyu ni dadangu mimi. Mama huyo huyo ni shangazi langu mimi. Kwa hiyo ifikiriwe sana sana. Maanake kuna madhehebu yanayo (inaudible).Wale waume wa kule sijui waume wa ninio wa sehemu za uarabuni ama sehemu za magharibi. Sisi wanaume wa kiafrika tuna tabia mbovu. Hatujali wala hatumkaribishi. Kwa hivyo mwanamke atambuliwe na kile anachotaka mwanamke afanyiwe kama inavyopasa ili mwanadamu sijui ninino.

Yeye ni mwanadamu sio mnyama au sio mtumwa kwa vile wewe umetoa pesa zako hizo shilingi sijui elfu ngapi umepigwa ndoa. Kesho wewe ni vile upendavyo. Ukifika pale unampiga talaka. Na uliishi na yeye miaka ishirini. Talaka hiyo kale ilikuwa ni ya nani kule. Au aende aanzeje maisha nawe umezaa naye. Hii ni ukolofi na ukafiri kabisa wa mwisho. Ni ukafiri kabisa wa mwisho na huna huruma hata kidogo. Uwe Islamu, uwe wewe ni mkristu. Huna huna. Wewe hebu kumbuka hiyo miaka mmeishi miaka ishirini halafu sasa wewe unakuja kumpa talaka. Mimi sina mengi ni hayo tu ndugu zangu. Asante sana.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Thank you very much Bwana Mwalinda. Abdallah Mwamose. Hayuko?

**Abdallah Mwamose:** Yuko. Kwanza natoa shukrani kwa ma-commissioner kufika hapa na wananchi wote wa Likoni ambao wamehudhuriwa kwa wingi hapa. Jambo ambalo pengine nitakuwa dakika moja kuharibu zile dakika zangu tano ni kwamba nilipitia pale asubuhi na nikakuta zaidi ya watu mia mbili……

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Abdallah waweza kujitambua.

**Abdallah Mwamose:** Naitwa Abdallah Halfani Mwamose. Mimi ni mwenyekiti wa Coast Drug Abuse Awareness Group Kenya miezi miwili iliyopita. Pia nitagusia sana kuhusu madawa ya kulevya. Kwa hivyo nilipofika Kwale nikakuta watu wengi sana kwa hivyo nilipokuwa nahudhuria hapa nilidhania ya kwamba pia sitapata nafasi ya kukaa. Lakini nilipokuja hapa nikakuta unyonge sana wa turnup ambayo leo tulifanya hapa.
Jambo langu la kwanza ambalo ningezungumza ni kuhusu madawa ya kulevya. Tumezungumza points nyingi nzuri nzuri hapa, za ardhi, za elimu, za natural resources. Hizo zote tunazipanga kwa sababu ya watoto wetu wale wako Primary school na wako Secondary school. Lakini sasa nitazungumza pointi moja ambayo inanihusu sana. Nilipopitia Mwatalafu ama hii sehemu hii leo, nilikuta watoto wamelala wengi zaidi ya sisi tuliokuja kwa Katiba kwa sababu wamekunywa ama wamevuta dawa za kulevya.

Ile Katiba tunayoipanga dakika hii hapa tunawapangia watoto hao hao. Sasa lengo langu ambalo nataka kuzungumza hapa la kwanza ni kwamba Serikali hii ya Kenya hii ambayo tunaipanga sasa Katiba mpya lazima ihakikishe kwamba kuna njia yoyote ya kuzuia madawa ya kulevya Kenya. Kwa sababu hatuwezi kupanga uchumi kama watoto hao hao tunaowapangia uchumi dakika hii tunapozungumza wamelala. Haitawezekana. Hiyo ni pointi ma-commissioner nataka mchukulie hatua ya lazima kwamba kama Serikali ambayo itachukua nafasi ya uongozi wakati ujao kama haitafanya ama kama haita-implement hiyo issue, basi opposition ihakikishe inachukua jukumu au Serikali hiyo ku-resign kwa sababu itakuwa haikufanya chochot.

Pointi ya pili nazungumza habari ya revenue collections. Tunapozungumza majimbo nafikiria tunazungumza mambo mengi sana ambayo yanahusikana na revenue collections. Kila mkoa una-collect pesa za kutosha na hizo pesa zote hazitumiwi kuendeleza sehemu hizo pesa zinazotoka. Tunataka majimbo kwa sababu ya kuhakikisha revenue collections zetu at least 60% ya hizo revenue zina-develop hizo areas. Ndio sababu tunataka majimbo. Hatutaki majimbo tu kwamba tunataka majimbo lakini pesa ziende kule kule. Hapana. Tunazungumza habari ya revenue collection.

Pointi nyingine ni kwamba revenue collections zenyewe zinakuwa collected mpaka yule ambaye anafanya kazi ng'ambo pia awe taxed. Si ni Mkenya? Wa-Amerika ambao wako nchi za nje wanakuwa taxed hizo pesa zinakwenda Amerika. Kwa hivyo sisi nasi pia tutahakikisha kwamba wale ambao wanafanya kazi nchi za nje na ni Wakenya wanakuwa taxed na hizo pesa ni revenue zinakuja. Kama ni mtu atoka Coast, hiyo revenue inakuja na inasaidia Coast.

Education: Tumezungumza habari ya facilities na hiyo sitaongezea. Lakini ni lazima itiliwe mkazo kuhakikisha kwamba wakati Serikali inazungumza ama wenzetu wa bara wanazungumza kwamba Pwani watu hawakusoma, ni kwamba hawakupata facilities za kusomea. Sasa mnataka mtu awe amefika University na hakuna University Pwani.

Mtoto wangu wa pili dakika hii amepita amepata B(plain) na hakuchukuliwa University. Juzi nikienda kwa P.D.E akaniambia hata kuna watoto wengine wamechukuliwa kwa C+ (plus). Na sasa ukiangalia connections unakuta wale wachaguzi kule ni watu ambao pengine ni watu wa kule kule. Hiyo ni kazi ni lazima niifanye kuhakikisha amechukuliwa. Sitalala hivi hivi kabla kuangalia. Lakini kama kila kitu kiko katika mkoa, huyo angekuwa mtoto wa kwanza pengine kuchukuliwa.

Tunataka powers ziwe katika Local Government. DC, DO's, PC's watu wote wawe wanatoka katika hizo areas. Tuna mfano mzuri kama nina dakika pengine moja hapo wa security, sungusungu. Tuna system ya sungusungu Pwani ambayo imeonyesha mfano mzuri sana wa kwamba tunapokuwa na Central Government tunaweza kumiliki au kuongoza sehemu zetu. Serikali ilishindwa na kuzuia uhalifu Likoni lakini sungusungu ambao ni watoto tu wa hapa hapa wameweza kuondoa uhalifu. Hiyo ni mfano mmoja wa kwamba tunaweza Serikali za *majimbo*.

Serikali za *majimbo* zinaendelea kwanzia miaka arobaini iliyopita. Sorry kwa kusema hivi kwamba Moi amevaa uniform ya Kanu lakini anajiweka kwake kimajimbo. Kwa hivyo hatutaki vitu kama hivyo vitendeke. Sio kwamba eti nikizungumza mimi majimbo na mwingine akizungumza wengine wachukuliwa jukumu. Hapana, tunataka Serikali za majimbo ili kila kitu tutamiliki wenyewe. Kazi, tunataka kazi wachukuliwe watu wa local areas. Kama ni Pwani kuna kazi, wachukuliwe watu wa Pwani kwanza. Kama inahitaji ujuzi fulani ama elimu fulani hapo basi anaweza kutoka mahali pengine kwa sababu hatuwezi kulazimisha mtu aende pale na hana ujuzi wowote.

Namaliza nikisema ma-councillors na wabunge ni lazima wawe na elimu. Hatuwezi kuchagua mtu ambaye ni mbunge au

councillor na ambaye hana elimu. Uchaguzi ujao pengine yule mtu wa chini kabisa atakuwa ana degree ya kwanza lakini wote pengine watakuwa na masters na zaidi. Kama ukichagua mtu ambaye hakusoma atakuakilisha namna gani? Mimi namaliza hapo nikisema asante sana.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Okey asante sana Bwana Abdullah. Kuja uandike jina hapa. Nitachukua majina pengine tano hivi ili tujue kama watu wako hapa na tujue ni wangapi tunao. Reuben Muyagida. Ako? Reuben ngojea kidogo. Salim Hamisi. Ameenda? Okey. Salim Kiliko. Hayuko. Basha Juma. Daniel Kitavi. Hayuko. Evelyne Mupa. Yuko? Okey. Betty Kinyanjui. Hayuko. Lula Mwinyi. Ameenda? Okey. Tutachukua hawa wawili kwanza Reuben Muyagida halafu Evelyne.

**Reuben Muyagida:** Ma-commissioner na ndugu wenzangu waislamu na wakristu hamjambo. Mimi nitachukua nafasi kumwambia ya kwamba mambo ya kuona watu wakitembea watu wa bara wako hapa, watu wa Pwani wako bara. Hili jambo lilianzishwa na Mungu mwenyewe sababu alitoa Ibrahimu nyumbani kwake akampeleka mahali ingine. Na Muhammed naye akatoka Mecca akaenda wapi? Medina. Kwa hivyo ni jambo ambalo ilifanywa na Mungu na hata Yesu mwenyewe alisema ‘ Hakuna mtu anaweza kuwa kuhani mzuri nyumbani kwao, kusudi watu watembee kusudi wafundishane’. Lakini kwenda kwa mji ya mtu sio eti kwamba unapenda kumkalia lakini ni kufundishana. Hapa anakosea irekebishe. Kwa hivyo mimi ningeomba ndugu wangu mlifika hapa mimi nitaenda kwa jambo moja moja.

Nitaanza na kazi. Kazi hapa Mombasa kampuni nyingi zimeajiri watu vibarua na utakuta mtu anafanya kibarua kama miaka kumi na wakati anawachishwa hiyo kazi na alikuwa anafanya kila siku sio eti alikuwa anafanya anazimamishwa, hakuna malipo yeyote. Kwa hiyo tungependa katika Katiba hii huyo mtu aangaliwe vizuri sana asiende bure. Hiyo kampuni imlipe kwa sababu imepata faida.

Hivo vitu anatengeneza huwa vinauzwa kwa bei ya juu sana na kampuni imepata faida. Kwa hivyo hao watu wachunguzwe. Kitu cha pili kuhusu mfanyikazi ni mshahara. Mshahara kama kungekuwa na kitu kinaitwa ‘standing order increament’ every year, hatungekuwa na hii shida kusema nenda mkazungumze nini, hapana. Iwe kama ni shilingi 10% every year mtu aongezwe na hakuna cha majadiliano tena. Sababu vitu vinaenda mbele. Kwa hivyo mkifanya hivyo katika Katiba ijayo kila kampuni iwe na standing order increament hata kama ni 30%, 30% . Mfanyikazi anajua mwaka ukiisha nitapata changu.

Hapo nitaendelea sababu mtu mnaweza kaa miaka kumi na vitu vinaongezeka na huyo mfanyikazi hakuongezwa kitu. Halafu kitu chengine ningesema kwa upande wa education, Serikali ielimishe wafanyikazi. Hiyo kitu kimesimamishwa na hivi karibuni hata huku mahospitalini tutapata watu wa kufanya kazi. Hata walimu wenyewe sababu kuelimisha mtu imekuwa too expensive. Kwa hivyo hiyo kitu Serikali irudishe sababu tutakosa wataalamu kujielimisha wewe ni ngumu.

Kwa hivyo hiyo kitu tungeomba Serikali irudishe. Halafu kwa upande wa ardhi mimi nimekaa hapa sana kuna kitu mimi sijaona mtu akizungumzia lakini kitu kinaitwa 'house without land'. Karibu hapa pote hawa watu wote hapa Likoni ni nyumba ambayo huna ardhi. Huyu mtu kama alikubali kukodisha kiwanja au unamlipa, ikikaa miaka ishirini wafanye hesabu hizo pesa zijulikane umelipa pesa ngapi akupe kabisa. Kama nikumuongezea kidogo mmalizane sababu hii kitu itakuja lete taabu baadaye. Atakufa awaache watoto bila kugawanya hiyo shamba. Sasa hujui utalipa nani. This is the problem. Hii kitu iko hapa Mombasa sana and it is a very big problem. House without land. Sasa hiyo kitu kimekuja mpaka mtu analipa nyumba shilingi elfu mbili kwa mwezi whichi is wrong.

Sasa hiyo msipochunguza kitakuja kutuletea taabu Pwani sababu mtu amekodisha shamba lake lote and yet he is claiming he is got land, he has got no land because you have been paying for forty years. Na kwa nini usifanye hesabu upewe hiyo ardhi. Halafu mahali mimi ninge-comment tu vile wamesema wakenya to limit ardhi ya mtu kumiliki. Sio mtu kuwa na ardhi karibu acre mia sita hali Mkenya mwingine hata mahali pa kuweka mguu ama mahali anajua anaweza kukaa tu hata matako peke yake hana. That is quite difficult. Kwa hivyo tulikuwa na mengi lakini muda umekataa lakini nangependa ma-commissioner mchunguze sana hiyo vitu. Mfanyikazi tuwe na standing order increament.

Hii mambo ya kuambiwa watu nenda mjadiliane inaleta shida. Hata walimu saa hii wangekuwa wako mbali sana. Mtu anafundisha forty years. Wakikaa miaka kumi wanamuongeza 7% which is wrong. Kwa hivyo hiyo kitu ndio mimi ….tuna mengi lakini sitaenda ndani na ningependa nimpe wengine ruhusa nao waendelee na mambo hii ya ardhi mchunguze sana hii ' house without land'. Na hizi ardhi za Serikali hazijapewa mtu, raia tuungane watupe maana tukiwacha ndio wengine wananyakua. Asanteni na Bwana awabariki. Jina langu ni Reuben Muyagida Mugalla.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana. Okey. Thank you very much. Natunamuuliza

Evelyne.

**Evelyne Mupa:** Mimi langu naona maneno yote yashamalizwa. Kwa hivyo mimi nikuongezea kuwa mimi bado niko katika ule ule. Kwa jina mimi naitwa Evelyne Mupa ni mkaaji wa Dibwini Likoni hapa. Kwa hivyo mimi mambo yote yashakwisha lakini mimi naongezea kuwa tunataka ile Serikali ya majimbo katika Kenya yetu. Haswa ninazungumzia kuhusu majimbo kupendekeza Serikali ya majimbo ni haswa Pwani tumekuwa watu wa kunyanyaswa na tumegadamizwa ili tusiweze kuwa na maendeleo yeyote. Tayari kugadamizwa kwetu kuko…..nitatoa mfano wa Ramisi ambapo sisi hapa ijapokuwa Coast tumechanganyikana.

Tumekuwa watu wa Pwani wote, Wakikuyu na Wajaluo na ninio lakini wamekuja wakawa wakaaji wa Ramisi, lakini ile Ramisi factory ikafanyaje? Ikafilisishwa na ikafungwa. Ambapo kama ingeendelea mpaka dakika hii, sisi tungekuwa tuna uwezo wa kutoa mchango mkubwa kama kuna harambee watu wa Pwani wangeweza kutoa harambee kubwa.

Tungeweza kupelekana Ulaya, tukapelekana University. Unaona? Lakini sasa sisi tumegadamizwa watu wa Pwani kwa kila njia. Katika makazi tumegadamizwa ili tusiweze kuwa na uwezo. Kilifi kule tulikuwa na mtambo wetu huko waendeleza akina mama na wanasaidia watoto wao na school fees. Angalia hivi sasa wakina mama wetu wa Kilifi hakuna hata mmoja ambaye anaweza kumpeleka mtoto shule. Kwa sababu hana mahali pa kutafutia zile pesa ambapo alikuwa ameutegemea ule mkolosho na sasa umegadamizwa.

Hii yote ni kampeni ya mtu wa Pwani ili asiweze kuwa na sauti katika Kenya hii. Hivi juzi mimi nilikuwa Nairobi katika graduation ya mass communication pale. Katika hiyo list ambayo hiyo ni ile graduation ilikuwa kutoka nafikiri 1998 mpaka 2001. Kusema lile la kweli tulikuwa na msichana wetu hapo alikuwa ana-graduate. Sasa katika ile listi ya watu wa Pwani hakika tena ni aibu, hakika tena, nilisikia majina kama mawili tu kutoka Pwani. 1998 upto 2001. Imagine. Sisi watu wa Pwani hatukusikika. Nilisikia msichana wangu tu. Keira mtu akiwa amepata diploma. Akiwa na kijana mwingine amepata certificate kutoka Pwani. All hao wote mnandi, nini nini. Hiyo inaonyesha majimbo moja kwa moja. Kwa hivyo badala ya kuficha ficha tunaomba twende kwenye majimbo maanake washatengenezwa watu wa bara. Kwa hivyo ni hayo machache. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Naam. Bi. Evelyne. Jiandikishe tafadhali. Nitataja majina kadha tena. Naftali Ambwayi. Ako? Hayuko. Athman Maringizeni. Ako? Hayuko. Safi Mwavumo. Hayuko. Juma Rashid. Ako? Okey. Juma ngojea kidogo. Said Ibrahim. Hayuko? Francis Kanja. Hayuko? Uko. Okey. Kofa Swaleh Komora. Hayuko? Swaleh M. Mwakuto. Hayuko. Muhammed Miraji. Hayuko. Sophia Ali. Hayuko? Misi Juma. Yuko. Fredrick Otieno. Hayuko. Ondieki Omondi. Hayuko. Mkonga Kibwana. Mkonga yuko? Okey. Kidua Fadhili. Hayuko. Muhammed Chiguyazo. Hayuko. Faith Mbatia. Okey. Kusema Ramadhani. Yuko? Okey. Juma Mohammed Mwavujo. Yuko? Rashid Juma Yeya. Hayuko. Salim Mwabarahe. Yuko? Okey. Fred Orina. Hayuko? Na wa mwisho Mukiri Ngari. Hayuko. Kwa hivyo tuna watu kama sita hivi halafu tumalize. Okey. Tutaenda kwa Juma Rashid.

**Juma Rashid:** Salam Alaikum. Mimi kwa jina naitwa Juma Rashid, nawakilisha kikundi cha MCDI kutoka Mwatarafa. Kikundi hiki kina wanachama thelathini na sita. Kwanza naanza na utawala. Tunapendekeza utawala wa majimbo. Mtawala wa jimbo achaguliwe na raia walio na asili ya jimbo hilo. Maafisa wote watumishi wa umma wawe ni wa kutoka wilaya hiyo kwanzia afisa wa elimu, afya, jeshi, polisi na kadhalika. Ikiwa hakuna anayefaa kushikilia madaraka fulani katika wilaya ataazima mtu mwingine kutoka wilaya nyingine.

Upande wa Rais: Raais awe amechaguliwa kwa wingi wa kura kutoka kila jimbo. Rais asiwe juu ya sheria. Rais asiwe na chama cha kisiasa. Rais asiwe mbunge. Rais akipatikana na kosa la jinai, ufisadi au kutumia ofisi yake vibaya katika mahakama alazimike kujiuzulu*. Akitofanya hivyo, Bunge la taifa lipige kura ya kutokuwa na imani na baadaye achaguliwe Rais mwingine.

Bunge la taifa: Mtu anayegombania ubunge awe ni mtu hajafanya kosa lolote la jinai. Wabunge wasiwe na uwezo wa kubadili kifungo chochote cha Katiba. Lazima kuweko na kamati ya kitaifa yenye wanachama kutoka mikoa yote ambayo itashughulikia

swala la mishahara na marupu rupu ya wabunge. Mswada ukikubaliwa na Bunge iwe ni sheria moja kwa moja basi na kuweko dharura ya kupata mwafaka kutoka kwa Rais.

Mahakama ya Kadhi: Kuweko na mahakama ya Kadhi ndogo na mahakama ya Kadhi kuu. Kadhi aweze kuchaguliwa na waislamu wenyewe. Mtu ambaye ni Chief Kadhi asipewe kazi nyingine ambayo haiambatani na kazi ya mahakama.

Uchaguzi: Sharti Katiba izuie kugawa maeneo ya uchaguzi kiholela kwa lengo la kusaidia vyama ama kundi fulani. Sharti Katiba izingatie kanuni ya uakilishaji unaotilia maanani idadi ya wanaowakilishwa.

Kwa upande wa ardhi: Wananchi wapate title deeds. Wasiokuwa na ardhi wapewe ardhi na ardhi zinazomilikiwa na watu binafsi ambazo zinatumiwa na ma-squatter katika jiji la Mombasa, ardhi hizi zipewe ma-squatter hao.

Mali asili: Serikali ilinde mali yasiharibiwe na mtu au kitu chochote. Serikali iruhusu mali ya haya ya asili iliyoko katika Mkoa wa Pwani kumilikiwa na mtu wa jamii au jamii maalum ya shirika fulani maalum.

Tatu, wakazi wa Mkoa wa Pwani ni lazima wafaidike na mali asili yao katika kila mia wa mwananchi wa Pwani wapate asilimia themanini, zilizobaki ziende Serikali kuu. Wafanyikazi wa Pwani katika taasisi za mali asili wawe ndio wengi. 80% , watu wanaofanya kazi katika bandari ya Kenya wawe ni watu wa Pwani wenye asili ya jimbo hilo. Kadhalika wafanyikazi katika mahoteli ya watalii na taasisi zingine za mali asili wawe ni wa Pwani.

Elimu na taasisi zake: Serikali itoe elimu ya bure kwa mashule ya Primary, na Secondary. Mashule ambayo yalikuwa ya waislamu yaregeshewe wenyewe waislamu. Haki ya mwanamke: Mwanamke atambuliwe kuwa ni mtu mwenye utu kamili. Mwanamke ana haki ya kuridhi mali ya wazazi wake, watoto wake, mumewe na ndugu zake kama hana watoto. Matangamano ya mume na mke ya kimwili kujamiana yachukuliwe ni kitendo cha halali kinachofaa wakati wowote wangali ni mke na mume.

Ulinzi na usalama wa taifa: Polisi GSU askari, jeshi wawe na nidhamu ya kutoingia nyumba za ibada. Kunapotokea hali ya hatari kama vile vita Katiba iruhusu Bunge kuwa na uwezo wa kutoa ruhusa kwa jeshi au polisi GSU kukabiliana na janga hilo. Rais asiwe amri jeshi wa mkuu wa majeshi ya silaha. Msimamizi wa fedha za umma, mdhabiti na mkaguzi mkuu awe na mamlaka ya kushitaki wale wote waliochukua fedha za umma.

Kuwe na tume ya kuangalia fedha za umma na ufisadi. Wale wote wanaoshiriki katika ufisadi walazimike kulipa pesa zote

walizochukua. Mkuu wa sheria asiingilie mashtaka ambayo yamefanywa na mdhabiti na mkaguzi mkuu kwa kuondolea mbali kesi. Sharti pesa za umma zisaidie wananchi au kikundi wanapotuma maombi ya msaada. Mtu yeyote ambaye amehukumiwa kuhusiana na kosa la ufisadi, azuiliwe kufanya kazi ya Serikali.

Serikali za mitaa: Sharti Katiba mtaitenganisha Serikali za mitaa na Serikali kuu. Asante sana lakini la mwisho naomba ma-commissioner mnapomaliza shughuli zenu nimeombwa kidogo muonane na bwana wengine hapa.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Juma Rashid. Francis Kanja.

**Francis Kanja:** Asante ma-commissioner na wenzangu walio katika kikao hichi. Nikianza na yangu ni kwamba yale yote wananchi wa Kenya wamechangia katika siku ya leo ni mambo wameyadhania kulingana na yale mateso wanayopata. Hii ni kwa sababu hawajui lolote kuhusu Katiba yetu.

**Interjection from the audience:** Toa maoni yako kama umesimama. Hapana kaa chini.

**Francis Kanja:** Mimi naumia na njaa kwa hivyo nitaomba nitoe maoni kama nimekaa. Kwa hivyo yale yote wameongea leo wamefanya kuyadhania tu kwa yale matatizo wameyapata katika maisha yao. Lakini hakuna lolote wajualo kuhusu Katiba yao. Kwa hivyo mimi ningeomba la kwanza kabisa Serikali yetu itoe vijitabu vinavyoelezea vizuri kuhusu mambo ya Katiba yetu. Kila mwananchi wa Kenya mahali popote alipo awe na uwezo wa kupata hicho kitabu na aelewe Katiba yake vile ilivyo. Kama ni sheria pia tuelewe shida zetu vile zilivyo hata mtu akivunja kitendo kule mbele hana ile haki ya kujitetea kwa sababu tayari anajua alitenda kosa.

Katika upande wa sheria hivo hivo ningeomba wale wote walioshikwa na wakapelekwa magerezani waachiliwe kwanzia leo ama kesho. Kwa sababu vile vitendo walivyofanya, wengine walifanya wakidhania ni mazuri, baadaye wakashikwa wakaambiwa ni mabaya na wakafungwa. Mpaka wa leo bado wako huko. Kwa hivyo ni vyema waachiliwe na wananchi waelezewe kuhusu sheria zao. Mtu akishaelewa akishikwa akipelekwa ndio sasa awajibike kile kifungo chake.

Katika upande wa sheria pia ningependa kusiwe na mambo ya fine. Mwananchi akishikwa na kosa aadhibiwe kulingana na kosa lake lakini asitiwe fine. Kwa sababu ile fine inapendekeza yule mwenye pesa. Asiye nazo ndiye mwenye kuumia. Ukienda kama Shimo la Tewa wengi wale wako kule ni watu ambao hawajiwezi. Mtu na centi zake huwezi kampata pale ndani. Ni kweli ama si kweli?

Katika upande wa uchumi ningependa nigusie katika upande wa umoja wa wanakenya. Kusema ule ukweli mambo ya vyama vya upinzani ulikuja hapa kwetu kutukaa wenye sisi. Na ndio maana tukawa hatuna ule umoja wa kuchangia katika ujenzi wa taifa letu. Ningeomba vizuri sana ikiwa itawezekana vyama vyote vya upinzani vitolewe hapa nchini kwetu. Kuwe na chama

kimoja tu ambacho kinaweza kikakosoa yale maovu Serikali inatenda lakini tusiwe na vyama vya upinzani. Kwa sababu katika kupinga mtu anaweza kupinga kizuri na kibaya lakini katika kukosoa kosoa yale ambayo ni maovu. Ni sawa ama si sawa?

**Audience:** Sawa.

**Francis Kanja:** Nina machungu kwa sababu nchi yetu yafifia na twaitazama tu kwa macho. Katika upande wa wanakenya, ni vizuri wanakenya iliweke kwamba ni stakeholders of their own country. Kwa hivyo chochote kifanyikacho katika nchi hii yetu lazima sisi wenyewe mwanzo tuwe contacted ndio tueleze kwamba ni mazuri kwetu ama ni mabaya.

Kwa sababu wengi wa hao wakubwa, huambiwa mambo, mambo ya kutuumiza sisi. Baadaye ndio wanatuelezea 'ooh ni watu wa kutoka nje'. Kama juzi kuna haya mambo ya IMF. Walisema kuna vikwazo walitiliwa kama hivi ya kuvunja vibanda vyetu hapa Mombasa na katika miji mingine. Baadaye walisema kwamba ni IMF walisema wavunje hivo vibanda ndio wameweze kupata ile misaada. Kukosa misaada ndio wakaanza kusema kwamba IMF ndiyo iliwaelezea kwamba wavunje vile vibanda ndio wapate ile misaada. Tungepewa hilo jukumu la kuamua kwamba wavunje ama wasivunje, sisi wananchi tungesema wasivunje. Lakini wao walijitia wako na akili sana wakaamua lile jambo kwa mbili. Na saa hii ndio maana wakenya wengi sana wanaumia.

Katika upande wa uchumi ningependelea yaani hata kama ni mfanyikazi wa nyumbani mwenyewe asipate chini ya elfu kumi na tano kuendelea. Na yule ambaye anafanya kazi ya muhimu sana yaani ya juu sana tuseme President kwa sababu hakuna mwingine wa kufanya kazi ya juu zaidi kuliko yeye asipate zaidi ya elfu hamsini. Hivi sasa unapata mtu anapata elfu moja mfanyikazi wa nyumbani ili hali President mwenyewe apata mamilioni ya pesa kila mwisho wa mwezi. Ni haki ama hiyo ni dhuluma? Ni haki?

Katika upande wa makazi ningeomba yaani mwananchi wa Kenya apate kazi moja. Kama ana kichwa kimoja apate kazi moja. Lakini asiwe na kichwa kimoja apate makazi kumi, wenzake watakula wapi? Ndio maana siku hizi unakuta mtu ametajirika anaitwa yeye ndiye (inaudible) hata anadhania kwamba ni devil worshipper.

Kumbe anatumia mali ya wananchi kujitayarisha yeye. Mwingine amekuwa maskini kiasi cha kwamba anasema amerogwa kumbe amenyanyaswa na wale walioko juu. Ni haki ama ni vipi hapo? Ikiwa ni President akiwa President asiwe MP na asishikilie nyadhifa yeyote ile isipokuwa ile ya President ndio awajibike katika kile cheo chake cha u-President. Ikiwa yeye ni MP asiwe Minister. Ashikilie ule wadhifa wake wa u-MP. Ikiwa ni Minister asiwe MP kabisa. Yaani kichwa kimoja kazi moja.

Katika upande wa corruption, yeyote mwenye kushikwa na mambo ya corruption sababu ndiyo wameharibu nchi yetu adhabu yake iwe ni kifo. Ukishikwa na corruption kwa vile ndiyo imeharibu nchi yetu adhabu yake ni kifo. Mshaelewa? Na uwaambie ukienda huko kwao. Katika upande wa pesa wale wenye kutoa centi nje wakaenda wakazificha huko tafadhali hizo centi zirudi

hapa na mtu akipatikana na kosa la kupeleka pesa nje adhabu yake ni kifo. Ndio wakome kabisa.

Katika upande wa foreign investors yaani ikiwa mtu amekuja ku-invest katika nchi yetu, yule mwenye kupata licence awe ni mwanakenya mwenzetu. Asipawe licence, kazi ni yake, kila kitu ni chake. Akichuma apeleka kwao. Mwanakenya apate licence ndio yule mu-investor awe chini ya yule mwanakenya kwa sababu bila licence no business. Au siyo? Haya basi.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Bwana Kanja dakika zako zimekwisha. Taja……

**Francis Kanja:** Just one minute. Utajiri wa viongozi wa Serikali ni vyema uwe ukikaguliwa na kundi fulani la watu. Ikiwa mtu anapata utajiri kupitia yaani mambo ya kunyanyasa wananchi, ule utajiri wake uweze kuchukuliwa na urudishwe katika mikono ya Serikali. Ili asije akawa tajiri wengine huku waumia. Kwa sababu saa hii hii 70%-80% of Kenyans wanaumia ili hali wale wakubwa wetu ambao wako kule juu wanaishi maisha ya kifalme. Ni sawa ama si sawa. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana umenyonga wengi lakini…..sorry. Asante sana. Tafadhali jiandikishe. Natutamuuliza Misi Juma. Misi Juma ako? Okey.

**Misi Juma:** Ma-commissioner wote mliohudhuria wananchi wenzangu nawasalimu nyote hamjambo. Mimi naona wakati umekwenda sana nina mengi ilikuwa ya kuongea lakini nitayapitia pitia tu. Kwanza kabisa tungependa kuongea habari ya utangulizi wa Katiba. Hii Katiba yetu ya Kenya hakina kitangulizi wowote. Utangulizi wake umesema tu kama Kenya is a republic country. Huo si utangulizi wa kuwa si tunaufurahia. Tunataka utangulizi ambao umemtaja Mungu, umeitaja sera zetu sisi wananchi wa Kenya. Umeongea vile mateso tuliyoyapata wakati wa ukoloni na umeongea mambo ya kiuchumi, mambo ya kimaisha, mambo ya kimsingi vile Katiba itakavyosimamia. Hilo ndio jambo la kwanza.

Jambo la pili tunaongea habari ya Katiba ambayo tunasema Constitutional Supremacy. Tunasema hivi ya kwamba Katiba isiwe inaweza kubadilishwa na Bunge. Ikiwa Katiba kuna kipengele chochote kinataka kibadilishwe kiwe kinabadilishwa na wananchi na wananchi wakishabadilisha ndio kipitishe bungeni wabunge wafanye approval.

Mambo mengine ni mambo ya uraia 'citizenship': Hapa Kenya tunaambiwa ya kwamba ikiwa mtu mzazi wake alizaliwa wakati wa 1962 Disemba 12 anaweza kupata uraia. Lakini je hao wanaopewa uraia huo kweli huwa ni wanakenya? Mimi naona wengi huwa si wanakenaya.

Tunataka uraia upewe mwananchi wa Kenya ambaye ni indigenous kwa Kiswahili tunasema mwanati ambaye ni wa Kenya kabisa ndio awe atapatiwa citizenship. Na pia ikiwa mimi ni mwanamke nimeolewa na mtu mwingine wa nchi nyingine na

nikazaa watoto, turuhusiwe watoto wetu wapate hiyo citizenship.

Kwa sababu Katiba tuliyo nayo inawaruhusu wanaume wanapooa mtu wa kutoka nchi nyingine apatiwe uraia. Kwa nini sisi wanawake pia tusiruhusiwe kupatiwa uraia? Tunataka huo uraia tupewe. Na ule uraia wa by naturalization mimi naona uraia huo ufutiliwe mbali maanake wale wengi wanaokuja wanakaa hapo wanafanya maasi makubwa wengine ni ma-terrorist kisha wanatoa pesa katika hizi ministries zetu za mambo ya immigration wananunua uraia ambapo wanatuharibia sana katika masilahi yetu ya nchi.

Mamobo mengine nataka tuongee habari ya watoto. Hapa kwetu Kenya watoto wanadhurika sana kimaisha. Tuna kama hizi child abuse. Unapata mtoto ananajisiwa mtoto mdogo lakini katika Katiba hakuna kipengele kilicho na nguvu, kipengele ambacho kina ukali cha kusema 'je mtu anapofanya makosa haya huhukumiwa kifungo gani? Kama sisi akina mama tungependelea yeyote anayefanya kitu kama hichi kumnajisi mtoto mdogo, mtoto ambaye hajatimia hata umri wa miaka kumi na nane, mtu kama huyo ahukumiwe kunyongwa.

Hilo ndilo lingekuwa wazo langu. Na pia tukizungumzia mambo ya wanawake, wanawake wengine wanapigwa na mabwana wanauawa. Pengine mwanamke hakupika chakula ama hakufanya nini, tunataka pia kuwe na Katiba mwanamke akiwa abused na bwanake atachukua hukumu gani na Katiba pia inazungumzia nini kuhusu abuse za wanawake majumbani mwao.

Mambo mengine tunaongea habari ya health. Hii health hapa Kenya tumeambiwa ya kwamba afya ni bora sijui afya ni bure na kuna mahospitali. Lakini tukiangalia kama hapa kwetu Likoni constituency ile hospitali tuliyo nayo kubwa ni ino moja health centre na ukifika hakuna madawa, madaktari pia saa nyingine hakuna. Hatupati facilities za kisawasawa. Ikiwa hii na ndio health centre ya ino constituency yetu kwa nini isikuwe kubwa na iwe na facilities zote. Kwa hivyo mambo ya afya tunataka yazingatiwe sana na kuwekwe kipengele cha kuhakikisha kuwa kila mkoa kuna hospitali za kutosha na hospitali ambazo zina matibabu ya kisawasawa ambazo zitaweza kuwafaidisha wananchi wote kimatibabu.

Jambo jengine nitazungumzia habari ya political parties. Ama pia nyanda za kisiasa kwa ujumla maanake sina wakati wa kuongea. Hivi vyama vya kisiasa, kwa mimi naona maoni yangu vipunguzwe viwe viwili tu ama vitatu. Kwa sababu vikiwa vingi vinakuwa na ukabila. Kila mtu anaamka leo anaamka kesho anatengeza chama chake. Inakuwa sasa Wakikuyu wana chama chao, Wajaluo wana chama chao naWanandi wana chama chao. Lakini je vikiwa viwili sikutakuwa na mchanganyiko wa makabila katika kila hicho chama cha political party? Na pia hizi political party ikiwa the ruling party inakuwa financed by the government also political party should be financed by the government the same.

Maanake tunaona kama mwenzangu alivyosema ino ruling party kama hiyo ndiyo ruling party kama hivi sasa kutakuwa na mambo ya uchaguzi. Unajua ruling party nayo inatumia benefits zote za Serikali. Inatumia magari ya Serikali na pia kwa vile yule mweka hazina anayechunguza pesa za umma wa Serikali amechaguliwa na Rais ambaye Rais anatoka katika chama fulani

akiitisha pesa anataka kufanyia siasa, kwani wananchi atanyimwa? Hawezi kunyimwa.

Basi kuwe na uwezo wa kuwa zile pesa zetu za kiserikali za umma zile mfuko wa hazina ya umma kuwe vitakuwa vinachunguzwa na vinaangaliwa na Bunge. Bunge ndio liwe linaangalia sio eti mtu binafsi peke yake amechaguliwa. Yeye ndiye State finacial controller, yeye ndiye anaangalia pesa anajua Kenya kuna pesa ngapi. Na akiambiwa pia na mtu fulani anaweza kuzitoa hizo pesa. Madam ningeomba unipe muda zaidi kidogo kuna pointi moja muhimu sana.

Katika structure na system of government ningependelea iwe ya *majimbo*. Kama wenzangu walivyotangulia kusema. Ikiwa ya *majimbo* maisha yatakuwa mazuri. Maanake kila jimbo litakuwa linafanya bidii kuona standard ya maisha yake yamekuwa vizuri. Ile rasilimali wanayopata watakuwa wakiitumia kutengezea jimbo lake. Na yale majimbo mengine ambayo yatakuwa na shida pia yanaweza kushirikiana na majimbo mengine kusaidiana lakini tufanye Serikali hiyo ya *majimbo*.

Na pia mimi ningependa kusema kitu kingine. Kuna watu wanakuwa nominated. Unasikia mtu leo amekuwa nominated MP. Ukikaa kesho unasikia amekuwa Minister. Ikiwa yeye hakuchaguliwa na wananchi wake pengine pia ali-contestna akashindwa lakini anapatiwa u-MP baada ya siku moja anapatiwa u-Minister an wale wengine ambao wako bungeni miaka na miaka hawapei huo u-Minister. Je huo ni kweli ni sawa? Wale ambao wako nominated should not be given portfolios.

Hawatakikana kuwa elevated mpaka kufikia Minister wapatiwe Ministry. Wabaki pale pale kwenye MP's. Na pia sisi wanawake tunataka tuwekewe viti vyetu Bunge. Tuambiwe kama 30% iwe ni wanawake. Wanawake wenyewe wachaguane wawe na representatives wao kule bungeni. Waweze kusema mambo yetu na miswada yetu ya wanawake yote watusimamie.

Jambo jengine ni mambo ya disabled. Disabled hawakutajwa kabisa katika Katiba. Tunataka Katiba iwataje disabled. Kunajengwa milango kama ile revolving door ya bank, je hao ma-disabled wanaweza kupitia milango kama ile ama hao hawahitaji hizo shughuli za benki. Pia wao wanahitaji kuingia benki lakini kwa nini Serikali isifikirie. Majumba ya ghorofa N.S.S.F. mtu anataka kwenda kujua habari ya malipo yake, hakuna lift. Je mwananchi kama yule naye ni disabled atapanda vipi afike kule juu. Vitu kama hivo lazima Serikali ivifikirie sana.

Upande mwingine ni mambo ya Chief Kadhi. Sisi waislamu tungependa wanavyuoni wale wasomi wa kiislamu walio na elimu ya juu ndio waweze kumchagua Chief Kadhi. Na Chief Kadhi asichaguliwe na wanasiasa ama Chief Kadhi achaguliwe na Rais ndio amchague Chief Kadhi. Tunataka achaguliwe na wanavyuoni ndio wanaojua dini ya kiislamu ni vipi na ni sifa gani watakazomchagua Chief Kadhi.

Pia tupewe desk ya wanawake katika Chief Kadhi. Wanawake saa nyingine tuna matatizo mengi ya ndani na huwezi kumwambia Chief Kadhi kwa vile ni mwanaume. Kwa hivyo tunataka mwanamke mwenzetu awe pale. Hata kama si Chief Kadhi lakini awe pale tu na deski yake ambapo tutaweza kuwa anatuakilisha matatizo yetu mpaka yale ya ndani.

Pia we need a Court of appeal katika Chief Kadhi court. Kesi kama imeshinda isiende High court imalizikie pale pale kwa Kadhi tuende kwa Chief Kadhi court of appeal. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Thank you very much. Asante sana Bi. Juma. Thank you very much kwa hayo maoni. Na Mkonga Kibwana. Ako?

**Mkonga Kibwana:** Salam Alaikum(islam). Mimi kwa jina naitwa Mkonga Kibwana. Mambo mengi yashasemwa lakini katika kuyatilia mkazo sina budi na mimi kuyarudia. Kwanza kabisa ningeomba kitangulizi katika Katiba yetu. Tuwe na wimbo wetu wa taifa pia katika Katiba yetu.

Jambo la pili ningeomba Katiba hii iandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili kila mwananchi aweze kuisoma Katiba ile. Na vile vile Katiba ile iwe wazi kwa kila mwananchi. Kila mwananchi anayetaka hiyo Katiba awe atakuwa na haki ya kuipata Katiba hiyo yenyewe. Na Serikali ninayoitaka mimi ni Serikali ya majimbo kivyovyote vile. Hatuweza kuwa na uhuru wa kikamilifu kama hatutakuwa na Serikali ya majimbo. Na lau watu hawataikubali hiyo Serikali ya majimbo, mimi nawaomba watu wa Pwani watafute njia zozote zile lakini Serikali ya majimbo. Hata kama huko hawaitaki lakini hapa Pwani tubakie na jimbo letu.

Vile vile ningeomba Katiba hii itakayofika ule uteuzi wa mawaziri, wakubwa wa polisi, wakubwa wa majeshi, wakurugenzi wakuu usiwe mikononi mwa Rais kwa sababu Rais amepewa kazi nyingi ambazo zingine alikuwa amepewa kwa sababu ya Katiba yenyewe. Na vile vile tunataka asiwe vile Chancellor wa vyuo vyote vikuu. Ningeomba pia Katiba yetu upande wa makadhi wateuliwe na wanavyuoni na Chief Kadhi hali kadhalika. Na mahakama hiyo ya Chief Kadhi iwe itakuwa na uwezo wa kuhukumu sheria kulingana na sheria za kiislamu. Na waislamu vile vile wapawe ruhusa kama mtu hataki kuhukumiwa na korti hizi zizisokuwa za kiislamu, aliye muislamu apawe ruhusa atake kuhukumiwa kulingana na sheria za kiislamu.

Jambo lingine pia waislamu wawe na korti yao kuu ama court of appeal. Na ningeomba katika Katiba yetu pia vile vile tuwekewe wakili ambaye atakuwa akilipwa na Serikali, wakili huyu ambaye atakuwa akitetea wale akina Mkonga ambao hawana pesa za kukodi ama za kulipa mawakili. Kwa sababu sisi twadhulumiwa sana kwa sababu hatuna fedha za kulipa mawakili na hatuna wakili hali ya tunalipishwa kodi ambavo pengine kodi kama zile zingekuwa zinalipwa mawakili ili nao wakawa vile vile wanatutetea.

Kitu chengine ni tarehe za uchaguzi wa nchi yetu. Sio kama vile Rais anavyotaka, ningeomba Katiba yetu ituekee siku, tarehe na mwezi maalum ambao tunajua wakati ule ukifika basi Bunge automatically litavunjwa. Sio Rais akisema Bunge atavunja kesho kutwa hapo ndio tutakapojua pengine Bunge litakuwa limevunjwa. Kama hivi sasa tungekuwa tunajua moja kwa moja kwamba tarehe fulani uchaguzi utakuwepo. Kwa hivyo kila anayetaka kugombea kiti wakati fulani atakuwa wakati huyo tayari

ameshajiweka tayari kugombea kiti chake.

Kwa upande wa budget ningeomba pengine katika Katiba yetu iruhusu budget zile zisomwe Kiswahili ziwe wazi kwa kila mwananchi. Ili kila mwananchi apate kusikia ni nini hasa kinachozungumzwa. Lugha hii ya kununua wengine hatukusoma, tulikwenda skuli tu. Kwa hivyo hizi budget mara nyingi huwa zinatupita. Halafu budget zenyewe pia ziwe zitajadiliwa Bunge kwanza kabla hazijasomwa kwa wananchi ili wananchi wakasikia ni nini kinachoendelea. Kwa sababu Bunge letu pia sasa limekuwa halina nguvu katika budget zile.

Wabunge wote wanasikia kile kinachozungumzwa katika budget siku ile ya budget peke yake. Ambapo itakuwa pia baada ya hapo hawana tena uwezo wa kubadilisha chochote kwa sababu Rais hataki kitu hicho kibadilishwe basi hicho kitu hakitabadilishwa. Mimi ningeomba budget vile vile pia izungumzwe na wabunge kabla haijatolewa kwetu sisi wananchi. Mimi naona nitakoma hapo kulingana na wakati. Vile vile natoa shukrani kwenu nyote kwa kunisikiza.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Mkonga. Kusema Ramadhani.

**Kusema Ramadhani:** Salam Alaikum. Kwa jina naitwa Kusema Ramadhani. Kwanza Serikali ninayoitaka nataka iwe Serikali ya *majimbo*. Nataka Serikali ya *majimbo*. Na sababu zake zimeelezwa na watu wengi sana. Kwa hiyo mimi sitaki kueleza sababu zake lakini nafikiria kila mtu ameelewa kwa nini sisi hasa watu wa Pwani tunapendekeza Serikali ya *majimbo*. Na nataka pia niwaulize kuwa ikiwa mikoa nyingine haitakubaliana na Serikali ya *majimbo*, Tume hii itafanya nini ili sisi ambao tunataka *majimbo* Mkoa huu wa Pwani tujue tutapewa haki zetu au hatutapewa. Hilo ni swali ambalo nataka mkaliulize huko mbele.

Kitu chengine ambao nataka kuchangia ni kuhusu mitihani. Mitihani inayoandikwa au inayoletwa katika shule zetu inakuwa exam biased. Utakuta maswali ambayo yanaulizwa katika mitihani hii, inapatia au inachangia mikoa mingine iweze kufaulu zaidi. Kwa mfano mwanafunzi anaulizwa ni sehemu gani katika Kenya kunakuzwa kahawa. Swali hilo hilo utakuta mtu ambaye ametoka hapa kwetu Mkoa huu wa Pwani hawezi kupata swali hilo. Na akiwa atalipata ni dhana tu. Kwa hiyo ningependa maswali ambayo inaulizwa katika mitihani ya kitaifa, iwe ni mitihani kwanza hata mtihani wenyewe ambao unapenda nataka uwe ni wa Province.

Wanafunzi wafundishwe na syllabus katika Province hiyo hiyo na mtihani wenyewe uwe na maswali yale yale katika Province na u-markiwe katika mkoa huo huo. Kwa sababu sisi kule ambao tumeenda tumeona mambo mengi ya uonefu kabisa. Mtu ni mwanafunzi hawezi hasa kuzungumza Kiswahili na wakati huo huo mwanafunzi huyo ambaye huzungumza Kiswahili katika mtihani anaonekana mwanafunzi huyu amefaulu zaidi. Haya ni maonevu kabisa. Kwa hiyo mimi napendekeza mtihani uwe kutokana na Provinces. Kama nchi zingine za kuendelea zinavyofanya.

Sheria za nchi yetu ziandikwe tu kwa lugha ya Kiswahili. Kwa sababu wale ambao hawakupata fursa ya kusoma Kiingereza au kujua kifaransa hawawezi kuvielewa sheria hizi. Kwa hiyo wale wengine ambao hawana fursa kama hizo wanadunishwa na sheria zao. Kwa hiyo mimi napendekeza sheria ziandikwe katika lugha ya Kiswahili ambapo mwananchi wa kawaida ataweza kunufaika na kuweza kujitetea katika mahakama.

Nikirudi katika Universities. Najua hii pointi hii imezungumzwa lakini nataka kutilia mkazo. Universities hapa Kenya wakija katika kuweka ile cut out point. Utakuta wanafunzi wengine ambao wanatoka mbali hawakuweza kuenda katika vyuo vikuu vya Serikali hawakuweza kweli kwenda katika national schools, utakuta mafanikio yao sio mazuri. Ni wanafunzi wale wale ambao wamepata fursa ya kwenda katika national schools wana-perform vizuri.

Kwa sababu resources ziko kule lakini tukienda katika Kenya katika mitihani huko vyuo vikuu tunakuta wanafunzi wale wale tunaowangusha. Na wengine sisi tumeenda pengine na C+ kwa hiyo pana maonevu makubwa sana. Kwa hiyo napendekeza Tume hii kila mkoa uwe na vyuo vyao ili wale ambao hawakupata fursa ya kwenda vyuo vikuu waweze kupata fursa na ataweza kufanikiwa kama wengine.

Nipatie nafasi kama dakika moja. Pia katika hivyo vyuo vikuu katika mikoa, faculties ziwe zinaangaliwa kutokana na mahitaji ya Provinces hizo hizo. Kwa sababu itakuwa ni kitu cha kupoteza wakati, college kama hii ya Utalii. Utalii nyingi ambazo zina-benefit Serikali hii ziko katika Mkoa wa Pwani. Lakini utakuta chuo hiki cha utalii kiko bara huko. Watu wa Pwani hapa ambao wangeweza kusoma na ku-benefit zaidi, hawezi ku-benefit. Kwa hiyo ningependa vyuo kama hivi au vyuo katika Serikali viende kutokana na mahitaji ya mikoa.

Mwisho kabisa ningependekeza askari, polisi, wachaguliwe, waandikwe kutokana na district au wilaya au Province kwao wanapoishi na wawe wananchi wa kawaida. Kwa sababu sisi hapa Pwani hasa tunanyanyaswa sana. Polisi amekuja hapa hajui mila za kindigo, hajui wadigo wanafanya nini. Akija anasema 'mnafanya mambo haramu hapa, ondoka hapa'. Hii ni kitu hatutaki kabisa tunataka watu waandikwe polisi kutokana na mikoa yao ili waweze kujua mila za sehemu hiyo. Ningekuwa na mengi sana lakini wakati umekwisha.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Thank you very much Bwana Ramadhani. Juma Mohammed Mwavujo.

**Juma Mohammed Mwavujo:** Ndugu zangu mabwana na mabibi mmeshindaje?

**Audience:** Sawa sawa.

**Juma Mohammed Mwavujo:** Nashukuru kusimama hapa kwa kuzungumza mazungumzo yaliyotuleta. Kitu cha kwanza

ambayo kinatushangaza sana katika Coast. Tuseme kitu cha kwanza katika Kenya navy, Kenya navy iko upande wa Pwani lakini chuo chake kikuu kiko Nairobi college yake. Ambayo hiyo si sawa kwa sababu bahari iko Pwani. Watu wa Kenya navy wanajifundisha ku-dive kwenye bahari sio kwenye vidimbwi. Anajifundisha kuoga kwenye kidimbwi. Yule ambaye anaweza kuogelea kutoka hapa mpaka Lunga lunga anakosa kazi. Yule ambaye anaoga kwenye kidimbwi ndiye anapata kazi kwa sababu yuko kule na kitu chenyewe kiko kule lazima apate.

Basi kwa hivyo Serikali twataka ijue kwamba na sisi pia tuna watoto wetu au sisi pia tunataka hayo makazi. Kama port. Port ni shirika ambalo liko Pwani lakini hatuna uwezo wa kufanya chochote kwenye hiyo port. Na ambao sisi ndio wenyewe wa kukaribisha wale wenzetu. Lakini sasa sisi tunafanywa kukaribishwa. Hiyo ni sawa? Hiyo Serikali twataka itizame kitu kama hicho. Na mchango mwingine ni kuhusu habari ya majimbo.

Majimbo hatukuyaanza sisi, yalianza na akina Kenyatta na akina Ngala. Sasa baada ya Kenyatta alipoona kama huyu kule Lan Caster house walizungumza baada ya miaka kumi wawe kila mtu atatawala jimbo lake. Sasa alipoona hii miaka kumi kabla haijafika huyu mtu tumuue. Akamuua jamaa. Sasa ambao twatetea majimbo akina nani. Basi kwa hivyo sasa sisi hatuna kitu ambacho kitatusaidia Coast isipokuwa ni majimbo. Ni kila mtu asimamie upande wake, Serikali moja. Lakini kila jimbo lijisimamie lenyewe. Nafikiri nikisema mengi itakuwa ni usiku. Basi asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante. Salim.

**Com. Zein Abubakar:** Salim waweza kusita agano ipite?

**Salim Salim Mwabarae:** Kabisa bwana. Salam Alaikum wandugu. Mimi kwa jina naitwa Salim Salim Mwabarae na Serikali ile ninayoitaka mimi ni Serikali ya majimbo. Ili kutilia mkazo Serikali ya majimbo na mgawanyo mkuu, usawa wa rasilimali na majukumu ningependa kuwe na Rais ambaye atakuwa mkuu wa dollar na kiongozi wa Serikali ambaye atakuwa Waziri Mkuu.

Upande wa Bunge: Bunge linatakaniwa liwe huru ili kuondoa uwezekano wa Rais kuingilia uamuzi wa Bunge na mfano mzuri tunaouona ni kama mswada wa Donde uliopasishwa na bado Serikali inaingilia. Mawaziri wanatakaniwa wachaguliwe kando na Bunge. Hii itaondoa wale watu ambao kwa mfano kama hivi sasa. Watu wa vyama vya upinzani wanashikilia ama wanajijenga zaidi juu ya yule atakayegombea kiti cha urais wakitarajia kuwa atakapochukue hatamu atawapa zawadi nono kwa kuwapa uwaziri. Hii itafanya Bunge liwe huru zaidi ikiwa wabunge watabakia na kazi ya Bunge na itatoa nafasi za kazi kwa wasomi wa Kenya ambao wana uwezo wa kumudu nafasi ambazo ziko na mawaziri.

Mahakama: Ningependa mahakama ya Kenya iwe huru na ili mahakama iwe huru, mahakimu hawatakaniwi kuchaguliwa na Rais. Na ingekuwa vyema kama wangechaguana wenyewe miongoni mwao pamoja na mawakili. Kisha kuna kifungu cha affirmative action. Nafikiri Katiba yetu haikuzungumzia affirmative action. Affirmative action wengine pengine tutakuwa

tunajiuliza ni nini, hii ni hatua ya kurekebisha makusudi. Nafikiri kutoka mwaka sitini na nne kuna makusudi mengi ambayo yametendwa yakuagadamiza maeneo fulani ama watu wa aina fulani. Kwa mfano kama upande wa ardhi, 1964 wakenya baada ya kuwa kukosa ardhi na Katiba yao ilipokuwa imeandikwa iwaruhusu wazungu wauze ardhi yao kwa bei ya maridhiano, Kenya iliomba mkopo kutoka kwa Uingereza ili waafrika wapate makao.

Hivyo basi hii ikawapa fursa waliokuwa kwenye utawala hususana jamaa ama tabaka fulani kuchukua zile pesa na kununua mashamba na kuyafanya yao. Hivyo basi wale wenyeji wa maeneo yale kwa mfano kama Ukambani wakakosa makao na wakaletwa Shimba Hill na waliokuwa kama Wakikuyu wakapelekwa Mpeketoni, Mariakani na kwingineko. Ningependa hii affirmative action ichukuliwe kama wale waliopewa yale mashamba yapunguzwe idadi ya ukubwa ule wa mashamba ili wenyeji wapate ardhi ama ikiwezekana wafukuzwe au wale wadigo nao ama watu fulani ambao hawana ardhi wapelekwe mikoa kama hiyo.

Upande wa ajira: Upande wa ajira ningependa wenyeji wa eneo wanalotoka ambalo kuna rasilimali ile inayotoa ajira wawe asilimia thelathini na tano na kama kutakuwa na upungufu watu wa kutoka kando na eneo lile wasizidi asilimia kumi na tano.

Retrenchment ambayo inaendelea hivi sasa kama kikwazo kimoja cha kupewa msaada ilikuwa inafaa itilie maanani zaidi, wenyeji wa eneo lile wawe asilimia kumi na tano katika watakaopunguzwa na watu wageni kando na lile eneo wawe asilimia themanini na tano ili kuweka ule usawa zaidi. Tukiwa bado tuko kwenye ajira ningependelea watu waweze kujadili malipo kulingana na haki ya jasho lao. Na isiwe kama hivi sasa ambapo Serikali inatoa pengine mshahara wa chini zaidi uwe elfu tatu na mia mbili na themanini na tano ambao bado uko chini zaidi kulinganishwa na ile kazi mtu anayoifanya.

Upande wa utawala: Ningependa ma PC waondolewe na badala yake kuwekwe ma governor ambao watakuwa wametauliwa na wenyeji. Cheo cha DC pia chafaa kifutiliwe mbali na kazi zake zigawanywe kwa Mayor atakayechaguliwa ili kumpa uwezo zaidi wa kumiliki rasilimali za eneo lile na pia kuendesha eneo lile ili liende mbele kimaendeleo. Kwa sababu kwa sasa kwa ufupi zaidi Mayor aliyeko sasa ama ma Mayor ambao wako katika mabaraza ya miji ni watu ambao wako pale kula pesa tu za umma na hakuna la maana analofanya kwa sababu kazi zote zinaendeshwa na county.

Upande wa Serikali na utawala: Nafikiri ingekuwa vizuri zaidi kama Serikali ingeletwa karibu zaidi na raia. Kuileta Serikali zaidi na raia ni vipi? Katiba iruhusu kuwe kuna korti za kijiji zitakazoangalia makosa mandogo mandogo kwani kila watu walikuwa na mila zao na walikuwa na namna zao za kujadili makosa na namna zao za kuadhibu. Kwa hivyo ningependa Katiba itilie maanani sana mahakama ndogo za vijijini.

Upande wa vyama: Vyama ningependa viwe viwili nafikiri sababu nyingi zishasemwa na pia kuwe na uhuru wa mgombea kiti ambaye atakuwa independent kupigania.

Juu ya urekebishaji wa Katiba: Katiba haifai kurekebishwa na Bunge isipokuwa tu wanafaa watayarishe mswada ambao unafaa upasishwe na raia kupitia referrundum. Watakao endesha ino referendum yawe makundi huru ya watu na sio watu watakaochaguliwa na Rais.

Juu ya Bunge: Ningependa kwa vile Serikali itakuwa ya majimbo, iko haja ya kupunguza idadi ya wabunge. Bunge latakaniwa liwe at least na wabunge…..Bunge la taifa liwe na wabunge sita kutoka kila mkoa hivyo basi kupunguza ghalama za umma na pia kuongeza mapato kwa nchi.

Juu ya uchumi: Kila jimbo baada ya kukusanya kodi latakaniwa lipeleke asilimia kumi na tano tu kwenye Serikali kuu iwe itashughulikia foreign affairs, majeshi, dharura na mishahara ya wabunge na Rais. Asanteni.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Salim na wewe ulikuwa wa mwisho. Sijui kuna mtu mwingine hajazungumza na anataka kuzungumza. Okey. Si tumpatie wakati awe wa mwisho. Tumpatie dakika moja na nusu. Okey.

**Chesine Emenza:** Asante kwa huu muda wa kuongea.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Lakini utaje jina.

**Chesine Emenza:** Jina naitwa Chesine Emenza na pendekezo langu la mwanzo ni kuhusu Rais. Rais apewe vipimo viwili tu vya miaka mitano mitano baada ya hiyo awe tena hawezi ku-qualify kupigania tena Rais. Na jambo la pili ni kuhusu nyinyi ma-commissioners muwe empowered kwa sababu wengi wetu kuna mawazo mengi hatutaweza kuyatoa because of ignorance here and there and you should be empowered. Some of you have traveled widely and you have experiences from various countries where you can copy so that you can benefit and Kenyans can benefit. You should be empowered to borrow those useful experiences you have had from other countries where you have gone.

Halafu tatu kuhusu elimu na matajiri that is employers. Every employer must be forced to train the labour force he has engaged. There should be mandatory scholarships within where the Kenyan worker is working. Still on higher education. The loans for help from help should also be given to family holders. Because most of the beneficiaries right now are the youth. Anyone who goes above the University or does not go to the University and gets an employment somewhere down there does not benefit from health in case he wants to further his education. It relies on mostly the resources he has gained through where he is working.

Lastly but not least. Citizenship: Mkenya akioa mtu wa nje akimleta hapa Kenya yule ana experience ambayo huyu Mkenya mwingine pengine hana lakini ile law im-allow yule foreigner aliyeolewa afanye kazi hapa. Mkenya anayeolewa nchi za nje

nishaona wakenya wanaolewa nchi za nje na wanaendelea na kufanya kazi kule. Inaonekana kambe* wakenya hawatamini labour force. There are some foreigners who are married to Kenyans, they come and stay in Kenya for many years without a job. But let them go back to where they are coming from. They stay for a week and then they get a job there.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana. Ulisema hiyo ndiyo ya mwisho?

**Chesine Emenza:** One more please.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Can you wind up quickly.

**Com. Zein Abubakar:** Ndugu yangu ufanye haraka kwa sababu sisi hatuoni tena mambo tunayoyaandika.

**Chesine Emenza:** Basi wacha nishukuru pale mmenipatia. Asanteni.
**Com. Zein Abubakar:** Fanya hilo lako la mwisho. Maliza hilo la mwisho. Nasema ufanye haraka tu. Maliza la mwisho.

**Chesine Emenza:** Thank you for the time you have given me.

**Com. Zein Abubakar:** Andika jina kule. Asante. Ndugu umetambuliwa wewe?

**Shambi:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Mimi nitakupa fursa useme kwa sababu nimeshasema yale tunayoandika hatuyaoni tena. Useme tu ikiwa kuna jambo ambalo unalo wewe halijatajwa na mtu mwingine. Sijui kama tunaelewana?

**Shambi:** Lishatajwa lakini nitilie mkazo.

**Com. Zein Abubakar:** Kama nikutilia mkazo litaje tu jina lako na ulitaje jambo hilo halafu umalize. Jina lako.

**Shambi:** Jina langu naitwa Shambi. Kitu ambacho nataka kutilia mkazo ni kuhusu elimu. Elimu iwe ni ya bure na katika vile vyuo ambavyo viko katika mikoa ambayo iko kando na Pwani vile vile vitagawanywa katika kila mkoa. Kila mkoa uwe na chuo chake na taasisi zote za elimu zitagawanywa sawa kila mkoa.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa Bwana Shambi. Asante bwana. Andika jina lako kwenye register. Kama utaona lakini. Sasa mimi ningependa kuwashukuru kwa dhati kubwa kwamba mmekuwa na subira na utulivu wa kusubiri mpaka sasa na pia niwashukuru kwa maoni yenu mengi mliyoyatoa lakini ningependa kuwakumbusha yale tuliyosema asubuhi kwamba ikiwa

hukuona kwamba umetosheka na maoni uliyotoa leo au baadaye mambo yakakujia kichwani kwamba unataka kutoa maoni zaidi, una fursa ya kuandika mswada wako na kuutuma kwa ofisi zetu zilizoko pale mjini kiziwani katika national library kwa coordinator wetu. Au unaweza kututumia moja kwa moja katika anwani ya posta au ukiwa Nairobi ukatuletea katika jumba la Kencom house ghorofa ya pili.

Sasa ningependa kumuomba co-ordinator Ahmed aje hapa amuombe mmoja wetu tufanye kama tunavyofanya ada yetu kawaida. Kama lile gari linaweza kuzimwa. Kama gari laweza kuzimwa ndio tufanye maombi halafu tufunge mkutano. Mwambieni huyo mwenye gari tafadhali azime gari.

**Ahmed:** Shukrani. Kama desturi yetu mmoja angekuja tukaomba dua na tukafunga kikao chetu kwa leo. Basi tuombe dua.

**Prayer in (Islam):** Asante Shukrani.

Meeting ended at 6.00 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&